# UCHANGANUZI WA MTINDO KATIKA TAHARIRI YA GAZETI LA *TAIFA LEO*

Na

**FLORAH CHEPKORIR**

**TASNIFU HII IMETOLEWA ILI KUTOSHELEZA BAADHI YA MAHITAJI YA SHAHADA YA UZAMILI (M.A.) KATIKA IDARA YA KISWAHILI YA CHUO KIKUU CHA NAIROBI**

**AGOSTI, 2016**

# UNGAMO

Tasnifu hii ni kazi yangu binafsi na haijatolewa kwa mahitaji ya shahada ya uzamili katika chuo kikuu kingine chochote.

__________________ __________________

**FLORAH CHEPKORIR** **TAREHE**

**C50/67037/2013**

Tasnifu hii imeandikwa na kutolewa kutahiniwa kwa idhini yetu kama wasimamizi walioteuliwa na Chuo Kikuu cha Nairobi.

__________________ __________________

**DR. HEZRON MOGAMBI** **TAREHE**

__________________ __________________

**PROF. PETER M. MATU** **TAREHE**

# TABARUKU

Kazi hii naitabarukia mume wangu mpendwa Geofrey Ruto na watoto wangu wapendwa: Ian Kiplangat, Vanessa Chepchumba na Emmanuel Kipngeno. Mapenzi, usaidizi na ushauri wenu ni chemichemi ya uvumilivu na bidii katika safari hii ya kiusomi.

Kwa wazazi wangu Samwel Ngetich na Rael Ngetich; mulininipa msingi mwema, mukanionyesha njia.

Nawapenda nyote, Mungu awabariki.

## SHUKRANI

Ningependa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa siha njema na fursa nzuri ya kuendeleza masomo yangu vilivyo, bila yeye singefika nilipo sasa. Neema zake zilinifaa zaidi.

Nimeweza kutimiza kazi hii kwa ukarimu, juhudi na hisani ya watu wengi. Ningependa kuwashukuru wafuatao ambao walinifaa kwa njia moja au nyingine mpaka nikafika kiwango hiki. Sitaweza kuwataja wote ila kuwataja tu baadhi yao.

Ningependa zaidi kuwatolea shukrani wasimamizi wangu Dkt. Hezron Mogambi na Prof. Peter M. Matu, ambao waliufuatilia utafiti huu kwa makini hatua baada ya hatua na kunielekeza na kunikwamua nilikokuwa nimekwama. Uongozi na mawaidha ya busara waliyonipa yamenifungua macho katika maswala ya kiusomi kwa njia ya kipekee. Baraka nyingi ziwafikie popote walipo.

Vilevile, ningependa kuwashukuru wahadhiri wangu katika idara ya Isimu na Lugha, Chuo kikuu cha Nairobi kwa kuniandaa kiakademia hadi kufikia kuweza kukabili kazi za kitaalamu: mwenye kiti wa idara, Prof. John Habwe, Prof. Iribe Mwangi, Prof. Kinenee Wa Mutiso, Dkt. Mwenda Mbatiah, Dkt. Prisca Jerono, Dkt. Jefwa Mweri, Dkt. Zaja Omboga, Dkt. Evans Mbuthia, Dkt. Swaleh Amiri. Ninawaombea baraka nyingi kwa kazi zenu.

Vilevile, siwezi kuwasahau wenzangu tuliosoma nao darasani kwa ushirikiano mwema, tulipokuwa tunapekua vitabu na kujadili pamoja: Emily Mosota, Symon Kihara, Kimutai Kimetto, Kelvin Odero, Norah Gitonga, Chesebe Mutali, Asha, Bosire Bosibori, Faith Muriithi, Jackline Nyutu na wengine ambao sitaweza kuwataja mmoja mmoja.

Shukrani zangu vilevile ziwaendee ndugu zangu, Isaac Langat, Boaz Langat na Caleb Langat, asanteni kwa kunihimiza niendelee na masomo, mkanipa msaada nilipohitaji. Pia nawashukuru Fancy na Peninah; Fancy, ulinishika mkono nilipohitaji msaada na Peninah, ulinichangamsha na kunipa moyo niendelee. Mungu awabariki.

# ORODHA YA VIFUPISHO

**EACC** Tume ya Maadili ya Kupambana na Ufisadi
(Ethics and Anti-corruption Commission)

**FKF** Shirikisho la Kandanda Nchini (Kenya)
(Federation of Kenya Football)

**IEBC** Tume Huru ya Uchaguzi na Mipaka
(Independent Electoral and Boundaries Commission)

**IPOA** Mamlaka ya Kuchunguza Utenda-kazi wa Maafisa wa Polisi
(Independent Police Oversight Authority)

**KCSE** Cheti cha Kuhitimu Masomo ya Sekondari - Kenya
(Kenya Certificate of Secondary Education)

**KN** Kikundi Nomino

**KNEC** Barasa la Mitihani ya Kitaifa - Kenya
(Kenya National Examination Council)

**KT** Kikundi Tenzi

**NPSC** Tume ya Kitaifa ya Huduma kwa Polisi
(National Police Service Commission)

**NTSA** Halmashauri ya Kitaifa ya Usafiri na Uchukuzi
(National Transport and Safety Authority)

**NYS** Huduma ya Vijana kwa Taifa
(National Youth Service)

**S** Sentensi

**TSC** Tume ya KuajiriWalimu
(Teachers Service Commission)

# IKISIRI

Tasnifu hii inatoa matokeo ya uchanganuzi wa mtindo katika tahariri ya gazeti la *Taifa Leo.* Utafiti huu ulinuia kuchanganua uteuzi wa maneno, virai na miundo ya sentensi iliyotumiwa na mwandishi wa tahariri ya *Taifa Leo*. Pia, uchunguzi wa mbinu za lugha na tamathali za usemi ulifanywa. Tahariri za miezi ya Januari hadi Machi zilikusanywa na kuchunguzwa, kisha tahariri 30 zikateuliwa; zile zilizosheheni mbinu za lugha na tamathali za usemi na mtindo wa pekee katika uteuzi wa maneno. Nadharia ya Umitindo ilitumiwa katika uchunguzi huu. Matokeo ya uchunguzi huo yalibainisha kuwa tamathali za usemi zinazotumika kwa wingi ni tashbihi, misemo/nahau na sitiari, zingine ni kinaya, maswali ya balagha, tashihisi, kwelikinzani na taswira. Pili, matokeo yalibainisha kuwa, mwandishi anateua maneno na virai, anatumia takwimu na miundo ya sentensi inayowasilisha ujumbe unaoonyesha mwelekeo na mtazamo wake. Matokeo pia yalibainisha kuwa mhariri anatumia lugha nyepesi inayoeleweka na wasomaji bila kusababisha utata wowote. Sifa zifuatazo za tahariri ya gazeti la *Taifa leo* zilidhihirika: mwandishi wa tahariri ya *Taifa Leo* anatumia mada zinazotoa muhtasari wa ujumbe uliomo, mhariri anaonyesha msimamo wake kuhusu suala linalozungumziwa kwa kuteua maneno kwa njia maalum, tamathali za usemi zinazoeleweka kwa urahisi hutumiwa kupamba lugha, takwimu zinatumika ili kudhihirisha usahihi wa ujumbe, na mwisho mhariri hushughulikia mambo yanayoathiri wanajamii na kusema kwa niaba yao.

## YALIYOMO

UNGAMO....................ii
TABARUKU.................... iii
SHUKRANI....................iv
ORODHA YA VIFUPISHO....................v
IKISIRI....................vi

**SURA YA KWANZA: UTANGULIZI** ....................1
1.1Usuli wa mada....................1
1.2 Tatizo la utafiti....................4
1.3 Malengo ya utafiti....................4
1.4 Nadharia tete....................4
1.5 Sababu za kuchagua mada....................5
1.6 Upeo na mipaka....................5
1.7 Misingi ya kinadharia....................6
1.7.1 Mtindo....................6
1.7.2 Nadharia ya umitindo....................7
1.7.3 Historia ya maendeleo ya umitindo....................8
1.7.4 Misingi ya nadharia ya mitindo au umitindo....................9
1.7.5 Viwango katika uchanganuzi wa mitindo....................10
1.7.6 Mambo muhimu ya kuchunguza kutegemea nadharia ya mitindo....................10
1.8 Yaliyoandikwa kuhusu mada....................12
1.8.1 Yaliyoandikwa kuhusu nadharia....................14
1.9 Njia za utafiti....................14
1.9.1 Ukusanyaji data....................14
1.9.2 Uchanganuzi wa data....................15

**SURA YA PILI: DHANA YA TAHARIRI**....................16
2.1 Utangulizi....................16
2.2 Tahariri....................16
2.3 Historia ya gazeti....................16

2.3.1 Historia ya *Taifa Leo* .......... 16
2.3.2 Historia ya tahariri .......... 17
2.4 Aina za tahariri .......... 18
2.5 Majukumu ya tahariri .......... 19
2.6 Sifa za tahariri .......... 22
2.7 Uhusiano kati ya tahariri na habari .......... 24
2.8 Mada za tahariri .......... 25
2.9 Muundo wa tahariri .......... 26
2.9.1 Mada ya tahariri .......... 26
2.9.2 Utangulizi .......... 26
2.9.3 Mwili .......... 27
9.3.4 Hitimisho .......... 27

**SURA YA TATU: SUALA LA LUGHA TEULE NA MIUNDO YA SENTENSI ...... 30**
3.1 Utangulizi .......... 30
3.2 Udhamiriaji .......... 30
3.2.1 Matumizi ya vitenzi .......... 30
3.2.2 Vitenzi vya kuripoti .......... 36
3.2.3 Vielezi .......... 37
3.2.4 Virai .......... 39
3.3 Toni .......... 42
3.3.1 Toni ya huzuni .......... 42
3.3.2 Toni ya kukashifu .......... 43
3.3.3 Toni ya kukata tamaa .......... 43
3.3.4 Toni ya kusikitisha .......... 44
3.3.5 Toni ya kuwa na matumaini .......... 44
3.3.6 Toni ya kupongeza .......... 45
3.4 Sentensi .......... 45
3.4.1 Sentensi sahili .......... 46
3.4.2 Sentensi ambatano .......... 47
3.4.3 Sentensi changamano .......... 48
3.5 Sajili za lugha .......... 49
3.6 Matumizi ya takwimu .......... 51

3.7 Uteuzi wa mada ..... 54
3.8 Hitimisho ..... 56

**SURA YA NNE : MBINU ZA LUGHA NA TAMATHALI ZA USEMI** ..... 57
4.1 Utangulizi ..... 57
4.2 Tamathali za usemi ..... 57
4.3 Misemo/Nahau ..... 58
4.4 Sitiari ..... 62
4.5 Tashbihi ..... 66
4.6 Maswali ya balagha ..... 68
4.7 Kweli kinzani ..... 69
4.8 Tashihisi ..... 70
4.9 Taswira ..... 71
4.10 Kinaya ..... 72
4.11Hitimisho ..... 75

**SURA YA TANO: MUHTASARI, MATOKEO NA MAPENDEKEZO** ..... 76
5.1 Utangulizi ..... 76
5.2 Muhtasari ..... 76
5.3 Matokeo ..... 77
5.4 Mapendekezo ..... 78
MAREJELEO ..... 79
VIAMBATANISHO ..... i

# SURA YA KWANZA: UTANGULIZI

## 1.1 Usuli wa mada

Magazeti yana nafasi yake katika jamii hata baada ya maendeleo ya kiteknolojia. Teknolojia imewezesha jamii kupata habari kwa njia nyingi kama vile televisheni, redio, kwenye mtandao; kupitia kwa simu na tarakilishi. Hata hivyo, magazeti yanahifadhi nafasi yake ya kipekee katika kupasha habari, matangazo ya kibiashara, nafasi za kazi na mengine.

Kazi hii inachunguza lugha na mtindo unaotumiwa katika uandishi wa tahariri ya gazeti la *Taifa Leo*. *Taifa Leo* ni gazeti la kila siku linalochapishwa na Kampuni ya Nation Media Group, na kusambazwa kote nchini Kenya. Nation Media Group ina magazeti matano yanayochapishwa na kusambazwa: *Daily Nation, Sunday Nation, Taifa Leo*, *Taifa Jumapili* na *East African*.

Lugha ni chombo kinachomwezesha binadamu kuwasiliana na watu wengine. Tunapotumia lugha, ya kimazungumzo na ya kimaandishi, lengo letu ni kupasha ujumbe kwa mpokezi. Jumbe zinazopitishwa zinaweza kuwa za kujulisha, kutahadharisha, kuhimiza au hata kushawishi. Wanahabari hufunzwa kutumia lugha kwa njia ya pekee ambayo inaweza kuendeleza jamii au inaweza kutenganisha jamii iwapo lugha haitatumiwa vizuri. Ni jambo lisilopingika kuwa lugha katika kila nyanja ya binadamu huwa na sifa za kiisimu ambazo hufanya lugha hiyo kuwa tofauti na nyingine.Taaluma ya uanahabari haijaachwa nyuma.

Mogambi (2011) anaeleza kuwa ukuaji wa uanahabari nchini Kenya umeathiriwa na watu wanaopatikana katika eneo husika (population composition), na athari zingine zitokazo nje kama vile ukoloni, utandawazi na sera za kitaifa ambazo zinaidhinishwa na dola. Sera mojawapo ya lugha imeweka Kiswahili kuwa lugha ya taifa na pia lugha rasmi nchini Kenya. Jambo hili limeipa hadhi lugha ya Kiswahili. Gathigi (2009) katika Mogambi (2011) anasema kwamba, katika mawasiliano ya uanahabari, lugha ni suala muhimu kwa kuamua idadi ya watu wanaoweza kufikiwa na njia fulani ya mawasiliano. Katika muktadha huu, gazeti la *Taifa Leo* linatumia lugha ya Kiswahili kufikia hadhira yake; Wakenya wengi wanatumia Kiswahili katika mawasiliano yao, kwa hivyo hawatapata ugumu wowote kusoma gazeti hilo.

Katika muktadha wa magazeti, matumizi ya lugha ni muhimu sana kwa kuwasilisha ujumbe unaonuiwa. Katika uandishi wa tahariri lugha ina majukumu mawili: kupasha habari na kushawishi msomaji. Hudgson (1996) anasema kuwa, uteuzi wa maneno ni muhimu sana kwa mchakato wa kushawishi na uwasilishaji, mwandishi anatumia maneno kuchezea hisia za msomaji, kuipa kazi hiyo umaridadi na mdundo. Urefu wa maneno na matumizi ya vivumishi vinasaidia mwandishi kujieleza kwa utaratibu anaotaka. Kulingana na Hudgson (1996), mwandishi anaweza kutumia lugha kufikia hisia za wasomaji au anaweza kutumia lugha kufikia malengo yanayohitajika.

Kwa nini gazeti kuwa na tahariri? Kulingana na *The Washington Post* (2003), katika miji ya Roma ya zamani, sehemu hii ya tahariri ilikuwa ya umma au kama sokoni ambapo watu walikusanyika kwa ajili ya shughuli za mahakamani na biashara ya umma. Tahariri ya kisasa inatoa nafasi nzuri ya kidiskosi. Tahariri zinasisimua mijadala na mazungumzo.

*The Washington Post*, (2003) inaendelea kueleza kuwa siku hizi, wasomaji hutarajia habari zisizo na maoni. Wananchi wakitaka kujulishwa habari, wanatarajia uwasilishi usiokuwa na upendeleo. Magazeti ya hapo awali yalikuwa ya kuegemea upande mmoja huku yakionyesha maoni yaliyoegemea upande wa wenyeji wa gazeti hilo. Kufikia katikati ya karne ya 19, maoni yalisongeshwa sehemu ya ukurasa wa tahariri. Inachukuliwa kwamba Hurace Greeley ndiye mwanzilishi wa ukurasa wa tahariri ya kisasa ya Marekani.

Tahariri ni maelezo yanayotoa maoni ambayo yana msingi wake kwenye jumbe za ukweli. Tahariri ni maoni yanayoandikwa na jopo la wahariri ambao wanawakilisha gazeti kama taasisi kwa ujumla, pamoja na mchapishaji.

Belmonte (2008) anaeleza kuwa, tahariri ni aina ya makala kwenye gazeti inayotoa maoni, yanayokusudiwa kushawishi msomaji. Richardson (2007) anasema kuwa sifa moja ya tahariri ni kuwa haiwezi kuwa ya kiutobinafsi. Hii inamaanisha kuwa kila mara wahariri hutoa maoni yao katika makala wanayoandika, mbali na kutupasha habari. Maoni hayo hubeba hisia zao, mitazamo na hata mapendekezo yao kuhusu maswala yanayojadiliwa.

Elyazale (2014) akimnukuu Sinclair (1995) anasema, tahariri ni makala katika gazeti yanayotoa maoni ya mhariri au mchapishaji kuhusu mada au habari iliyogusiwa kwenye gazeti hilo. Anaeleza kuwa tahariri huwa na maneno kati ya 200 hadi 500 na hupatikana katika sehemu maalum kwenye gazeti. Tahariri ya *Taifa Leo* hupatikana katika ukurasa wa 10 wa gazeti hilo na ukurasa wa 16 katika gazeti la *Taifa Jumapili*.

Koubali (2007) anataja aina za tahariri kama: tahariri ya taasisi, barua kwa mhariri na tahariri za kibinafsi. Tahariri yoyote ile ni matini ya kutoa maoni ambapo mwandishi anakusudia kushawishi msomaji kuhusu jambo fulani. Koubali anaeleza kuwa tahariri ya taasisi huwa zinaandikwa na wanajopo wa uhariri na kwa hivyo humulika itikadi ya gazeti hilo. Wahariri katika kuandika tahariri huwa kiwakilishi cha sauti iliyo rasmi.

Wahariri huwa na sifa ya kushawishi na kuwa na upendeleo, wanachukua mwelekeo fulani unaoonyesha msimamo wa gazeti hilo. Tahariri huandikwa kuhusu mada mbalimbali, ukweli na uhalisi wa mambo huwasilishwa kwa njia mbalimbali. Mhariri anachagua mada na kuamua mwelekeo atakaochukua.

Kulingana na Van Dijk (1988) tahariri zina sifa zifuatazo: ujumbe kutolewa kwa mukhtasari, kutathmini na hitimisho la kipragmatiki. Van Dijk anasema kuwa, muhtasari hutolewa ili kumkumbusha msomaji jambo linalozungumziwa. Pili, tahariri hutoa tathmini ya jinsi mambo yalivyo na tatu, tahariri hujaribu kutoa suluhisho kwa maswali kama, nini kitakachofuata? Jambo gani lapaswa kufanywa?' Tahariri hulenga kutoa masuluhisho kwa maswali yaliyojitokeza. Masuluhisho hayo yanatolewa kwa njia ya kivitendo; kile gazeti linafikiria kwamba yapaswa kufanywa.

Kutokana na maelezo ya wataalamu hapo juu, ni dhahiri kwamba tahariri ina nafasi yake na majukumu ya kutekeleza katika gazeti husika. Ni vipi tahariri ya gazeti la *Taifa Leo* linavyoshughulikia maswala muhimu katika jamii yake?

## 1.2 Tatizo la utafiti

Tatizo la utafiti wa kazi hii ni kuchanganua mtindo katika uandishi wa tahariri ya gazeti la *Taifa Leo*. Gazeti la *Taifa Leo* linatumia lugha ya Kiswahili ambayo ni lugha rasmi na pia lugha ya Taifa nchini Kenya. Mbali na gazeti hili kuwapasha habari na kuwaburudisha wasomaji wake, kuna ukurasa wa tahariri ambao ndio sauti rasmi la gazeti hilo (Koubali 2007). Wahariri wa gazeti wana jukumu la kupitisha maoni yanayogusia maswala nyeti katika jamii. Je, wahariri wa gazeti hili hutumia mtindo gani ili kuwafikia wasomaji wake ambao ni wananchi wa kawaida? Ni jinsi gani wahariri wanavyoteua lugha katika kiwango cha leksika na sintaksia ili kupitisha ujumbe unaoathiri msomaji kwa njia ambayo mhariri amenuia? Ni vipi anavyoteua mada za tahariri? Maswali haya ni muhimu kujibiwa katika muktadha wa kazi hii.

## 1.3 Malengo ya utafiti

Lengo kuu la utafiti huu ni kutambua mitindo ya lugha inayotumiwa na mwandishi wa tahariri ya *Taifa Leo,* malengo maalum ni yafuatayo:

a) Kubainisha jinsi mhariri anavyoteua maneno na kuyatumia kwa lengo maalum.
b) Kubainisha mbinu za lugha na tamathali za usemi zinavyojitokeza katika tahariri ya *Taifa Leo.*
c) Kubainisha sifa za lugha ya uandishi wa tahariri ya *Taifa Leo*.

## 1.4 Nadharia tete

a) Uteuzi wa maneno unafanywa kwa njia maalum inayokusudiwa na mwandishi.

b) Mbinu mahsusi za lugha zinatumiwa na mhariri wa gazeti la *Taifa Leo* ili kufanikisha ujumbe wake.

c) Lugha ya uandishi wa tahariri ya *Taifa Leo* ina sifa za kipekee zinazolitambulisha gazeti hili.

## 1.5 Sababu za kuchagua mada

Tahariri ni sehemu ya gazeti ambayo ni muhimu sana. Hii ni sehemu inayobeba maoni na msimamo wa jumba au taasisi ya gazeti hilo. Sehemu hii ya tahariri inazua mambo yanayoweza kufanyiwa mijadala na kutoa mwongozo wa kitaaluma kuhusu mambo tata yanayowasumbua wanajamii (Ate, 2008). Kazi hii inalenga kuchunguza jinsi waandishi wa tahariri ya *Taifa Leo* wanavyotumia lugha kuwasiliana na wasomaji wake.

Baadhi ya wasomi wamefanya utafiti kwenye gazeti ya *Taifa leo*. Uchunguzi mojawapo unaoshugulikia gazeti la *Taifa Leo* ulifanywa na Omari na Meitamei (2014). Katika utafiti wao walichunguza jinsi *Taifa Leo* linatumiwa kama kifaa cha kufunzia Kiswahili katika shule za sekondari nchini Kenya. Utafiti wao ni tofauti na wetu kwa sababu sisi tumechagua sehemu ya tahariri na kuchunguza mtindo na matumizi ya lugha.

Utafiti mwingine umefanywa na Otuoma (2015) kuhusu vibonzo katika gazeti la *Taifa Leo.* Utafiti huu ulichunguza maudhui kwenye vibonzo vinavyohusu ugatuzi. Matokeo ya uchunguzi huu yalibaini kuwa maudhui ya ufisadi na siasa yanatawala katika vibonzo husika, pia matumizi ya tamathali za lugha yanatawala katika lugha ya vibonzo. Utafiti wetu ni tofauti na wa Otuoma kwa sababu tunachunguza sehemu ya tahariri. Kwenye ukurasa wa tahariri, mhariri hutumia maneno pekee ilhali katika vibonzo, maneno huandamana na picha ili kuwasilisha ujumbe.

Katika usomaji nimegundua kuwa kuna pengo la kiusomi linalohitaji kuzibwa. Uhakiki wa kimtindo katika tahariri ya gazeti la *Taifa Leo* utawafaa wasomaji na watafiti wengine na kuchangia pakubwa katika somo la Isimujamii.

## 1.6 Upeo na mipaka

Utafiti huu unashughulikia mtindo kama unavyotumiwa na mhariri wa gazeti la *Taifa Leo*. Tulishughulikia tahariri ya gazeti la *Taifa Leo* na *Taifa Jumapili*. Uchanganuzi wa kimtindo ulifanyiwa tahariri ya miezi ya Januari hadi Machi, 2016. Miezi hii mitatu ilitupa tahariri za hivi punde na ndizo zilizofaa kwa uchanganuzi wetu. Tulichunguza matumizi ya lugha na mtindo wa kuwasilisha ujumbe yakiwemo: rejesta za lugha, miundo ya sentensi, aya, uteuzi wa maneno, tamathali za usemi na

mbinu zingine za lugha. Utafiti huu haukuangazia maudhui yanayojadiliwa katika tahariri husika bali ulichunguza jinsi lugha na mtindo umetumiwa kupitisha ujumbe na maoni ya mwandishi. Vilevile, utafiti huu uliongozwa na nadharia ya Umitindo. Nadharia hii imetuwezesha kuchanganua tahariri kwa njia iliyo mwafaka.

## 1.7 Misingi ya kinadharia

### 1.7.1 Mtindo

Mtindo unaweza kuhusishwa na lugha iliyoandikwa, lugha ya kifasihi na isiyokuwa ya kifasihi ingawa kwa kawaida unahusishwa na matini za kifasihi zilizoandikwa. Katika uandishi wa fasihi, mtindo hutumiwa kwa maana nyingi: ni mazoea ya lugha kama wanavyosema wana-umitindo Crystal na Davy (1969). Mtindo huweza kuhusisha mazoea ya lugha ya mtu binafsi au jamii-lugha. Hii ndiyo maana ambayo huwajia watu akilini wanapozungumza kuhusu mtindo wa uandishi wa mtu fulani, mtindo wa kuzungumza, wa kutoa hotuba hadharani. Mtindo ni upekee wa kujieleza katika maandishi au mazungumzo. Ni jinsi waandishi huandika na pia ni njia tofauti za watu wanavyozungumza au kuandika katika miktadha ya kawaida ya kila siku. Kulingana na Miles (1971), mtindo na umbuji ni kama uteuzi wakisanii wa kibinafsi wa kila mtunzi.

Syambo na Mazrui (1992), wanaeleza kwamba mwandishi mzuri wa fasihi ni yule anayeweza kutumia msamiati, tamathali za usemi na miundo mingine ya lugha kumfanya msomaji awe na hisia fulani.

Leech (2007) anaeleza kuwa mtindo kwa fasiri ya kijumla, ni jinsi lugha inavyotumika katika muktadha fulani, inavyotumiwa na mtu kwa madhumuni fulani. Leech anasisitiza kuwa kwa kawaida mtindo huhusishwa zaidi na matini ya fasihi andishi. Mtindo unaelezwa kuwa sifa za lugha inayotumiwa.

Mjadala umekuwepo kuhusu mtindo, swali likiwa; ‘mtindo unarejelea nini au nani’? Kwa upana, mtindo unaweza kurejelea yaliyoandikwa na pia yaliyosemwa, ya fasihi na aina zote za lugha zinazitumiwa siku baada ya siku ( Leech & Short, 1981).

### 1.7.2 Nadharia ya umitindo

Kulingana na Leech (1969), nadharia ya Umitindo ina viwango ambavyo humwezesha mchanganuzi wa matini ya kifasihi kuvizingatia ili kutekeleza uhakiki kwa njia ifaayo. Leech anaorodhesha aina za ukiushi wa kaida za matumizi ya lugha ambao hutokea katika mtindo wa kazi za kifasihi. Viwango vya ukiushi ni hivi vifuatavyo:

(i) Ukiushi wa kimsamiati/ kileksia

(ii) Ukiushi wa kisarufi

(iii) Ukiushi wa kilahaja

(iv) Ukiushi wa sajili

(v) Ukiushi wa kifonolojia

(vi) Ukiushi wa kimaandishi/ kigrafolojia

(vii) Ukiushi wa kimapisi/ kihistoria

(viii) Ukiushi wa kisemantiki

Uchanganuzi wa mtindo katika tahariri utazingatia: ukiushi wa kimsamiati, ukiushi wa kisarufi, ukiushi wa sajili, ukiushi wa kigrafolojia na ukiushi wa kisemantiki. Lyons (1981) anaeleza umitindo kuwa ni uchunguzi wa ubadilishaji wa mtindo katika lugha na jinsi ambavyo` watumiaji wake wanavyotumia. Naye Finch (2000), anaeleza umitindo kama tawi la isimu inayotumia njia za kiisimu kuchanganua dhana ya mtindo katika lugha.

Agu (2008) anasema kwamba uchunguzi wa kimtindo unajumlisha uchunguzi wa sintaksia, uteuzi wa maneno, nahau, taswira na mengine. Anaeleza kuwa, katika kiwango cha kisintaksia, inahusisha miundo ya sentensi. Uteuzi wa maneno na jinsi anavyoyapanga ili kufanikisha malengo yake ya kisanii. Umtindo pia unahusisha matumizi ya tamathali za usemi. Kulingana na Agu aina hii ya lugha hutumiwa ili kuipa kazi iliyoandikwa uzuri, kuweza kutumia maneno machache ipasavyo na

kupata uzito wa maudhui. Maelezo ya wananadharia hawa yanafaa kwa kutupa mwelekeo ili kuweza kuchanganua mtindo katika tahariri.

Wamitila (2003:39) anasema yafuatayo kuhusu umitindo:

> Dhana hii hutumiwa kurejelea taaluma inayohusu uchunguzi wa lugha na uchanganuzi wa jinsi mbalimbali za kuelezea matukio katika kazi za kifasihi. Ni taaluma iliyoko kati ya uchunguzi wa lugha na uchunguzi wa fasihi au jinsi lugha inavyotumiwa katika matini au kazi za kifasihi. Elimumitindo huweza kuhusisha uchunguzi wa sifa za kimtindo zinazojitokeza katika kazi fulani na zinazomtambulisha mwandishi anayehusika.

Kutokana na ufafanuzi huu, Wamitila anaeleza nadharia hii kama Elimumitindo, lakini baadaye katika mwaka wa 2008, anaiita nadharia ya Umitindo. Wamitila (2008) anatoa ufafanuzi wa kina kuhusu nadharia ya umitindo. Anasema kuwa, Umitindo hutumiwa kurejelea mkabala wa uchanganuzi unaohusisha manufaa ya isimu na huweza kuelezwa kama nadharia ambayo iko katikati ya isimu na fasihi. Kimsingi, nadharia hii ina mwelekeo wa kifani na inadhamiria kuchunguza mtindo wa matini za kifasihi.

Mkabala wa umitindo uliwekwa msingi na mawazo yanayohusishwa na wana-urasimu hasa maandishi ya Roman Jacobson na mawazo ya wana-umuundo. Umitindo unaweza kuchunguza mtindo wa kinachosema au kuwasilishwa na jinsi kinavyowasilishwa au fani na maudhui (Wamitila, 2008).

### 1.7.3 Historia ya maendeleo ya umitindo

Leech na Short (2007) wanaeleza kuwa umitindo ni tawi la Isimu inayochunguza njia zote za kujieleza zinazopatikana kwenye lugha fulani**.** Wanaeleza kuwa neno umitindo lilishuhudiwa mara ya kwanza katika '*The Oxford English Dictionary'* mwaka wa 1882, likimaanisha (umitindo ) sayansi ya mtindo wa fasihi, uchunguzi wa sifa za kimtindo.

Msingi wa nadharia ya umitindo kulingana na Wamitila (2008) ni nadharia ya balagha. Nadharia ya balagha ilikuzwa na kuendelezwa katika jadi ya Kiyunani na

Kirumi ambayo ilidhamini jinsi ya kuzungumza au kuwasilisha ujumbe kwa njia ya kimaandishi, balagha ina makundi matatu makuu:

a) Balagha ya kisheria/kilengo
b) Balagha ya kiutetezi/kihukumu
c) Balagha ya kushawishi/kisifa/kisherehe
Kimsingi balagha ilidhamiriwa kufundisha njia zifaazo za kushawishi umma lakini ilikua na kuishia kuwa uwanja maalum wa kitaaluma. Msisitizo mkubwa wa balagha ulikuwa kwenye mazungumzo yafaayo na ulumbi (wa kushawishi) kwa njia hii balagha ilichukua mkabala wa kupendekeza njia zifaazo za usomaji na ulumbi. Taaluma hii iliainisha na kuchunguza elementi za kimsingi za lugha za binadamu. Kwa njia hii, taaluma hii iliuweka msingi wa taaluma ya isimu na uwanja wa uhakiki kama unavyojulikana hivi leo.

Mkazo wa nadharia hii ni sanaa ya usemaji au balagha au jinsi ya kuwasiliana. Msingi wake mkuu katika uchunguzi wa matini au kazi za kifasihi ni kuchukulia kazi au matini ya fasihi kama sauti ya binadamu.

Nadharia hii inashughulika na wepesi au uchagamano katika sanaa hiyo ya usemaji kwa kuangalia maneno, virai na ruwaza za sentensi na ufaafu wake katika matumizi yake. Uchunguzi huu unahusisha basi kubainisha mbinu za kibalagha na kisemaji ambazo hutumiwa na mzungumziwa ili kufanikisha ujumbe na mawasiliano yake na mlengwa au hadhira yake.

**1.7.4 Misingi ya nadharia ya mitindo au umitindo**

Wamitila (2008) anaeleza kuwa nadharia hii ya umitindo inajikita kwenye uchunguzi wa lugha kwa kiasi kikubwa. Uchunguzi huu wa lugha unapania kubainisha ubunifu uliopo na kuutekeleza kwa undani na unasaidia katika uelewekaji wa matini au kazi za kufasihi.
Mkabala wa mitindo unadhamiria kuzichunguza matini za kifasihi kwa kuuchunguza mtindo kwa njia ya kisayansi - yenye nidhamu na taratibu za kitaaluma.

Uchunguzi wa mitindo unaweza kuangaliwa kwa kuchunguza mikabala miwili. Kwanza, upo mkabala wa jadi ambao unatenganisha baina ya yaliyosemwa (maudhui au yaliyomo ambao pia huweza kuelezwa kijuujuu kama ujumbe au maana ya kifasihi) na jinsi yalivyosemwa (fani). Mtindo unachunguza jinsi ujumbe au maana hiyo inawasilishwa kwa matumizi ya njia na mbinu tofauti ambazo zinadhamiriwa kuwa na athari fulani ya kiujumi kwa mlengwa au msomaji.

Wamitila (2008) anaongeza kwamba, maarifa yanayotokana na isimu hutumiwa ili kubainisha sifa za kimtindo za kazi au matini ya kifasihi. Sifa hizi zinaweza kuwa za kifonolojia (ruwaza za sauti, vina mizani), kisintaksia (miundo ya sentensi, aina ya sentensi, za kimsamiati maneno dhahania na maneno dhabiti, kuwepo kwa idadi ya nomino, vielezi, vivumishi n.k) na kibalagha (matumizi ya tamathali za usemi, urudiaji na mbinu za urudiaji huo, jazanda n.k).

### 1.7.5 Viwango katika uchanganuzi wa mitindo

Ili kuweza kutumia nadharia ya mitindo kwa njia ifaayo, inahalisi kubainisha viwango kadhaa ambavyo mchanganuzi wa matini ya kifasihi anapaswa kuviangalia ili aweze kutekeleza kazi yake kwa njia ifaayo (Wamitila, 2008).

Viwango hivi ni:

a)Kiwango cha kimaandishi(grafolojia)

b)Kiwango cha kifonetiki

c)Kiwango cha kimofolojia

d)Kiwango cha kisintaksia

e)Kiwango cha kisemantiki

f)Kiwango cha kiusemi/kidiskosi

### 1.7.6 Mambo muhimu ya kuchunguza kutegemea nadharia ya mitindo

Wamitila (2008) anatoa mwongozo kuhusu mambo muhimu ambayo yatatuongoza katika uchanganuzi wa mtindo wa tahariri: uteuzi/suala la lugha teule, sarufi na tanzu/mtindo, lugha ya kitamathali na miundo ya lugha, mtazamo na mtindo, na lugha na itikadi.

#### 1.7.6.1 Uteuzi /suala la lugha teule

Matumizi ya lugha yoyote ile huhusisha uteuzi wa maneno au msamiati unaotumiwa. Uteuzi wa maneno ni muhimu kwa kuwa huwa mojawapo wa kitambulishi kikuu cha matini au kazi ya kifasihi (Wamitila, 2008). Ni muhimu kudokeza kwamba, mwandishi anaweza kufanya uteuzi ambao ana ung'amuzi wake (yaani anajua kuwa anafanya uteuzi huo) au akaufanya uteuzi ambao hauna ung'amuzi wake.

#### 1.7.6.2 Sarufi na tanzu/mtindo

Sarufi ambayo inajumlisha viwango vya kimofolojia na kisintaksia huangaliwa kama msingi mkuu wa lugha ambao unadhibiti matumizi ya lugha yenyewe. Kwa kuwa lugha ndiyo nyenzo kuu katika kazi za kifasihi, basi sifa na matumizi yake huwa na athari kubwa katika uchanganuzi wa matini za kifasihi. Wamitila (2008) anaongeza kuwa, sifa nyingine muhimu katika uchunguzi wa kisarufi ni suala la udhamiriaji (modality). Udhamiriaji hurejelea njia za kiisimu zinazotumiwa kuvumishia au kuelezea nia aliyo nayo mtumiaji wa lugha. Udhamiriaji unaweza kuwa wa:

Uwezekano - Huenda Juma yuko Mombasa.

Umazoea - Omari hupenda kulalamika sana.

Unuiaji - Hamu anawazia kumnunulia mkewe zawadi.

Ulazima - Rais hana budi kumwachisha kazi Waziri wa Fedha.

Vitenzi vilivyopigiwa mstari vinatuelekeza kwenye udhamiriaji wa msemaji na huweza kuelezwa kama vitenzi vya udhamiriaji (modal verbs).

#### 1.7.6.3 Lugha ya kitamathali na miundo ya lugha

Lugha ya kitamathali ni sifa muhimu ambayo inapasa kuchunguzwa katika matini. Tunapotumia nadharia ya mitindo, uchunguzi huu unapaswa kubainisha umuhimu wa lugha hiyo ya kitamathali katika kazi au matini inayohusika. Mchunguzi anapaswa pia kuchunguza miundo, urefu au ufupi wa sentensi, usahili na uchangamano wa sentensi na labda kubainisha ni zipi zinazochukua nafasi kubwa.

#### 1.7.6.4 Mtazamo na mtindo

Mzungumzaji au mwandishi yeyote huchukua mkabala fulani kuhusu anayoyasema au kuyazungumzia. Mtazamo huu unaweza kuwa na mchango mkubwa kwenye upokezi wa maneno anayoyasema au jinsi mlengwa anavyoyaelewa. Hii ina maana kuwa mtazamo ni dhana muhimu sana katika uchanganuzi wa mitindo ya kazi ya kifasihi.

#### 1.7.6.5 Lugha na itikadi

Mchanganuzi wa kimtindo hana budi kuchunguza mwelekeo wa kimsimamo au kimawazo, yaani itikadi, unaochukuliwa na msimulizi au mwandishi. Lugha inayotumika ni nyenzo muhimu ya kubainisha au hata kuchimuza itikadi hiyo. Mchanganuzi wa kimtindo atachunguza jinsi ukuzi wa maneno au uteuzi wa kiisimu na mipangilio au ruwaza zake kwa ujumla unavyochangia katika kuiangaza itikadi hiyo.

## 1.8 Yaliyoandikwa kuhusu mada

Susinskiene (2010) alichunguza  mbinu ya kunominisha vitenzi katika magazeti ya *The Gurdian, The Times,* na *The Daily Telegraph.* Unominishaji huhusishwa na matini ambazo huhitaji maneno machache huku yakipitisha ujumbe mzito. Kress (1983) anasema kuwa matendo ya muhimu yanatajwa kama nomino (yananominishwa) ili kumwondoa mtendaji na kumwacha msomaji katika taharuki. Kwa kutaja kitendo kwa njia ya unominishaji, haitajulikana wakati gani na kwa hivyo habari hizo zinaweza kwenda na wakati. Unominishaji ni mbinu ya kiisimu na kwa wakati huo huo inatumiwa kama mbinu ya kuleta mshikamano kwenye matini husika (cohesive device). Unominishaji pia huturuhusu kudondosha watendaji na wakati.

Bonyadi (2011) alifanya uchunguzi linganishi  wa tahariri za magazeti mawili ya Kiingezera, moja la Marekani, *The New York Times* na  pili, la  Kiajemi, *Tehran Times.* Madhumini ya uchunguzi huo ni kutambua jinsi tahariri hizo zinavyodhihirisha matumizi ya udhamiriaji. Matokeo yalionyesha kwamba mhariri

alitumia vitenzi vya udhamiriaji (auxiliary modal verbs) kama 'itakuwa' (will) ama 'ingekuwa' (would) kuliko alivyotumia aina zingine za vitenzi vya udhamiriaji. Pia, wingi wa matumizi ya vitenzi vya kubashiri inaonyesha kuwa lengo kuu la mwandishi wa *New York Times* ni kutambua kile kinachowezekana kufanyika. Kwa upande mwingine mwandishi wa *Tehran Times,* alitumia vitenzi vya kuonyesha ulazima kwa wingi kuliko *New York Times,* kwa hivyo mhariri wa *Tehran Times* anashughulika zaidi na kile kinachopaswa kufanywa.

Wekesa (2012) alichunguza iwapo tahariri zinaweza kutimiza mahitaji ya uandishi yanayoibua hisia za msomaji (rhetorical demands). Matokeo ya utafiti huo ni kwamba, tahariri za magazeti ya Kenya (yanayotumia lugha ya Kiingereza), yanafuata muundo wa kiagumenti (argument structure) na kwamba uhusiano wa vishazi unaashiria sehemu za miundo mbalimbali ya tahariri hiyo. Tofauti na utafiti wa Wekesa, kazi yetu inashughulikia mtindo katika tahariri ya *Taifa Leo*.

Ontieri na Meitamei (2014 ) walitafiti kuhusu jukumu la gazeti la *Taifa Leo* kama kifaa cha kufundishia Kiswahili katika shule za sekondari. Walidhibitisha kwamba Gazeti la *Taifa Leo* linaweza kutumiwa kufunza maswala ya njeo, upatanisho kati ya nomino na kitenzi, uakifishaji, uyakinishaji, ukanushaji pamoja na uundaji wa vitenzi. Kazi hii ni tofauti na kazi yetu kwa sababu tutajikita katika sehemu ya tahariri.

Olamide na Aminu (2014) walifanya uchanganuzi wa vitendo usemi katika tahariri ya jarida la *Tell*, Nigeria. Walichunguza sehemu ya utangulizi wa tahariri wakitumia nadharia ya vitendo usemi. Matokeo ya utafiti huo yalionyesha kwamba sehemu ya utangulizi inasheheni vitendo usemi vinayoathiri mtazamo wa wasomaji. Kazi yao ni muhimu katika utafiti huu kwa sababu inachangia katika kuchunguza jinsi mhariri anavyotumia lugha, na hasa vitenzi katika sehemu ya utangulizi.

Otuoma (2015) alifanya uchanganuzi wa mtindo na maudhui wa vibonzo katika gazeti la *Taifa Leo.* Utafiti huu ulibaini kwamba, maudhui ya ufisadi na siasa zinatawala katika vibonzo husika, pia matumizi ya tamathali za lugha inatawala katika lugha ya vibonzo. Utafiti huu ni wa manufaa kwetu kwa sababu tunaangazia mtindo katika gazeti la *Taifa Leo*. Tofauti ni kwamba utafiti wetu ni wa tahariri na wa Otuoma ni wa vibonzo .

### 1.8.1 Yaliyoandikwa kuhusu nadharia

Kitsao (1975) alihakiki mtindo katika kazi za kinathari za Kiswahili akitumia nadharia ya umitindo. Kitsao amefafanua kwa undani dhana ya mtindo na elimumitindo. Kisha, akachunguza jinsi mtindo unavyojitokeza katika kazi teule alizozishughulikia: mashairi, tamthilia, hadithi fupi na riwaya. Matokeo ya utafiti wa Kitsao ni muhimu kwa utafiti huu wetu kwa kuwa yanatupatia mwelekeo wa kuchanganua vipengele vya mtindo katika tahariri.

Lugwiri (2011) alifanya uhakiki wa kimtindo katika *Utenzi wa Tambuka*, alishughulikia sitiari, taashira na tashbiha katika uwasilishaji wa dhamira. Katika utafiti huu, Lugwiri anatumia nadharia ya Umitindo na anabainisha wazi jinsi vipengele vya tamathali za usemi vinavyobainika katika utenzi-husika. Anaonyesha kuwa tamathali za usemi ni mihimili mikuu ya maudhui na dhamira. Utafiti huu unahusu mtindo katika tahariri ya *Taifa Leo*, matokeo ya utafiti wa Lugwiri yana manufaa katika kuchanganua vipengele vya kimtindo tutakavyovishughulikia.

Soi (2014) alitafiti methali za Kipsigis akitumia nadharia ya umitindo na ya uhusiano. Katika utafiti wake Soi alichanganua mtindo katika methali, mbinu alizozipata ni sitiari, tashihisi, kweli kinzani na mengine. Anasema kwamba mbinu hizi zitumiwapo hukuza uwasilishaji wa ujumbe wa methali. Kazi hii ni ya muhimu kwetu kwa kuwa tunatumia nadharia ya umitindo ili kuchunguza matumizi ya lugha na tamathali za usemi.

## 1.9 Njia za utafiti

### 1.9.1 Ukusanyaji data

Gazeti la *Taifa Leo* lilinunuliwa kila siku. Tahariri za gazeti ya *Taifa Leo* za mwezi wa Januari hadi Machi mwaka wa 2016 zilishughulikiwa ili kuchangia data ya kazi hii. Tahariri za miezi iliyotajwa zilichanganuliwa. Tahariri zilizoshughulikia mada mbalimbali: siasa, maswala ya kijamii, uongozi, uhusiano wa kimataifa na mengineyo zilichunguzwa. Jumla ya tahariri 91 zilikusanywa kwa kipindi cha miezi mitatu. Mtafiti

alipitia tahariri zote 91 na kuteua tahariri 30 zilizosheheni mbinu anuai za lugha na mitindo kwa kutumia uteuzi pendelea.

Utafiti wa maktabani ulifanywa. Mtafiti alisoma vitabu vya wataalam na waandishi mbalimbali walioandika kuhusu nadharia ya umitindo na mtindo. Makala na tasnifu mbalimbali zipatikanazo kwenye mtandao zilisomwa ili kutupa mwanga kuhusu tahariri. Mtafiti alisoma tahariri nzima, akatambue mtindo wa uwasilishaji ujumbe katika tahariri husika na matumizi ya lugha.

### 1.9.2 Uchanganuzi wa data

Baada ya kupitia tahariri zote 30, mtafiti alichanganua data na kuainisha kwa kategoria mbili. Kategoria ya kwanza inaonyesha mitindo ya lugha ya tahariri husika. Maelezo ya kitathmini yametolewa katika sehemu hii. Kategoria ya pili inaonyesha mbinu za lugha katika tahariri. Data imechanganuliwa kwa kutoa maelezo ya kitathmini.

# SURA YA PILI: DHANA YA TAHARIRI

## 2.1 Utangulizi

Katika sura hii, tunashughulikia dhana ya tahariri, tumeeleza maana ya tahariri, historia ya gazeti kwa ujumla, kisha tukatoa historia ya gazeti la *Taifa Leo* na historia ya tahariri. Maelezo yanatolewa kuhusu aina za tahariri, majukumu ya tahariri, sifa za tahariri na uhusiano kati ya tahariri na habari.

## 2.2 Tahariri

Tahariri ni makala ambayo hutoa maoni ya gazeti au jarida kuhusu jambo fulani. Van Dijk (1996) anasema tahariri ni aina ya diskosi ya kutoa maoni yanayolenga umma mkubwa, malengo yakiwa ni kushawishi. Inamulika mawazo ya walio wengi katika bodi ya tahariri, walio katika uongozi wa gazeti, ambao unaundwa na wahariri na mameneja wa biashara. Mara nyingi huwa haijatiwa saini. Kama vile mawakili hufanya, wahariri hujenga mabishano (argument) na kujaribu kuwashawishi wasomaji ili wafikirie kwa njia iliyo sawa na vile wahariri wanavyofikiria. Tahariri zinanuiwa kuathiri maoni ya umma kukuza uhakiki (critical thinking) na wakati mwingine kusababisha watu kuchukua hatua kuhusu jambo fulani.

### 2.3 Historia ya gazeti

Uchapishaji ulivumbuliwa kabla ya 1450. Historia ya gazeti ilianza katika karne ya 17 (Kroupova, 2012). Katika kipindi cha historia ya gazeti, kuna mambo mengi mapya yaliibuka, mengine yalikataliwa na mengine yakakubaliwa na jamii. Ili kufikia kiwango cha kukubaliwa, gazeti limepitia mengi magumu. Kati ya changamoto ambazo gazeti lilipitia ni: ukosefu wa elimu, uchukuzi mbovu, kukosekana kwa teknolojia, uadui kati ya makampuni ya magazeti na sheria zinazodhibiti uhuru wake, (Kroupova, 2012 katika Franklin, 2008).

#### 2.3.1 Historia ya *Taifa Leo*

Gazeti la *Taifa Leo* ni gazeti la Kampuni ya Nation Media Group (NMG) ambayo ina afisi zake Barabara ya Kimathi jijini Nairobi. Kulingana na Loughran (2010) gazeti la *Taifa Leo* lilichapishwa mara ya kwanza 1958, na Mwingereza Charles Hayes na mwenzake Tebbutt, wakati huo likiitwa *Taifa*. *Taifa* lilikuwa gazeti la kila wiki.

Loughran (2010) anaeleza changamoto zilizowapata wachapishaji wa gazeti hili lilipozinduliwa. Kwanza, Hayes anasema kwamba hawakupata pesa za kuwalipa wafanyakazi mshahara kwa miezi mitatu ya kwanza baada ya kuzinduliwa kwake. Pili, kwa sababu ya ukosefu wa magari ya kusafirisha na kusambaza gazeti hilo, walituma nakala za gazeti la *Taifa* kupitia mabasi bila kujua iwapo zingefika zinakotumwa. Shida nyingine ilikuwa kwamba watu wengi hawakujua kusoma na kuandika. Hayes anasema kuwa, ilikuwa vigumu sana kupata matangazo ya kuweka kwenye gazeti hilo. Hata hivyo, idadi ya nakala zilizochapishwa mara ya kwanza ilikuwa 10,000. Gazeti la *Taifa* lilikuwa ya kurasa 8, ukurasa wa kwanza ulichapishwa kwa senti 25 tu, lakini kama anavyoeleza Hayes, kulikuwa na shida ya uchechefu wa pesa wakati huo.

Mbali na changamoto hizo, gazeti la *Taifa* lilikuwa jipya na lenye matumaini makuu katika soko la wakati huo, sera yake ilikuwa ni kuunga mkono mapambano ya Kenya kujipatia uhuru. Kichwa cha habari cha gazeti la kwanza kilikuwa *'When shall we see freedom',* habari hii iliwavutia wengi wa Wakenya waliokuwa na hamu ya uhuru. Jina lililopewa gazeti hilo; *Taifa*, kwa Kiingereza *'Nation'* lilifaa sana kwa gazeti hili kwa wakati ambapo Waafrika walikuwa makini katika kujipatia jamii huru ( Loughran, 2010).

Mwaka wa 1959, gazeti hili likanunuliwa na Aga Khan na likawa gazeti la kila siku na kuitwa *Taifa Leo* kufikia mwaka wa 1960. Gazeti la Kiingereza, *Sunday Nation* lilizinduliwa Machi 1960, na *Daily Nation* likazinduliwa Oktoba 1960. Loughran (2010) anaeleza kuwa mhariri mkuu wa kwanza wa asili ya Kiafrika alikuwa Hilary Boniface Ng'weno, aliyeteuliwa 1964.

### 2.3.2 Historia ya tahariri

Ate (2008) akimnukuu Yaasa (1996), anaeleza historia ya tahariri kuwa asili yake ni miaka ya 1830, na kwa wakati huo, tahariri ilirejelea makala yaliyoandikwa na mhariri. Katika karne ya 20, tahariri ilianza kupanuka. Kukawa na tofauti kati ya ukurasa wa tahariri na barua kwa mhariri. Katika kipindi hicho magazeti mengine yalianza kuweka tahariri katika ukurasa wa sehemu ya kushoto (Ate, 2008).

Zamani, magazeti yaliegemea upande mmoja, huku yakieleza maoni ya wanaomiliki gazeti hilo (*The Washington Post, 2003*). Mchapishaji wa *New York Tribune* alifanya gazeti lake liwe sauti iliyowakilisha taifa ili kupigana na utumwa. Kulingana na *News*

*History Gazette*, katika *The Washington Post (2003)* inaeleza kuwa katika mwaka wa 1862 tahariri iliandikwa na Greeley '*Prayer of Twenty Millions'* ili kumsihi Rais Lincoln kuwaachilia huru watumwa. Lincoln alimjibu mwenyewe kwamba, hata ingawa lengo lake (Lincoln) halikuwa kuokoa au kuwaangamiza watumwa, lengo lilikuwa kuokoa Muungano (union).

Katika miaka ya 1920, Uanahabari wa kitaaluma (professional Journalism) ukarudi nyuma kwa kuandika magazeti madogo yenye picha na vichekesho (tabloids). Huu ni wakati ambapo majarida kama *Time* yalianzishwa na 'Canons of Journalism' likakubalika (*The Washington Post*, 2003).

*The Washington Post* (2003), inaendelea kueleza kuwa kanuni za American Society of Newspaper Editors (ASNE) za mwaka wa 1922, zilitilia mkazo utendakazi wa kitaaluma na maadili. Kanuni za ASNE za hivi karibuni zinaonyesha kwamba tahariri, barua kwa mhariri na makala, ziandikwe kwa ufasaha na kwa kiwango kilicho sawa na taarifa za habari. Magazeti ya kisasa yamepanua na kuipa hadhi (dignity) na kutajirisha ukurasa wa tahariri ili idhihirishe maoni ya wahariri na hata waandishi wageni.

### 2.4 Aina za tahariri

Tahariri zinaweza kuwekwa kwenye vikundi kulingana na malengo ya mwandishi wa tahariri husika. Ate (2008) anaeleza aina tatu za tahariri zifuatazo:

Aina ya kwanza ni tahariri za kufasiri. Tahariri hizi zinaandikwa hasa zikiwa na lengo kuu la kueleza mambo yaliyo katika hali ya hatari (at stake) kwa kuyaweka wazi ili msomaji ayaangazie. Tahariri za kiufasiri zinaweza kuwa chanya na hasi au isiyopendelea upande wowote kutegemea jinsi mhariri anavyoshughulikia mada yake.

Pili ni tahariri za kipinga (controversial), aina hizi za tahariri zinawasilishwa zikiwa na lengo mahususi la kuonyesha msimamo maalum. Zinalenga kumdhibitishia msomaji kuhusu jambo ambalo anapaswa kufanya huku mhariri akionyesha kinyume chake kwa kuangazia ubaya wake. Tahariri hizi hazina nafasi ya kutokuwa na upendeleo; zinaweza tu kupinga, au kuunga mkono.

Nazo tahariri za kiufafanuzi zinatoa swala linaloudhi (vexing issue) ili msomaji atoe uamuzi wake. Tahariri hizi zinafungua mawazo, zinachokoza (provoking) maswala

ya siasa, kijamii na za kiuchumi ili msomaji apate kuyachukulia msimamo. Tahariri hizi zinatambua tatizo, kufafanua na kuruhusu msomaji kutafuta suluhisho.

Kulingana na Ate (2008), katika enzi ya kutatua matatizo, wenye ujuzi wanaona kuwa tahariri za kiufafanuzi hazifai kwa sababu zinanakili matatizo kama yalivyo na kuachia msomaji tatizo la kuamua. Tahariri hizi zinaendelea kufifia katika taaluma ya uanahabari kwa sababu yana upungufu wa kimuundo, hayatoi suluhisho kwa matatizo yaliyojitokeza/ yaliyotambuliwa.

Kwingineko, *Characteristics of Editorial Writing,* (haina tarehe) inaeleza aina nne za tahariri. Aina ya kwanza ni tahariri za kufafanua na kufasiri. Katika aina hii ya tahariri, wahariri huzitumia kueleza jinsi gazeti lilivyowasilisha mada iliyo na utata (sensitive and controversial), kwa mfano gazeti la shule linaweza kuelezea sheria mpya. Mwandishi atakuwa akifafanua na kutoa ufasiri wa sheria hizo mpya ili zieleweke vyema. Pili, kuna tahariri za kuhakiki. Tahariri hizi zinahakiki kwa njia ya kutoa maoni, maamuzi na hali ya mambo huku zikitoa suluhisho kwa matatizo yaliyotajwa. Lengo la kimsingi (immediate) ni kuwajulisha wasomaji kuhusu tatizo bali sio kutoa suluhisho.

Tahariri za kushawishi zinalenga kuhusu suluhisho bali si kutambua tatizo. Kutoka kwa aya ya kwanza,wasomaji wanahimizwa kuchukua hatua maalum iliyo chanya, mfano mzuri wa tahariri za kushawishi ni tahariri ambazo zinaidhinisha misimamo ya kisiasa.

Mwisho kunazo tahariri za kusifu, tahariri hizi huwasifu watu na mashirika kwa kufanya jambo vizuri. Ate (2008) anasema kwamba ni nadra kupata tahariri kama hizi, kinyume na zile tatu za mwanzo.

## 2.5 Majukumu ya tahariri

Dhima ya tahariri ni kueleza maoni ya gazeti na ya wahariri wa gazeti hilo. Van Dijk (1992) anaeleza kuwa, ni jukumu la tahariri kuibua maoni ya wahariri wa gazeti na maoni hayo yanayoungwa mkono na mfululizo wa mijadala ambayo yanakusudiwa kuchangia katika kazi ya tahariri, ambayo ni kushawishi. Van Dijk (1992) anaendelea kueleza kuwa, wahariri wanajaribu kuzalisha mtazamo na itikadi zao wenyewe kwa umma, wakiwa na lengo la kuhalalisha utawala na nguvu ya kikundi maalum. Kulingana

na maoni haya ina maana kwamba tahariri ni njia ya kueneza itikadi miongoni mwa umma kama njia ya kuonyesha udhibiti na nguvu ya kundi hilo. Hata hivyo tahariri inaweza pia kufanya kinyume cha hayo. Badala ya kusema maoni ya gazeti, mhariri anaweza kusema kwa niaba ya mwananchi wa kawaida. Van Dijk (1995) anasisitiza kuwa, jukumu la tahariri ni kuunda maoni ya umma; kwa wale watu wanaosoma tahariri zinasaidia kupata uamuzi kuhusu mambo katika ulimwengu.

Van Dijk (1996) katika Belmonte (2008) ametoa ufafanuzi wa kina kuhusu jukumu la tahariri; tahariri ni makala ya kutoa maoni na ina jukumu la wazi katika kuumba na kubadilisha maoni ya umma. Kuendeleza utangamano wa kijamii na wanahabari, wasomi na wengine wanaohusika na maswala ya lugha, na kuathiri mjadala wa kijamii, maamuzi na mambo mengine ya kijamii na ya kisiasa. Hii ina maana kuwa tahariri inampa ujuzi msomaji ili kuunda au kubadilisha maoni na kuhimiza mtagusano kati ya msomaji na mwandishi.

Greenberg (2000) anaeleza kuwa, tahariri huchukua jukumu muhimu la kimawasiliano kwa kuwapa wasomaji wa gazeti sauti ya kipekee na yenye mamlaka ambayo husema nao kwa njia ya moja kwa moja.

Albright (2006) anachangia kwa kusema kuwa tahariri inaweza kubadilisha ulimwengu hasa wakati ambapo teknolojia mpya imeenea. Hii ni kwa sababu kuna ushirikiano na uhusiano kati ya msomaji na tahariri; mhariri anaandika tahariri, msomaji anaandika barua kwa mhariri ili kutoa maoni yake.

Hallock (2008:23) anasema kuwa tahariri zinaandika kile serikali zinahitaji kutoka kwa gazeti na uandishi wa gazeti. Hili linawezekana wakati ambapo serikali inatoa ufafanuzi kuhusu mambo yanayostahili kufikia wananchi.

Ate (2008) anafafanua majukumu ya tahariri mojawapo likiwa ni kuhakiki hali ya siasa katika jamii, uchumi, maadili na mitanziko (dilemmas) ya kijamii. Mhariri wakati mwingine hufanya kazi ya watetezi au wanaharakati wa kutetea haki za kibinadamu, wakipaaza sauti kuhusiana na dhuluma na ukiukaji wa maadili na mambo yaliyokubaliwa katika jamii. Tahariri huvamia sera za serikali ambazo hudhulumu raia. Kwa upande mwingine wa serikali, iwapo upande mmoja wa kijamii ukiamua kwa mfano kuchukua sheria mkononi mwao, tahariri zinapaswa kuhakiki.

Tahariri humulika maarifa ya wakati husika kwa kuangazia masuala yaliyo tata katika jamii, tahariri hujaribu kuangazia pande mbili kwa kila jambo. Zinatoa na kuchanganua mihimili na upungufu wa mambo yanayohusu umma huku ikipendekeza masuluhisho ya mambo tata (Ate, 2008).

Ate (2008) anaeleza kuwa tahariri huleta mambo yanayoweza kufanyiwa mjadala na kutoa mwongozo wa kitaaluma ili jamii iweze kujadili na kufikia uamuzi wa mambo yanayowasumbua wanajamii (burning issues).

Jukumu lingine la tahariri kwa maoni ya Ate (2008), ni kuwakinga waliodhulumiwa (defend the underdogs) katika jamii. Katika jamii yoyote ile, kuna tofauti za kiuchumi kati ya matajiri (walio na nguvu) na maskini (wasio nayo). Waliosoma na wasiosoma. Walio matajiri wanapowadhulumu maskini kwa njia isiyofaa tahariri huinuka na kuwakinga. Mahusiano kati ya makundi ya kijamii huchunguzwa na wanahabari na lile jukumu la utetezi hufanywa na tahariri ili kutetea wale wanaodhulumiwa.

Tahariri pia huidhinisha na kuunga mkono jambo linalohusu umma. Wahariri wanaweza kuunga mkono masuala yanayoonyesha ukarimu na yanayohusu umma. Wahariri si wataalamu ambao kazi yao ni 'kubweka na kuuma' ambao kila mara kazi yao ni kuvamia tu (Ate, 2008). Kwa mfano, iwapo wanaounda sera na wanaoitekeleza sera hiyo (executors) wanafanya kazi yao vizuri, tahariri hutambua juhudi zao. Mbali na kuunga mkono, waandishi wa tahariri wakati mwingine huweza kutambua sehemu inayohitaji kupigwa msasa katika sera hiyo kabla ya kuidhinisha. Jukumu lingine la tahariri ni kwamba linaathiri uundaji sera na maamuzi yanayofanywa kuhusu maswala fulani. Tahariri huchochea waundaji sera ili kuunda ajenda ambazo zitasaidia kutekeleza uongozi unaokubalika.

Tahariri huhimiza na kumshawishi msomaji kukubali kuwa jambo fulani ni sahihi au si sahihi. Baadhi ya tahariri hujaribu kuwavuta (woo) watu katika jamii, mashirika au hata serikali ili ikubali mwelekeo fulani kwa manufaa ya jamii nzima. Tahariri kama hizo huwa zimesheheni mambo yasiyopingika (facts) ambayo yanapambwa na lugha ya kushawishi, inayoacha alama isiyofutika kwa msomaji (Ate, 2008)

Tahariri hupasha habari, huburudisha wanajamii kwa masuala anuai kuhusu jamii hiyo. Jumbe zinazopatikana katika tahariri zinaweza kusaidia kutunza taasisi adilifu (sacred) za kitaifa kama vile ndoa na dini. Mbali na hayo, kupitia vyombo vya uhariri, wanajamii

wanaweza kuhimizwa wahusike katika miradi muhimu ya kimaendeleo. Miradi hii inaweza kuwa pamoja na zoezi la chanjo, kuhesabu watu na mengine (Ate, 2008).

Mwisho, Ate (2008) anaongeza kuwa tahariri inaweza kuwapa mwanga waundaji sheria kwa kuunda miswada ambayo baadaye huweza kuwa sheria za nchi. Tahariri inayoacha alama kwa hadhira yake lazima ionyeshe hekima na uadilifu na iwe sauti ya jamii.

## 2.6 Sifa za tahariri

Lengo la tahariri ni kumshawishi na kujishindia msomaji wake ili akubaliane na maoni yake. Heybels & Weaver (2011) wanaeleza kuwa, kushawishi ni mchakato ambapo mwasilishi anaathiri imani na mwelekeo au tabia ya mtu mwingine. Wanasema kuwa, kushawishi ni juhudi iliyopangwa na yenye kukusudiwa na mwasilishaji ili mwelekeo wake ukubaliwe na hadhira lengwa. Ili tahariri ziwe za kuvutia na kunata, mbinu za tamathali lazima zitumuke katika utangulizi, mwili na hitimisho.

Ate (2008) anapendekeza mikakati ifuatayo kuhusu uandishi wa tahariri:

Kwanza, uandishi wa tahariri uwe sahili lakini unaoonyesha kuwa ni kazi ya shirika na ukomavu katika matumizi ya lugha udhihirike. Isiwe ya kushurutisha msomaji kwa sarufi inayotatanisha. Lengo kuu ni kuwasiliana ili msomaji aelewe kwa urahisi.

Lugha ndio msingi wa mawasiliano, hata kama wasomaji wa tahariri ni watu walioelimika, mwandishi wa tahariri ahakikishe ametumia lugha vizuri ili kuwahusisha hata wale walio katika kiwango cha chini katika elimu. Lugha inayotumiwa iepuke utata wa kuwasilisha ujumbe moja kwa moja.

Tahariri iwe na mnato wa moja kwa moja (first impression), aya ya kwanza ya utangulizi isiwe inayochosha. Aya ya kwanza, pili na tatu ziwe za kuvutua ili zimpeleke msomaji afikie kwenye mwili na hatimaye hitimisho la tahariri hiyo.

Ate (2008) anaendelea kueleza kwamba, mwandishi aweze kudumisha mvuto wa awali uliopatikana katika aya ya kwanza. Mwandishi atumie ukweli uliodhibitishwa na uliotolewa mahali panapoaminika. Tahariri huweza kudumisha maslahi na

matamanio ya msomaji iwapo kuna idhibati kuwa yanayowasilishwa yanatoka kwenye asili inayoaminika.

Mwandishi wa tahariri atumie takriri. Vipengele au hoja muhimu katika tahariri lazima irudiwe tena na tena ili kuhakikisha kuwa msomaji ameyapata vizuri. Mbinu hii inapaswa kutumiwa kwa busara na umakinifu mkubwa.

Matumizi ya tamathali za usemi, hulainisha toni, mtindo na mtazamo wa tahariri. Mbinu za tamathali kama jazanda, tashbihi zitumiwe kwa makini katika tahariri ili ile athari inayotarajiwa iweze kufikiwa. Matumizi ya tamathali hizi huacha alama ya kudumu katika akili za msomaji hivi kwamba atakuwa na jambo la kukumbuka.

Kauli ya kufungia ni muhimu katika tahariri. Ili msomaji wa kawaida ashawishike, maandishi yanapaswa kuwa yamemchochea vya kutosha. Mwandishi atumie maneno yenye nguvu na yanayoweza kukumbukwa anapomalizia tahariri. Kauli ya mwisho iweze kufunga msomaji.

Lazima tahariri iwe na 'ladha' yashirika husika . Taasisi hiyo ya uanahabari (the media establishment) lazima isikike ikisema katika tahariri wala isionekane kwamba ni kazi ya mtu binafsi.

Lugha ya tahariri inapaswa iwe sahili na isiyotatanisha; lugha iwe inaeleweka na hadhira lengwa hata kama lengo la tahariri ni kuathiri hadhira, kuelimisha au kuburudisha . La sivyo, lengo la tahariri halitafikiwa .

Mhariri anapaswa kulenga ndipo katika uandishi wake. Aseme anayopaswa kusema bila kumzungusha msomaji kwa maneno mengi. Sifa nyingine muhimu iliyodokezwa na Ate (2008) ni kuwa tahariri iwe na mambo yanayomhusu binadamu. Hii ni kwa sababu, watu huwa na haja ya maswala yanayohusu binadamu wenzao.

Tahariri iwe ya kuvutia.Tahariri ambazo ni hafifu na zisizochangamsha haziwezi kuathiri hadhira lengwa ipasavyo. Mbinu za kushawishi na mbinu zingine zinaweza kutumiwa kwa lengo hilo. Mwisho, tahariri yoyote ile lazima iwe ya kiasili kwa yaliyomo na hata kwa toni yake. Yawe mawazo yanayotokana na utafiti wa mwandishi mwenyewe. Jumba la gazeti halipaswi kuiba au kunakili tahariri ya gazeti lingine.

## 2.7 Uhusiano kati ya tahariri na habari

Habari huhusiana vipi na tahariri? Tahariri na habari ni vitanzu vya utanzu mmoja wa uandishi wa magazeti. Hivyo basi habari na tahariri zitalingana na wakati mwingine kutofautiana kwa njia mbalimbali. Kwanza, habari hutolewa kwa njia ya kiutobinafsi (objectively) na tahariri hutolewa kwa kupendelea (subjective). Tahariri inaweza kuibua maoni ya umma yanayopinga au yanayounga mkono maswala muhimu. Habari huhusu matukio ya wakati huo ili kusaidia hadhira kujielewa na kuelewa mazingira yake. Habari huathiriwa na matukio, ripoti hadhira na mambo mengine. Ate (2008) anaeleza uhusiano uliopo kati ya habari na tahariri kama ifuatavyo;

Uhusiano wa kwanza ni sifa ya wakati. Ate (2008) anaeleza kuwa habari zinazovutia ni zile zinazohusu matukio ya hivi punde, tukio la wiki moja iliyopita halivutii hadhira kama tukio lililotendeka jana usiku. Hata hivyo, mhariri hatalazimika kuandika tahariri kuhusu matukio ya wakati huo, lakini wakati mwingi, chemchemi ya tahariri ni vichwa vya habari za hivi punde.

Pili, Ate (2008) anaeleza sifa ya umbali kimahali. Umbali au kukaribia kwa tukio huamua ikiwa habari itavutia walengwa ua la. Tukio la ajali linalotendeka kwa mfano, Afrika Kusini, halivutii kama ambavyo lingevutia ikiwa ajali hiyo ingetendeka mjini Nakuru. Kukaribiana au umbali unaweza kuangaliwa kisaikolojia pia, mwathiriwa wa virusi vya UKIMWI katika nchi ya Kenya atavutiwa na habari za kupatikana au kugunduliwa kwa tiba ya virusi hivyo nchini Marekani, haijalishi umbali kimasafa.

Uhusiano mwingine ni ule unaohusu umaarufu. Ate (2008) anafafanua kwamba aghalabu, watu maarufu na shughuli maarufu huwa habari za kuvutia. Viongozi kama rais, maaskofu, maseneta na wengine huwa vivutio vya habari kwa yale wanayosema na kutenda. Tahariri kwa upande wake, huwa sauti ya wasio na nguvu. Mhariri atafanya kazi ya kutetea wasio na sauti katika jamii inayotawaliwa na wenye nguvu.

Habari huundwa na matukio yasiyo ya kawaida kama vita, maandamano majanga ya kimaumbile. Mara nyingi habari za matukio mabaya, yasiyopendeza na ya kushangaza huvutia waandishi wa habari. Tahariri zinazohusu matukio yaliyotajwa hapo juu huandikwa hivi kwamba tahadhari inatolewa ili kuepuka majanga kama hayo wakati mwingine.

Sifa nyingine kulingana na Ate (2008) inahusu madhara au matokeo ya matendo na maamuzi yanayopitishwa. Hadhira huwa na hamu ya kusikia mambo ambayo yanaathiri moja kwa moja maisha yao, yawe ya sasa au ya wakati ujao. Mambo kama kuongezeka kwa bei ya mafuta, nyongeza za mishahara huwa vivutio vikuu kwa wasomaji na watazamaji wa habari.

Mbali na hayo, habari za kuvutia na zile zinazohusu watu. Habari ni zile ambazo hufanya mtu wa kawaida kusikitika (empathise ) na waathiriwa. Matukio kama wizi wa kimabavu, ajali na vifo, huwa yananasa na kuvutia kwa sababu huweza kutendeka kwa mtu yeyote. Mhariri anaweza kuteua mada ya tahariri kutoka kwa habari hizo zinazohusu watu.

Mwisho, Ate (2008) anasema kuwa habari za moja kwa moja (factual) ni zile zinasema jinsi mambo yalivyo. Habari zinazoripotiwa huwa msingi kwa waandishi wa tahariri na makala katika gazeti (features). Kabla tahariri kuandikwa kuhusiana na jambo lolote lazima kwanza iwe imeripotiwa kwa njia ya kutangazwa au iwe ni habari zilizochapishwa. Kwa hivyo, ni kazi ya mhariri kufasiri habari, kuchanganua na kutambua maoni ya umma kuhusu mambo yaliyo muhimu katika habari zilizoripotiwa.

## 2.8 Mada za tahariri

Jumbe zinaweza kupatikana kutoka kwa mada za habari au matukio kutoka vichwa vya habari. Matukio hayo lazima yawe ya kusisimua matarajio ya umma (Ate, 2008).

Ate (2008) anaongezea kuwa waandishi wa tahariri wanaweza kupitia katika mtandao na kupata jumbe zinazofaa za kuandika au kutajirisha tahariri. Pahali pengine ni rekodi na machapisho ya umma (public and printed records). Mwandishi wa tahariri anaweza kupata habari au ujumbe kutoka machapisho mbalimbali kuhusu ushuru, ndoa, gazeti rasmi la serikali (Goverment gazette), katiba, mijadala bungeni. Shughuli za kijamii zinaweza kumpa mwandishi mada. Mwandishi mzuri lazima awe anatangamana na jamii vizuri, watu wa matabaka mbalimbali ili ajue kile kinachoendelea. Mwandishi wa tahariri anaweza kupata habari zaidi za kuongezea

mada yake kutoka kwa maafisa wa usalama, kama vile polisi, iwapo jambo linazungumziwa linahitaji ujuzi wao.

Wahariri watalazimika kutafuta watu wenye ujuzi wakati wanapozungumzia mambo ya kitaaluma na mambo ya hali ya juu kiteknolojia. Kwa mfano, jambo la kisheria linahitaji ujuzi wa wakili kabla ya kuliandika. Ni muhimu ili kumwepusha mhariri kufanya kosa kubwa. Madaktari, waandishi, wadau wa elimu na wajuzi wengine wanapaswa kushirikishwa iwapo jambo linalozungumziwa linahusu maeneo yao ya ujuzi (Ate, 2008).

Vitabu vya kila aina vipatikanavyo maktabani vinaweza kuwa na habari za kuandikia tahariri. Vitabu kama thesauri, makamusi, ensaiklopidia, almanak na vingine vinaweza kupatikana maktabani.

## 2.9 Muundo wa tahariri

Tahariri kama uandishi wa aina yoyote huwa na muundo; jinsi aya zimepangwa kihatua na kimtiririko. Muundo wa kawaida wa tahariri huwa na sehemu nne kuu kwa mfano, mada ya tahariri, utangulizi, mwili na hitimisho.

### 2.9.1 Mada ya tahariri

Mada hutanguliza tahariri. Mada inapaswa kuwa inayonata kwa kutumia maneno machache. Mada huwa kama dirisha la tahariri, kwa hivyo haipaswi kuwa isiyovutia, inayotatanisha wala isiwe ya kupotosha. Etim (1996) anatoa vidokezo vifuatavyo kuhusu mada inayonata ; inaweza kuchukua muundo wa swali.

Wakati mwingine, kauli za kawaida na nukuu zinaweza kuunda kichwa kizuri cha tahariri. Kwa mfano, mistari ya wimbo wa taifa, kutumia mbinu ya takriri ; kurudia silabi au hata herufi fulani. Etim (1996) anaendelea kueleza kuwa, kuchezacheza na maneno kunaweza kuzua mada inayovutia hasa iwapo ni tahariri za kusifu .

### 2.9.2 Utangulizi

Kitangulizi ni aya ya kwanza baada ya kichwa cha tahariri. Sawa na mada ya tahariri, kitangulizi kinapaswa kuwa cha kunata ili kumsukuma msomaji kusoma tahariri nzima. Kitangulizi kizuri lazima kishikilie matamanio yaliyoibuliwa na mada ya

tahariri. Mwandishi wa tahariri anaweza kutumia maswali, ukinzani (contrast) au kutaja hoja moja kwa moja bora awe ameeleza vizuri.

Etim (1996) anataja sifa za kitangulizi kuwa:

i) Kiini cha tahariri
ii) Iendeleze toni iliyodokezwa kwenye mada

### 2.9.3 Mwili

Hii ni sehemu inayobeba ujumbe wa tahariri kwa kina. Sehemu hii itasheheni pande zote mbili za swala linalozungumziwa. Migogoro ya kila aina inaibuliwa na kutatuliwa katika sehemu hii. Mwili wa tahariri huwa ni jukwaa la makabiliano (reaction) kuonyesha msimamo wa gazeti kuhusu jambo fulani. Mwili wa tahariri lazima uwe na mantiki, tangamanifu au wenye kufuatika katika uwasilishaji na uchanganuzi wa data. Kuwe na mapatano/muamana (harmony) wa maneno na masuala yanayojadiliwa. Iwapo ni tahariri za kushawishi, sehemu hii itakuwa ya kiagumenti (Etim,1996). Kiagumenti kwa maana ya; kutokuwa na upendeleo, kulinganisha na kutofautisha, kutumia takwimu panapofaa na kuwajuza wasomaji mambo wasiyoyajua.

### 9.3.4 Hitimisho

Hitimisho ni sehemu ya mwisho ya tahariri. Mara nyingi hitimisho inaweza kuwa inasisitiza yale ambayo mhariri ameyataja katika sehemu ya mwili ya tahariri. Hitimisho inaweza kufanya kazi ya kutilia nguvu zaidi maoni yaliyotajwa hapo mwanzoni mwa tahariri. Mwandishi wa tahariri hujiepusha na maneno mengi yanayorudiwarudiwa .

Kulingana na Okoro na Agbo (2003), hitimisho linaweza kuandikwa kwa njia ya moja kwa moja na kwa muhtasari. Pili, kuandikwa ili kutoa mwito kwa hatua kuchukuliwa, na tatu, hitimisho liandikwe hivi kwamba ni rahisi kunukuliwa. Hitimisho linapaswa kumwacha msomaji akifikiria.

Ifuatayo ni kielelezo cha muundo wa tahariri ya *Taifa Leo* iliyo na sehemu tatu kuu; utangulizi, mwili na hitimisho.

**Madiwani wafikirie upya kuhusu elimu**

***Taifa Leo*, 27/01/2016**

| | |
|---|---|
| Hatua ya madiwani kupinga mswada unaolenga kuinua kiwango chao cha elimu ya wanaotaka wadhifa huo ni ya kuvunja moyo.<br>Mswada huo unatoa pendekezo kuwa madiwani wawe na elimu ya kiwango cha diploma ama digrii kuanzia uchaguzi mkuu wa 2017.<br>………………………………………………………………..<br>Hata hivyo, wameungana pamoja kuupinga kwa visingizio kuwa uwezo wa uongozi haulingani kwa vyovyote vile na kiwango cha elimu alicho nacho mtu. Madiwani pia wamedai kuwa mswada huo ni njama za Bunge la Kitaifa la kuwahujumu.<br>Madiwani hawa huenda wanasema kweli, lakini wanapaswa kufahamu kuwa nyakati zimebadilika. Elimu imekuwa mhimili mkuu wa uendeshaji wa shughuli mbalimbali nchini na kote duniani.<br>Japo ni kweli kuna hali za kipekee ambapo baadhi ya viongozi bora si lazima wawe wamesoma, ukweli ni kuwa elimu huwa muhimu sana katika uimarishaji wa utendakazi wa viongozi wanaochaguliwa.<br>Kwanza, majukumu yao yanahitaji wawe na elimu ya kutosha. Wanapaswa kujadili na kupitisha miswada muhimu inayohusu usimamizi na uendeshaji wa Serikali za Kaunti. Pia wana usemi mkubwa kuhusu jinsi fedha ambazo serikali hizo zinatengewa na Serikali Kuu zinapaswa kutumiwa.<br>Ni muhimu kwa miswada inayowasilishwa kuwa mizuri na yenye manufaa kwa wakazi wa kaunti husika. Hili ni jukumu ambalo linahitaji uelewa mpana wa utaratibu mzima wa utayarishaji wa mswada husika, na jinsi utakuwa na manufaa | Utangulizi<br><br><br><br><br><br>………………<br><br><br><br><br><br><br><br><br><br>Mwili |

| | |
|---|---|
| kwa walengwa wakuu.<br>Kando na hayo, majukumu yao ni mazito na yenye umuhimu mkubwa kuliko madiwani wa zamani. Wengi, hasa vijana, wanawachukulia kama mifano ya kuigwa katika jamii. Madiwani wanalipwa vizuri na maisha yao yameimarika. Ni mfano gani wanaotaka kuonyesha vijana? Kwamba unaweza kufanikiwa bila ya masomo ya maana? | |
| ………………………………………………………………<br>Kwa hivyo, yawapasa kutambua kuwa kuinuliwa kwa kiwango cha elimu, kutakuwa na manufaa kwao binafsi pamoja na uongozi mzima wa Serikali za Kaunti. | ………………<br><br>Hitimisho |

Kwa upande mwingine, Bhatia (1993) anaeleza kuwa muundo wa tahariri huwa na sehemu nne zifuatazo:

Sehemu ya kwanza ni kuwasilisha kesi/hoja. Katika sehemu hii matukio halisi yanayotendeka katika dunia ya kila siku yanawasilishwa. Inaweza kuelezwa kama kupanga mambo (forming issues) kufafanua mambo au kufafanua mambo muhimu.

Baada ya kuwasilisha hoja, inafuata sehemu ya pili ambayo ni kuanzisha mjadala. Mwandishi anaeleza uwezekano kwa kuangazia pande mbili, hali ambayo anaona kuwa haingepaswa kuwa (kupinga) na hali ambayo ingepaswa kuwa.

Sehemu ya tatu ni ya kufikia uamuzi. Katika sehemu hii, mwandishi anaonyesha vile mambo yangepaswa kuwa au yanafaa kuwa. Baada ya mwandishi kuangazia hoja za pande zote mbili, anateua upande mmoja na kuonyesha ubora au ufaafu wake. Hii ni sehemu ambapo mwandishi anatoa hitimisho lake.

Sehemu ya mwisho ni ya mapendekezo. Mwandishi anapendekeza jinsi ya kufaulu kutatua swala lililojadiliwa. Anazua mbinu mbadala zinazoweza kukwamua hali zilizotambuliwa kuwa na utata.

# SURA YA TATU: SUALA LA LUGHA TEULE NA MIUNDO YA SENTENSI

## 3.1 Utangulizi

Sura ya tatu inashughulikia mtindo wa uandishi wa tahariri ya *Taifa Leo.* Tumeeleza udhamiriaji na jinsi unavyodhihirika kupitia kwa uteuzi na matumizi ya vitenzi, virai na vielezi. Tumeeleza jinsi mwandishi anavyotumia maneno yanayodhihirisha toni mbalimbali. Tumechunguza pia miundo ya sentensi zilizotumiwa, sajili za lugha, matumizi ya takwimu na hatimaye tukaeleza jinsi mwandishi anavyoteua mada za tahariri.

## 3.2 Udhamiriaji

Udhamiriaji ni njia ya kipekee ambavyo mwandishi au mzungumzaji anavyoelezea mwonoulimwengu au itikadi yake. Fowler (1986) anasema kuwa lugha haituruhusu kusema jambo bila kuonyesha mwelekeo (attitude) kuhusiana na jambo hilo, hii ina maana kuwa, ni vigumu kupata maandishi ambayo yana sifa za kiutobinafsi (objective), yasiyo na mapendeleo. Katika maandishi yoyote yale, mtazamo wa mwandishi na mkabala anaochukua anapoandika hudhihirika katika kazi yake.

Udhamiriaji unadhihirika kwa kutumia mikakati ya kimatini (textual strategies) kama vitenzi vishirikishi, (auxiliary verbs) vielezi vya udhamiriaji, vivumishi (evaluative adjectives), vitenzi (reporting verbs), na virai (generic phrases). Wahariri wa gazeti la *Taifa Leo* wametumia kitenzi *pasa/paswa* ili kuonyesha msimamo wao kuhusu swala linalojadiliwa.

### 3.2.1 Matumizi ya vitenzi

Mbali na kutujuza habari kuhusu hali ilivyo, mwandishi wa tahariri anaonyesha msimamo wake na hata kutoa mapendekezo kuhusiana na jambo linaloangaziwa. Mifano ya sentensi zifuatazo zimenukuliwa kutoka tahariri za *Taifa Leo:*

*1. Kando na changamoto za idara ya polisi nchini, kuna matatizo mengine kama ya kulinda maslahi ya maafisa ambayo rais* <u>*anapaswa*</u> *kutilia manani.(Taifa Leo 03/03/2016)*

*2. Serikali inapaswa kushirikiana na sekta ya kibinafsi kutoa vyumba vinavyowafaa maafisa wa polisi.(Taifa Leo 03/03/2016)*

*3. Spika Muturi anapaswa kuonyesha uwajibikaji kuhusu suala hili jinsi Uhuru Kenyatta na jaji mkuu Willy Mutunga walivyofanya kwa maafisa katika idara wanazosimamia moja kwa moja. (Taifa Leo 09/02/2016)*

*4. Msimamo wa Bwana Michuki unapaswa kuwa funzo kuu kwa maafisa wakuu wa NTSA, kuwa ni hadi pale watakapokuwa na msimamo mkali ndipo nidhamu itarejea katika sekta ya matatu. (Taifa Leo 26 /01/2016)*

*5. Ijapokuwa hakuna visa vikubwa vya ghasia vilivyoripotiwa kuna mapungufu kadhaa yaliyojitokeza ambayo yanapaswa kukemewa. (Taifa Leo 21/02/2016)*

*6.Tunafahamu kuwa kuandamana ni haki ya kikatiba ya raia wote lakini inapasa kutekelezwa kwa kuzingatia sheria. (Taifa Leo 24/03/2016)*

*7. Ijapokuwa hatuielekezi lawama moja kwa moja, kauli yetu ni kuwa ukali wa kauli yake ulipaswa kudhihirika kuanzia jana. (Taifa Leo 26 /01/2016)*

*8. Sharti serikali itoe mikakati na mwongozo wa uchimbaji madini na mafuta kabla ya matapeli wa ughaibuni hawajaibuka na kugeuza Kenya kuwa kama mataifa ya Kiarabu ambayo yana utajiri mkubwa wa mafuta lakini wenyeji wanataabika kwa sababu ya mizozo. (Taifa Leo 18/03/2016)*

*9.Ushindani mkubwa wa madini na mafuta unaendelea katika masoko ya kitaifa na sharti Kenya ijiweke katika nafasi ya kunufaika na bidhaa hizi badala ya kutegemea mazao ya kilimo pekee. (Taifa Leo 18 /03/2016)*

Katika mifano ya 1 na 2, mwandishi anaarifu kuwa kuna matatizo mengine ambayo rais *anapaswa* kuzingatia. Anapendekeza ushirikiano kati ya serikali na sekta ya kibinafsi ili kutatua shida ya ukosefu wa makao kwa maafisa wa polisi. Haya ni kufuatia agizo la Rais Uhuru Kenyatta kwamba makurutu 10,000 wa polisi wasajiliwe ili kuimarisha hali ya usalama nchini Kenya. Kwa maoni ya mhariri, maafisa wa polisi wakiongezeka, inamaanisha kuwa shida ya makazi ya polisi itaongezeka pia, ndio sababu anatoa

pendekezo kuwa matatizo mengine yashughulikiwe kwanza. Kwa hivyo Rais *anapaswa* kushughulikia tatizo la makazi ya polisi kwanza.

Mwandishi katika mfano wa 3 anatumia neno 'anapaswa' kueleza mwelekeo wake kuhusu madai ya ufisadi bungeni. Kwa maoni ya mhariri, Spika Muturi hajawajibika katika kazi yake, hajachukua hatua yoyote kwa wabunge waliotajwa kwa kuhusika kwa ufisadi. Licha ya ripoti ya EACC iliyowasilishwa kwake Muturi mwaka jana (2015), hakuna hatua aliyochukua dhidi ya wabunge hao. Kwa hivyo mhariri anaelekeza kuwa Spika Muturi awajibike.

Katika mfano wa 4, mwandishi anatumia 'unapaswa' kuelezea msimamo wake kuhusu swala la NTSA. Mwandishi anawaelekeza maafisa wa NTSA waige mfano wa aliyekuwa Waziri wa Uchukuzi marehemu John Michuki, kwa msimamo wake mkali uliolainisha sekta ya uchukuzi. Mwandishi anaona kwamba maafisa wakuu wa NTSA hawakuhakikisha kuwa tangazo lao limezingatiwa na wahudumu wa matatu. Anawashauri wawe na msimamo mkali ili sheria zifuatwe kikamilifu.

Katika mfano wa 5, mwandishi anatumia maneno 'yanapaswa kukemewa' kueleza msimamo wake kuhusu uchaguzi mkuu wa urais nchini Uganda ambapo Rais Yoweri Kaguta Museveni alitangazwa mshindi. Kwenye uchaguzi huo, mwandishi anaonekana kutoridhika na vile upinzani ulivyohangaishwa na serikali ya Museveni. Matumizi ya vitoa machozi kuwatawanya wapinzani na hata bunduki ili kuwatisha wapinzani hao ni baadhi ya mapungufu ambayo mhariri anakemea. Haya ni mambo ambayo anasema kuwa *yanapaswa* kukemewa.

Katika mfano wa 6, mwandishi anawakumbusha wafuasi wa Cord kuzingatia sheria iwapo wataandamana, kwa kutumia kitenzi 'pasa'. Anasema kwamba kuandamana ni haki lakini *inapasa* kutekelezwa kuzingatia sheria. Muungano wa Cord haukufurahishwa na uamuzi wa IEBC wa kukataa kuidhinisha pendekezo la kura ya maamuzi ya Okoa Kenya. Jambo hili limepelekea viongozi wa muungano huo kuchukua hatua nyingine. Mwandishi anabashiri kuwa huenda viongozi hao wanawazia kuanzisha maandamano. Kwa hivyo mwandishi anawakumbusha wanaohusika kuwa maandamano hayo yatekelezwe kwa kuzingatia sheria.

Kitenzi 'paswa' katika mfano wa 7, kimetumika kuonyesha kasoro ya NTSA ambapo ilikosa kutekeleza amri iliyotoa kwa wahudumu wa matatu. Mhariri anaposema

‘ilipaswa kudhihirika kuanzia jana,’ ni kama anampa kinara wa NTSA fursa nyingine kuonyesha ukakamavu wake kwa kuhakikisha kuwa amri anazotoa zinafuatwa kikamilifu.

Mwandishi anaelekeza ushauri wake kwa serikali ya Kenya katika mifano ya 8 na 9 kwa kutumia kitenzi ‘sharti’. Serikali ya Kenya kwa maoni ya mhariri, imekuwa ikitegemea mazao ya kilimo pekee, jambo ambalo pengine si la busara kwa sababu utegemezi huu hautoshi kutimiza mahitaji mengi ya serikali na wananchi kwa ujumla. Hivyo basi, mwandishi anaishurutisha serikali anaposema ‘sharti serikali itoe mikakati na mwongozo’ itakayohakikisha kuwa imenufaika na mafuta yaliyopatikana katika eneo la Kerio Valley.

Vitenzi vingine vya udhamiriaji vimetumika mbali na kitenzi kisaidizi *pasa*. Vitenzi *faa, stahili, hitajika* vimetumiwa na mwandishi ili kuonyesha mwelekeo wake kwa suala husika. Mifano ifuatayo inaelezea hali hii:

*10. Hivyo basi mwaka mmoja uliosalia kabla ya uchaguzi mkuu uandaliwe, <u>unafaa</u> kutumiwa kuonyesha wananchi kuwa hawakukosea kuchagua viongozi wao kwenye uchaguzi mkuu uliopita. (Taifa Leo 12/02/2016)*

*11. Kutokana na matukio hayo, Kenya na nchi nyinginezo barani <u>zinafaa</u> kufahamu kuwa chaguzi za urais ni muhimu sana kwani huwa zinawakilisha sauti na matakwa ya raia. (Taifa Leo* 21/02/2016)

*12.Wahudumu wa teksi jijini Nairobi <u>wanafaa</u> kukubali tuko katika enzi za teknolojia na waanze kukumbatia teknolojia za kisasa kuendeleza biashara zao. (Taifa Leo 05/02/2016)*

*13.Walimu wakuu wa shule za umma ambazo hazifanyi vyema kwenye mitihani ya kitaifa ya mwaka uliopita <u>wanastahili</u> kueleza kwa nini matokeo hayakuridhisha. (Taifa Leo 31/03/2016)*

*14. Badala ya kuanzisha mizozo, wahudumu wa teksi wa kawaida <u>wanahitajika</u> kujifunza kuhusu mbinu ambazo kampuni hiyo inatumia. (Taifa Leo 05/02/2016)*

Mwelekeo wa mwandishi unadhihirika anapotumia kitenzi *faa* katika mfano wa 10, kwa maoni yake, serikali ya Jubilee haijafanya kulingana na matarajio ya wananchi waliowachagua. Mwandishi anazungumzia jinsi viongozi wa kisiasa na maafisa wengine wakuu wa umma wanavyotumia mali ya umma kwa ubadhirifu mkuu. Ametaja safari za viongozi kuzuru nchi za kigeni, hasa madiwani; safari ambazo hazina faida kwa nchi ya Kenya. Mwandishi anashauri serikali iweze kutumia muda mfupi uliobaki kurekebisha makosa yake.

Mwandishi wa tahariri anaeleza katika mfano wa 11 kuwa, uchaguzi nchini Uganda 'unafaa' kuwa funzo kwa nchi jirani kama Kenya. Matukio yaliyofuata uchaguzi wa urais nchini Uganda hayakufurahisha. Mwandishi amearifu jinsi serikali ilivyotumia nguvu kuhangaisha upinzani huku kiongozi wa upinzani Dkt Besigye akikamatwa mara tatu kwa wiki.

Mfano wa 12, mwandishi anawaelekeza wahudumu wa teksi kukubali ushindani kwa kutumia kitenzi 'wanafaa'. Mwandishi anaeleza hali ambapo mzozo ulizuka kati ya wenye teksi na kampuni ya Uber ambayo ina mizizi yake katika mataifa ya magharibi. Kampuni ya Uber inatumia mbinu za kisasa kurahisisha utendakazi wao na hivyo kupunguza gharama. Huduma za kampuni hii ni ya bei nafuu ikilinganishwa na za wahudumu wa teksi wa humu nchini. Mwandishi anawashauri wahudumu wa teksi wa humu nchini kukubali ushindani uliopo na kubadilisha mbinu zao za kutenda kazi.

Mwandishi ametumia vitenzi visaidizi vinavyoonyesha uwezekano wa matukio yanayorejelewa, vitenzi hivi ni pamoja na; huenda, -weza, -takuwa na –elekea.

*15. Ujuzi wake kama mkufunzi wa Harambee Stars wa under-23 na klabu ya Mathare United huenda usitoshe kujenga timu yenye uwezo wa kutetemesha mahasimu kwenye mashindano ya kimataifa.(Taifa Leo 27/02/ 2016)*

*16. Hata ingawa msimamo wa Mwendwa huenda ukawa mzuri kwa kiwango fulani, yamkini nchi hii itakosa kupiga hatua ya maana kutokana na sababu mbalimbali kumhusu kocha huyo.(Taifa Leo 27/02/2016)*

*17. Tume pia inaweza kuwaita viongozi wa upinzani na kuweka bayana mfumo uliotumiwa kukagua sahihi hizo. (Taifa Leo 24/03/2016)*

Mwandishi wa tahariri hii katika mfano wa 15, anashuku uwezo wa kocha Stanley Okumbi ambaye awali alikuwa mkufunzi wa Harambee Stars wa under-23. Stanley aliteuliwa na Nick Mwendwa ambaye ni rais wa shirikisho la soka nchini Kenya. Mhariri anashuku uwezo wake wa kuiendesha timu ya Kitaifa ya Harambee Stars anaposema kuwa ujuzi wake 'huenda' usitoshe kuweza kumenyana na timu zingine katika mashindano ya viwango mbalimbali. Vilevile katika mfano wa 16, mwandishi anaposema 'msimamo wa Mwendwa huenda ukawa mzuri', anaonyesha kutoridhika na msimamo wa Mwendwa wa kuteua kocha Okumbi, hata ingawa msimamo huo unaweza ukawa mzuri.

Kuhusiana na mgogoro uliopo kati ya Cord na IEBC, katika mfano wa 17, mhariri anapendekeza kuwa tume *inaweza* kuwaita viongozi wa Cord ili kuwaelezea waziwazi jinsi ukaguzi wa sahihi ulivyofanywa. Mwandishi anatoa mapendekezo yanayoweza kutumiwa kutatua mgogoro uliopo.

Mbali na kuonyesha uwezekano, mwandishi pia ametumia vitenzi vya kubashiri; *–takuwa na –elekea,* kwenye mifano ifuatayo:

*18.<u>Itakuwa</u> vigumu kushinda vita ufisadi ikiwa wabunge wanaoshiriki uovu huo hawatachukuliwa hatua za kisheria.(Taifa Leo 09/02/2016)*

*19. Kama desturi; Klabu za Kenya <u>zinaelekea</u> kuleta aibu kwenye soka ya shirikisho la [Caf]. Hii ilionekana wiki jana baada ya Gor Mahia na Bandari Fc kutandikwa na timu pinzani kwenye mashindano ya klabu Bingwa Afrika na kombe ya Afrika, mtawalia.(Taifa Leo 20/02/2016)*

Katika mfano wa 18, mhariri anabashiri ugumu wa kushinda vita dhidi ya ufisadi anaposema 'itakuwa' vigumu. Hii ni kwa sababu hatua za kisheria hazichukuliwi kwa wanaoshiriki ufisadi. Anaeleza kuwa baadhi ya wabunge waliitisha pesa za mafuta au kuandikisha kuwa walihudhuria vikao ilhali ni uongo. Wabunge waliotajwa walipomtisha Spika wa Bunge Bw. Muturi, alibadili msimamo wake na kuwatetea wabunge hao. Hii ndio sababu mhariri anabashiri kuwa vita hivi havitakuwa rahisi kushinda.

Mwandishi anabashiri uwezekano wa timu za soka kuleta aibu kwa mara nyingine kwa mashabiki wao, katika mfano wa 19. Mwandishi ametumia kitenzi *zinaelekea* kuonyesha kwamba tayari dalili zimeonekana. Hii ni baada ya Gor Mahia kushindwa

katika mashindano ya klabu Bingwa Afrika na kwa upande mwingine, timu ya Bandari FC kutandikwa na timu pinzani katika mashindano ya Kombe la Afrika.

### 3.2.2 Vitenzi vya kuripoti

Mwandishi anaweza kutumia vitenzi vya kuripoti ambavyo havikutumiwa na msemaji wa kwanza wa kauli inayoripotiwa. Mwandishi akitumia vitenzi kama 'alikiri,' 'alionya', 'anadai', 'anashuku' na mengine, huwa ameingiza mtazamo na mwelekeo wake kuhusu jambo linalojadiliwa.

*23. IPOA ilionya kuwa kuishi kwa mazingira mabovu kunaathiri kisaikolojia utendakazi wa polisi.(Taifa Leo 03/03/2016)*

*24. Bwana Muturi alikiri madai kwamba baadhi ya wabunge waliitisha pesa za mafuta au kuandikisha kuwa walihudhuria vikao ilhali ni uongo. (Taifa Leo 09/02/2016)*

*25. IPOA hata hivyo imekiri kuwa haina mamlaka ya kufanya uchunguzi dhidi ya NPSC. (Taifa Leo 10/02/2016)*

*26. Mwenyekiti (NPSC) anasisitiza kuwa tume inaendesha majukumu yake kwa uadilifu. (Taifa Leo 10/02/2016)*

*27. IEBC imekariri kuwa inazingatia ukubwa wa maeneo wala si idadi ya watu.(Taifa Leo 15/02/2016)*

Katika mfano wa 23, IPOA inatoa tahadhari kuhusu hali inayowaathiri maafisa wa polisi. Mwandishi ametumia kitenzi 'onya' ili kuvutia makini ya msomaji na hasa ili serikali ipate kuchukua hatua haraka iwezekanavyo. Mazingira mabovu yanaathiri utendakazi wa polisi wakati ambapo huduma zao kwa taifa zinahitajika zaidi.

Katika mfano wa 24, kitenzi 'kiri' kimetumiwa na mwandishi kwa lengo maalum. Mwandishi anataka kuonyesha kuwa pengine Spika Muturi angekuwa na chaguo la kuficha habari hizo zinazohusu wabunge wafisadi, lakini aliamua (baada ya kushinikizwa au kwa hiari yake) kufichua habari hizo. Na katika mfano wa 25, mwandishi wa tahariri anaeleza kuwa IPOA *imekiri* kuwa haina mamlaka ya kuchunguza utendakazi wa NPSC. Mwandishi ametumia kitenzi hicho 'kiri' kuonyesha

kuwa jambo hilo halikuwa wazi kwa watu wengi, labda wengi walikuwa wakitarajia kuwa IPOA ingeweza kuchunguza NPSC.

Katika mfano wa 26, maafisa wa NPSC wanadaiwa kupokea hongo kutoka kwa maafisa wa polisi ambao maadili yao ni ya kutiliwa shaka. Kulingana na madai haya, maafisa wa NPSC wanaochunguza polisi wamekuwa wakipokea hongo kati ya Sh.300,000 na Sh 500,000. Hata hivyo, licha ya madai haya, NPSC inasisitiza kuwa inafanya kazi yake kwa uadilifu.

Mwandishi anatumia kitenzi 'kariri' katika mfano wa 27 kumaanisha kuwa msemaji alishasema maneno haya hapo awali; anayarudia kwa mara nyingine. IEBC inakariri kauli hiyo kufuatia tetezi za upinzani kuwa maeneo yaliyo na wafuasi wa muungano wa Cord au vyama vingine vya upinzani, yalipokea vifaa vichache vya usajili. Mwandishi anatumia kitenzi hicho kuonyesha kwamba IEBC ina uhakika wa mambo inayosema.

### 3.2.3 Vielezi

Vielezi ni aina ya maneno yanayofafanua kitendo. Vielezi vya jinsi vinaweza kutumiwa na mhariri kuonyesha mtazamo wake kuhusu jinsi kitendo fulani kilivyofanyika au kitakavyofanyika. Kwa mfano,

*1. Kuwaruhusu wabunge kuendelea kufuja pesa za mlipa ushuru bila ya kujali kuchukuliwa hatua, kutafanya Wakenya waamini kuwa ufisadi ni jambo la kawaida. Hili ni jambo ambalo lisiposhughulikiwa ipasavyo litaangamiza kabisa uchumi, maadili na utaifa wa Kenya.(Taifa Leo 09/02/2016)*

*2. Tunatarajia mamilioni ya pesa ambazo zilitumiwa kupumbaza maafisa wa umma kwa kuwaruhusu kusafiri nje ya nchi mara kwa mara bila sababu, sasa zitapata kutumiwa katika miradi muhimu itakayoendeleza mbele maendeleo. (Taifa Leo 12/02/2016)*

*3. Tunatarajia uchunguzi utafanywa kikamilifu safari hii, na hatua zitachukuliwa dhidi ya wale wote watakaopatikana na hatia bila kubagua yeyote kisiasa wala kimamlaka. (Taifa Leo 19/02/2016)*

*4. Kufutwa kwa maafisa hao ni tukio moja tu. (Taifa Leo 25/01/2016)*

*5. <u>Bila shaka</u> matarajio ya timu hizi mbili kujiinua kurejesha mashabiki viwanjani kuimarisha msisimuko mbali na kuchangia kukuza soka ya kitaifa hasa Harambee Stars, sasa yamepigwa jeki. (Taifa Leo 01/02/2016)*

Katika mfano wa 1, mwandishi ametaja kiwango cha uharibifu ambao unaweza kutokea iwapo ufisadi hautapigwa vita, kwa kutumia kielezi *kabisa*. Madhara ya ufisadi katika taifa la Kenya ni pamoja na kuangamiza uchumi na kupanua mwanya kati ya matajiri na maskini. Maadili yatadidimia kwa sababu vizazi vijavyo vitarithi tabia za ufisadi. Itakuwa vigumu kwa Wakenya kuungana kama taifa moja kwa sababu ya chuki na kutoaminiana kati ya watawala na watawaliwa.

Katika mfano wa 2, mwandishi ametumia kielezi 'mara kwa mara' na 'bila sababu' kuonyesha kuwa safari za maafisa wa umma zimezidi, na kwamba safari hizo hazina manufaa yoyote kwa taifa. Maafisa wa umma na madiwani wamekuwa wakisafiri ng'ambo, safari ambazo zinagharimu serikali pesa nyingi sana ambazo zingetumiwa kwa miradi ya maendeleo.

Katika mfano wa 3, madai ya ufisadi dhidi ya Waziri wa Ugatuzi Bi Ann Waiguru yametia doa utendakazi wa EACC kwani ilikuwa imetangaza kuwa Bi Waiguru hakuwa na hatia yoyote. EACC imelazimika kuchunguza upya madai hayo. Mwandishi anatumia kielezi *mara hii* kumaanisha uchunguzi utarudiwa kwa mara nyingine na matarajio yake ni kuwa uchunguzi utakapofanywa tena, utakuwa mkamilifu na usio na dosari.

Hisia za mwandishi zinadhihirika jinsi alivyoteua maneno katika mfano wa 4. Kielezi '*tu*' kinaashiria kwamba hajaridhika na hatua ya kuwafuta kazi maafisa wa polisi. Hatua nyingine zaidi yafaa kuchukuliwa ili kusuluhisha tatizo hilo na mengine yanayohusiana nayo. Mwandishi anapendekeza kuwe na sera maalum ya kupambana na ufisadi. Kuwe na utaratibu unaotambuliwa na raia kuhusu usikizaji na uamuzi kuhusiana na kesi za ufisadi.

Matumizi ya kielezi *bila shaka* katika mfano wa 5, inaonyesha uhakika alionao mwandishi kwa yale anayosema. Ana hakika kwamba ufadhili uliopewa timu ya kitaifa ya Harambee Stars utaimarisha soka humu nchini.

### 3.2.4 Virai

Kirai ni neno au fungu la maneno lililodokeza maana lakini maana hiyo si kamilifu. Haina muundo wa kiima – kiarifu kama ule wa sentensi. Kinabeba tu sehemu ya sentensi. TUKI (2004) inadai kuwa kirai ni kipashio cha kimuundo kinachoundwa na neno moja au zaidi na hakina mwingiliano wa kimuundo wa kiima – kiarifa. Massamba (2004) anadai kuwa kirai ni kipashio cha kimuundo chenye zaidi ya neno moja lakini ambacho hakina uhusiano wa kiima – kiarifa (yaani hakihusishi mtendaji wa tendo na tendo lililotendwa.) Mifano ya virai katika gazeti la *Taifa Leo* yalibainika katika sentensi zifuatazo:

*1.<u>Kama desturi;</u> Klabu za Kenya zinaelekea kuleta aibu kwenye soka ya shirikisho la [Caf]. Hii ilionekana wiki jana baada ya Gor Mahia na Bandari Fc kutandikwa na timu pinzani kwenye mashindano ya klabu Bingwa Afrika na kombe ya Afrika, mtawalia. (Taifa Leo 20/02/2016)*

Katika mfano wa 1, mwandishi anatumia kirai 'kama desturi' kuashiria mwelekeo wake kuhusu klabu za Kenya. Inaonekana kwamba timu za soka humu nchini zina mazoea ya kufanya vibaya kwenye mashindano. Dalili za kushindwa kwa timu hizi zimeanza kuonekana. Mwandishi haoni matumaini ya timu hizi kushinda.

*2.<u>Litakuwa jambo la busara</u> endapo viongozi wa Cord watawasiliana na IEBC ili waelewe dosari zilizosababasha pendekezo lao kukataliwa.(Taifa Leo 24/03/2016)*

Mwandishi anatoa mapendekezo yake anapotanguliza kwa kirai 'litakuwa jambo la busara'. Hili linafuatia mtafaruku uliopo kati ya Cord na IEBC. Muungano wa Cord ulihisi kwamba Jubilee ilishirikiana na IEBC kuzima kura ya maamuzi ya 'Okoa Kenya'. Mwandishi anahofia kuwa kunaweza kuzuka kwa maandamano ya Cord na wafuasi wake.

*3.<u>Si siri kuwa</u> walimu katika shule za umma hufanya kazi katika mandhari duni mno, kuliko wenzao walio wa shule za kibinafsi.(Taifa Leo 21/03/2016)*

Mwandishi katika mfano wa 3 anatanguliza sentensi kwa kutumia kikanushi *si,* kwa madhumuni maalum. Inawezekana kuwa kunao watu fulani wanaotaka tuamini kwamba walimu wa shule za kibinafsi na wa shule za umma wanafanya kazi kiwango

kinachofanana. Kwa hivyo mwandishi huyu anafichua uhalisi wa mambo na ndio sababu moja inayofanya shule za umma zisifanye vyema kwenye mitihani ya kitaifa.

*4.<u>Wito wetu ni kuwa</u> hatua ichukuliwe kuepusha ghasia kwa sababu hali kama hiyo inaweza kutikiza uthabiti telezi tunaofurahia nchini kwa sasa.(Taifa Leo 24/03/2016)*

Msimamo wa mwandishi wa tahariri unaibuliwa kwa kirai kitangulizi 'wito wetu ni kuwa' katika mfano wa 4. Mtafaruku uliopo kati ya Cord na IEBC unaweza kuibua ghasia iwapo suluhisho halitapatikana. Mwandishi anapendekeza tume ya IEBC kuwaita viongozi wa upinzani na kuweka bayana mfumo uliotumiwa kukagua sahihi zilizowasilishwa.

*5.<u>Ukweli uliopo ni kuwa</u> hapatakuwa na mabadiliko kwenye matokeo ya wanafunzi kama walimu wakuu watabadilishwa ilhali mandhari wa utoaji wa elimu bado ni mabovu.(Taifa Leo 21/03/2016)*

Katika mfano wa 5, serikali inapaswa kuzingatia 'ukweli uliopo' kwamba mandhari ya utoaji elimu yanapaswa kubadilishwa, mbali na kubadilisha walimu wakuu. Kuna uwezekano kwamba sababu zingine zinachangia matokeo mabaya ya wanafunzi. Mwandishi anapendekeza hatua nyingine kuchukuliwa, baada ya ukweli uliopo kutambuliwa.

*6. <u>Tunatumai kuwa</u> safari hii, Wakenya watatumia silaha muhimu ya kura kuzuia ulafi huu ambao umepita mipaka. (Taifa Leo 22/02/2016)*

Kinachodokezwa na mwandishi katika mfano wa 6, ni kwamba wananchi wa Kenya hawajatumia silaha yao vizuri wanapowateua viongozi watakaowaongoza. Wamekuwa wakichagua viongozi pasipo kuzingatia sifa zao, viongozi waliojawa na tamaa na ulafi, wasiojali mahitaji ya wananchi. Kwa sababu sasa wametambua ulafi walionao viongozi, mwandishi anasema *tunatumai kuwa* Wakenya wamepata funzo, na kwamba wataweza kufanya uchaguzi wa busara ifikapo mwaka ujao (2017).

*7. <u>Labda hekima tunayoweza kufanya</u> kwa sasa ni kusubiri kuona jinsi Okumbi atakavyofanikisha timu hii ndiposa ibainike iwapo mrithi kutoka ng'ambo atatafutwa au la.(Taifa Leo 27/02/2016)*

Katika mfano wa 7, mwelekeo wa mwandishi kuhusiana na kocha mpya wa Harambee Stars unaonyeshwa na maneno anayoteua; *labda hekima tunayoweza kufanya*.

Mwandishi wa tahariri hii hana imani na kocha aliyeteuliwa kuongoza timu ya kitaifa. Mwandishi anampa kocha huyo muda, yuko radhi kusubiri mpaka aone iwapo ataweza au atashindwa. Lakini kwa mtazamo wake (mhariri) kuna uwezekano mkubwa wa Okumbi kushindwa, na kocha mwingine mrithi wa ng'ambo kutafutwa.

*8.Ni vyema rais kuzingatia ripoti ya IPOA (Mamlaka Huru ya Kuchunguza Utendakazi wa Idara ya Polisi) kabla ya kuharakisha shughuli ya kuongeza maafisa wa polisi nchini.(Taifa Leo 03/03/2016)*

Katika mfano wa 8 mwandishi anatumia kirai *ni vyema* kutoa maoni yake kuhusu hali ya maafisa wa polisi. Kinachohitaji kupewa kipaumbele, kulingana na mhariri, ni kushughulikiwa kwa mahitaji ya polisi kisha baadaye polisi zaidi kuongezwa. Hii ni kufuatia agizo alilotoa Rais Uhuru Kenyatta la kusajiliwa kwa makurutu 10,000 ili kuimarisha hali ya usalama nchini. Mwandishi wa tahariri hii anapendekeza kuwa rais azingatie ripoti ya IPOA kabla ya kuongeza maafisa wa polisi. Ripoti ya IPOA ilionyesha kuwa maafisa wa polisi wanaishi kwa mazingira mabovu, hali ambayo inaathiri utendakazi wa polisi.

*9. Ni aibu kuwa na idadi kubwa ya polisi ambao wanaishi kwa vyumba vidogo wanavyofinyana licha ya kuwa wengine wameoa na wana haki ya kulinda maisha yao ya kibinafsi.(Taifa Leo 03/03/2016)*

Hali ya maafisa wa polisi kukosa makazi bora inakashifiwa na mwandishi kwa kutumia maneno *ni aibu* katika mfano wa 9. Anaeleza kuwa takriban polisi 58,000 hawana nyumba mwafaka za kuishi. Hali hii ya ukosefu wa nyumba kama anavyoeleza mhariri, ilisababisha maafisa wa polisi kujinyonga na kuchangia mizozo miongoni mwao. Hii ndio sababu mwandishi anaeleza kuwa ni aibu.

*10. Kilicho wazi ni kwamba wanasiasa hao wanapanda hisia za chuki miongoni mwa Wakenya.(Taifa Leo 07/01/2016)*

Kirai *kilicho wazi ni kwamba* katika mfano wa 10, kinadokeza kuwa anachosema mhariri ni jambo ambalo silo siri tena. Bw. Suleiman Shahbal alisikika akisema kuwa serikali inapanga kushinda katika Uchaguzi Mkuu wa 2017 kwa njia zozote zile. Kwa upande mwingine, kiongozi wa upinzani ambaye pia ni kinara wa Cord Bwana Raila Odinga alidai kwamba serikali ina njama ya kuiba katika uchaguzi mkuu ujao. Matamshi haya ya wanasiasa wanaweza kueneza chuki na uchochezi kwa wananchi.

Mwandishi hivyo basi anashangaa kwa nini hatua za kisheria hazijachukuliwa dhidi ya viongozi ambao wanapanda hisia za chuki.

*11.Imedhihirika kuwa teknolojia hupelekea kurahisisha utoaji wa huduma na hata wakati mwingi hupunguzia wateja gharama ya kupokea huduma tofauti.(Taifa Leo 05/02/2016)*

Katika mfano wa 11, mwandishi anaanza kauli yake kwa kirai 'imedhihiria kuwa'. Hii inaonyesha kuwa ana uhakika wa anayoyasema. Anaeleza kuwa Kampuni ya Uber inatumia mbinu za kisasa kufanya biashara ya teksi jijini Nairobi. Kampuni hiyo imetumia mbinu za kisasa kujipunguzia gharama ya matumizi katika biashara na hivyo kupunguza ada inayotozwa kwa wateja wao. Wateja wengi watakuwa wakitafuta huduma zao kwa sababu ya gharama ya chini. Mhariri anaeleza jinsi benki zimeshirikiana na kampuni ya Safaricom ili kurahisisha utumaji wa pesa. Mifano aliyotoa mwandishi ndiyo inayomfanya awe na uhakika na kusema 'imedhihirika kuwa'.

## 3.3 Toni

Toni ya mwandishi kurejelea suala linalozungumziwa inadhihirika kupitia maneno anayoteua mwandishi. Toni inaweza kuwa ya huzuni, kukashifu, kukata tamaa, kusikitisha, kuwa na matumaini, ua ya kupongeza.

### 3.3.1 Toni ya huzuni

Toni ya huzuni imedhihirika kupitia uteuzi wa maneno ambayo mwandishi ameyatumia. Mifano ifuatayo kutoka gazeti la *Taifa Leo* inabeba toni ya huzuni:

*1.Ni jambo la kuhuzunisha kwamba wakulima ambao ndio wanaomenyeka zaidi katika shughuli ya kuwatafutia watu riziki, huishia kuwa hohehahe bila ya pesa mfukoni. Kinyume chake, watu ambao hawajui hata jembe linavyoshikwa, ndio wanaofurahia manoti na faida kubwa. (Taifa Leo 16/02/2016)*

*2. Kifo cha Bw Salah Farah, aliyewaokoa abiria Wakristo katika shambulio dhidi ya basi moja mwezi Desemba mwaka uliopita katika eneo la Mandera ni cha kuhuzunisha.(Taifa Leo 19/01/2016)*

Toni ya huzuni inadhihirika jinsi mwandishi anavyoteua manenona kuyatumia. Katika mfano wa 1, *inahuzunisha* kuona jinsi wakulima wanavyopitia shida ya kazi kubwa bila mapato, wanafanya kazi nyingi lakini faida huwaendea wengine ambao huwa wanastarehe. Pia katika mfano wa 2, kifo cha Salah kinasababisha huzuni. Bw. Salah aliokoa maabiria Wakristo katika shambulio kule Mandera. Kifo chake kinahuzunisha hasa baada ya yeye kuhusika katika kitendo cha utu na ubinadamu kiasi hicho.

### 3.3.2 Toni ya kukashifu

Toni ya kukashifu inaonekana katika mifano ifuatayo ya *Taifa Leo:*

*3. Kitendo cha maafisa hao hakikustahili, lakini kinatilia nguvu ripoti mbalimbali za mashirika ya kama Transparency International(TI),kwamba kuna uozo na ufisadi katika idara ya polisi Kenya.(Taifa Leo 25/01/2016)*

*4. Ijapokuwa hakuna visa vikubwa vya ghasia vilivyoripotiwa, kuna mapungufu kadhaa yaliyojitokeza ambayo yanapaswa kukemewa.(Taifa Leo 21/02/2016)*

*5.Ikiwa ni kukosoana, si lazima serikali itumie vikosi vya usalama kuuhangaisha Upinzani, au viongozi wa Upinzani kuanza kuwatukana wenzao Serikalini.(Taifa Leo 21/02/2016)*

Katika mfano wa 3, mwandishi anaeleza kuwa maafisa wa trafiki waliitisha hongo barabarani hadharani, walifanya kitendo kinachofaa kukashifiwa, mwandishi anasema kuwa 'kitendo hicho hakikustahili'. Maafisa hao wa Mombasa hawakujali kuwa rais alikuwa katika eneo hilo, pamoja na wakuu wengine serikalini.

Toni ya kukashifu inadhihirika pia katika mifano ya 4 na 5, wakati mwandishi *anakemea* kitendo cha serikali kuuhangaisha upinzani. Serikali ya Rais Museveni ilitumia vitoa machozi, na vikosi vya usalama kumhangaisha kiongozi wa upinzani Dkt. Kizza Besigye na wafuasi wake jambo ambalo mwandishi anaona kuwa *si lazima*.

### 3.3.3 Toni ya kukata tamaa

Vile vile, toni ya kukata tamaa imedhihirika katika mifano ifuatayo ya *Taifa Leo;*

*6. Hatua ya madiwani kupinga mswada unaolenga kuinua kiwango chao cha elimu ya wanaotaka wadhifa huo ni ya kuvunja moyo.(Taifa Leo 27/01/2016)*

*7. Itakuwa vigumu kushinda vita ufisadi ikiwa wabunge wanaoshiriki uovu huo hawatachukuliwa hatua za kisheria.(Taifa Leo 09/02/2016)*

Mwandishi katika mfano wa 6 anaelezea kitendo cha madiwani kupinga mswada unaolenga kuinua kiwango chao cha elimu, ni kitendo cha *kuvunja moyo* kwa sababu madiwani wanapaswa kuwa mfano mzuri kwa vijana kwa kuunga mkono miswada kama hiyo.

Katika mfano wa 7, mwandishi anaonyesha kukata tamaa kwenye mapambano dhidi ya ufisadi, kwa sababu hatua za kisheria hazichukuliwi kwa wale wanaopatikana na hatia. Anaposema *itakuwa vigumu,* anaonekana kukata tamaa. Wabunge wanaohusika katika ufisadi wanaachwa bila kuhukumiwa, jambo hili linafisha mioyo wakenya wanaosubiri wakitumaini kuwa sheria itafanya kazi.

**3.3.4 Toni ya kusikitisha**

Mwandishi wa tahariri ya *Taifa leo* ameteua maneno yanayoonyesha toni ya kusikitisha, katika mfano ufuatao;

8. *Ufichuzi kwamba wabunge wetu wamekubaliana walipwe mishahara ya miezi minane ambapo hawatakuwa bungeni unasikitisha.(Taifa Leo 22/02/2016)*

Katika mfano wa 8, inasikitisha kuwa wabunge wanapanga njama ya kulipwa mshahara hata baada ya muda wao wa kuhudumu bungeni utakuwa umekwisha. Inaonyesha vile wabunge wasivyojali maslahi ya wananchi ambao ni walipa ushuru. Wabunge wanatumia uwezo na mamlaka walionao kujipitishia miswada itakayowafaidi wao wenyewe.

**3.3.5 Toni ya kuwa na matumaini**

Mfano ufuatao kutoka tahariri ya *Taifa leo* unadhihirisha toni ya kuwa na matumaini;

9. *Ni jambo la kutia moyo kuwa mashirika sasa yameanza kujitokeza kudhamini baadhi ya klabu za nchini humu ambazo zimekuwa zikisaka hisani kama hiyo bila mafanikio.*(*Taifa Leo 30/01/2016)*

Katika mfano wa 9, kuna matumaini sasa ya timu za Gor Mahia na AFC Leopards kufanya vyema katika mashindano yajayo. Hii ni baada ya klabu hizi za soka kupata ufadhili ambao walikuwa wakisubiri, mwandishi anaona kuwa jambo hilo ni la *kutia moyo.* Shirika la ubashiri la Sportpesa lilijitwika jukumu la kudhamini ligi kuu ya Kenya.

Vilevile, mwandishi wa tahariri ya *Taifa leo* hii ametumia toni ya kuhimiza katika mfano huu;

*11.Wahudumu wa teksi jijini Nairobi wanafaa kukubali tuko katika enzi za kiteknolojia na waanze kukumbatia teknolojia za kisasa kuendeleza biashara zao.(Taifa Leo 05/02/2016)*

Mwandishi anawahimiza wahudumu wa teksi anaposema *wanafaa kukubali* kuwa teknolojia ni jambo ambalo haliwezi kupingwa. Anawahimiza wahudumu wa teksi wajifunze kutokana na mbinu ambazo kampuni ya Uber inatumia. Mwandishi anaeleza kuwa tuko katika enzi za kiteknolojia, kwa hivyo tunapaswa kujitayarisha kwa mabadiliko ambayo yataathiri shughuli zetu.

### 3.3.6 Toni ya kupongeza

Mwandishi wa tahariri anatumia maneno yanayoonyesha toni ya kupongeza katika mfano huu;

12. *Hatua ya serikali kuamua kupunguza kwa asilimia 50 bajeti inayotumiwa kwa usafiri wa maafisa wakuu wa umma ni ya kupongezwa. (Taifa Leo 12/02/2016)*

Serikali imechukua hatua nzuri inayohitaji *kupongezwa*, hatua ya kupunguza asilimia 50 bajeti inayotumiwa kwa usafiri wa maafisa wa umma inaonyesha kuwa serikali iko tayari kutunza mali ya umma kwa niaba ya mwananchi. Mhariri ametaja safari za maafisa wa umma kuwa ni safari za mara kwa mara na ambazo hazina sababu.

## 3.4 Sentensi

Sentensi imeelezwa na Habwe na Karanja (2004) kama mtungo wa lugha wenye kiimana kiarifa. Wanaeleza kuwa, kimuundo sentensi zinaweza kuainishwa kwa msingi wa umbo lake. Kunazo aina kuu tatu za sentensi:

i) Sentensi sahili

ii) Sentensi ambatano

iii) Sentensi changamano

### 3.4.1 Sentensi sahili

Sentensi sahili ni sentensi ambayo ina kitenzi kikuu kimoja. Sentensi ya aina hii si lazima iwe rahisi kueleweka kimaana au iwe fupi katika muundo wake. Sentensi sahili hueleza wazo moja tu ambalo hubebwa na kushazi kikuu kimoja. Mifano ya sentensi sahili kwenye tahariri ya *Taifa Leo* ni kama :

*1.<u>Tulitarajia kuona</u> makali ya NTSA.( Taifa Leo 26/01/2016)*

*2.Yeye <u>ni</u> kafara ya ujumbe wa ukweli.(Taifa Leo 19 /01/2016)*

*3. Tiba <u>ni</u> viongozi kuchukua hatua kali za kisheria.(Taifa Leo 07/01/2016)*

*4. Kwanza, majukumu yao <u>yanahitaji wawe</u> na elimu ya kutosha.(Taifa Leo 27/01/2016)*

*5.Tangu leo, matokeo ya msimamo mkali wa Bw Michuki <u>yangali dhahiri</u>.(Taifa Leo 26/01/2016)*

*6.Kilimo kwa miaka mingi <u>kimechukuliwa kuwa</u> uti wa mgongo wa nchi yetu.(Taifa Leo 16/02/2016)*

Sentensi ya 1 inabeba wazo moja kuu, linalodokezwa na vitenzi 'tulitarajia kuona'. Sentensi hii sahili inaeleweka moja kwa moja kuwa matarajio ya kuona NTSA ikitekeleza wajibu wake hayakutimia.

Sentensi ya 2 inatuarifu sifa moja ya Bw. Salah isiyopingika, analinganishwa na kafara kwani alijitolea kuwaokoa wengine pasipo kujali usalama wake. Kitenzi kishirikishi 'ni' kimetumiwa.

Yeye / ni kafara ya ujumbe wa ukweli.

KN KT

Sentensi sahili huwa na kitenzi kimoja au wazo moja kuu. Katika mfano wa 4, wazo moja linabebwa na vitenzi viwili sambamba ‘yanahitaji wawe’ na ‘yangali dhahiri’ katika mfano wa 5.

Tangu leo, matokeo ya msimamo mkali wa Bw Michuki / yangali dhahiri.

KN KT

Mwandishi anapotumia sentensi sahili, ujumbe unawasilishwa kwa njia ya moja kwa moja bila kusababisha utata wowote kwa msomaji.

### 3.4.2 Sentensi ambatano

Habwe na Karanja (2004) wanaeleza kuwa sentensi ambatano huwa na vishazi huru viwili au zaidi ndani yake.Vishazi huru ambavyo navyo huwa sentensi sahili huambatana kwa kutumia viunganishi. Mifano ifuatayo ya sentensi ambatano zimetumiwa na mhariri wa *Taifa Leo*

*7. Wahudumu wa teksi jijini Nairobi wanafaa kukubali tuko katika enzi za teknolojia* <u>*na*</u> *waanze kukumbatia teknolojia za kisasa kuendeleza biashara zao.(Taifa Leo 05/02/2016)*

*8.Bengi hizo zilipinga mtindo huo wa utoaji wa huduma za pesa* <u>*na*</u> *kulalamika biashara zao zingeathirika vibaya.(Taifa Leo 05/02/2016)*

*9. IPOA* <u>*hata hivyo*</u>*, imekiri kuwa haina mamlaka ya kufanya uchunguzi dhidi ya NPSC. (Taifa Leo 10/02/2016)*

*10.*<u>*Kwa upana*</u>*, watoto hao huanza kukumbwa na changamoto za kimaisha wakiwa wangali wachanga.(Taifa Leo 07/02/2016)*

*12.Itakuwa aibu* <u>*ikiwa*</u> *utawala uliopo utakumbukwa kwa kufanya safari nyingi zaidi nje ya nchi bila kujali maslahi ya wananchi.(Taifa Leo 12/02/2016)*

Sentensi mfano wa 7, imeundwa kwa kuambatanisha sentensi sahili mbili na kutumia kiunganishi *na*:

S [$S_1$(KN+KT)+U+$S_2$(KN + KT)]

$S_1$ Wahudumu wa teksi jijini Nairobi /wanafaa kukubali tuko katika enzi za teknolojia.

KN KT

$S_2$ Wahudumu wa teksi / waanze kukumbatia teknolojia za kisasa kuendeleza biashara zao .

KN KT

Sentensi mfano wa 8, imeundwa kwa sentensi mbili zinazohusiana:

$S_1$ Bengi hizo / zilipinga mtindo huo wa utoaji wa huduma za pesa.

KN KT

$S_2$ Bengi / zililalamika kuwa biashara zao zingeathirika vibaya.

*KN KT*

### 3.4.3 Sentensi changamano

Aina hii ya sentensi huwa na angalau kishazi huru na kishazi kingine tegemezi. Sentensi hii inaweza kuwa na vishazi tegemezi viwili (Habwe na Karanja, 2004). Zifuatazo ni mifano ya sentensi changamano kutoka kwa tahariri ya gazeti la *Taifa Leo:*

*13. Sharti serikali itoe mikakati na mwongozo wa uchimbaji madini na mafuta kabla ya matapeli wa ughaibuni hawajaibuka na kugeuza Kenya kuwa kama mataifa ya Kiarabu ambayo yana utajiri mkubwa wa mafuta lakini wenyeji wanataabika kwa sababu ya mizozo.(Taifa Leo 18/03/2016)*

*14. Kwa hivyo, wakati inapowatafutia masoko ya moja kwa moja, itakuwa vyema pia iwapo itahakikisha kuwa, mbolea ya bei nafuu pamoja na matingatinga miongoni mwa vifaa vingine vya shambani, vinapatikana kwa bei nafuu kwa wakulima.(Taifa Leo 16/02/2016)*

Sentensi ya 13 ni changamano kwa sababu imeundwa kwa kishazi huru na kishazi tegemezi kama ifuatavyo:

Kishazi huru

Sharti serikali itoe mikakati na mwongozo wa uchimbaji madini  na mafuta kabla ya matapeli wa ughaibuni hawajaibuka na kugeuza Kenya kuwa kama mataifa ya Kiarabu.

Kishazi tegemezi

Ambayo yana utajiri mkubwa wa mafuta lakini wenyeji wanataabika kwa sababu ya mizozo.

Sentensi hii ina mawazo mengi yaliyojumuishwa kuwa sentensi moja. Inazungumzia serikali kutoa mikakati , kisha matapeli wa ughaibuni wanaoweza kunyonya raslimali ya taifa, na mataifa ya kiarabu yanayotaabika kwa sababu ya mizozo.

Sentensi ya 14 imeanza kwa kishazi tegemezi;

Kishazi tegemezi  (Kwa hivyo, wakati inapowatafutia masoko ya moja kwa moja,)

Kishazi huru (. . . itakuwa vyema pia iwapo itahakikisha kuwa, mbolea ya bei nafuu pamoja na matingatinga miongoni mwa vifaa vingine vya shambani, vinapatikana kwa bei nafuu kwa wakulima.)

Matumizi ya sentensi changamano inamwezesha mwandishi kuwasilisha mawazo mengi yanayohusiana katika katika sentensi moja.

### 3.5 Sajili za lugha

Iribemwangi na Mukhwana (2011) wanaeleza kuwa sajili ni taaluma ya isimujamii ambayo humaanisha kaida na mikondo ya kimawasiliano itumiwayo katika hali na miktadha fulani kwa madhumuni fulani maalumu. Waandishi wa tahariri ya *Taifa Leo* wamegusia masuala anuai ya kijamii, kisiasa, elimu, maadili, usalama na mengine mengi. Ili mwandishi afaulu kueleza ujumbe wake kwa njia mwafaka, ieleweke na msomaji, ameweza kuteua msamiati unaofaa kuelezea mada husika. Msamiati mwafaka unasaidia uelewekaji wa ujumbe unaopitishwa.

Mwandishi anapoandika kuhusu michezo, anatumia msamiati unaolingana na anachoandika. Ametaja timu za kandanda nchini kama vile *AFC Leopards, Harambee Stars, Gor Mahia, (Kogalo). (Taifa Leo, 01/02/2016)* Ametaja pia majina ya mechi ya

viwango tofauti kama vile *mechi ya Klabu Bingwa Afrika (Caf). (Taifa Leo, 27/02/2016)* Mwandishi pia ametaja mashirika yanayofadhili timu hizo, kwa mfano *Sportpesa, mCHEZA, Betway, Mumias Sugar (Taifa Leo, 01/01/2016).* Msamiati mwingine uliotumika ni *ligi, soka, kabumbu, kocha, kandanda, msimu, kutia saini mkataba, udhamini n.k (Taifa Leo, 01/01/2016).*

Mbali na msamiati wa michezo, mwandishi pia ametumia msamiati wa usafiri. Mifano ni: *NTSA (Halmashauri Ya Kitaifa Ya Uchukuzi Na Usafiri), vidhibiti mwendo, mikanda ya usalama, sheria za trafiki, Waziri wa Uchukuzi, eksozi, sekta ya uchukuzi na sekta ya matatu (Taifa leo, 26/01/2016), nauli na teksi (Taifa Leo, 05/02/2016).*

Msamiati unaorejelea kilimo ni: *matingatinga, kilimo cha kahawa, majani, pareto, tumbaku, miwa, mbolea, Waziri wa Kilimo, jembe, pembejeo za kilimo, mazao, masoko, kilimo ni uti wa mgongo wa nchi (Taifa Leo,16/02/2016).*

Waandishi wa tahariri ya *Taifa Leo* wamezua mijadala kuhusu siasa nchini Kenya na mataifa mengine, wamefaulu kupitisha ujumbe wao kwa kutumia msamiati unaohusu siasa, majina ya vyama, uongozi, na taasisi mbalimbali za uongozi. Baadhi ya mifano ni kama ifuatayo: *Bunge, ufisadi, Rais, sera rasmi, uchumi, (Taifa Leo 25/01/2016), mlipa ushuru, spika, (NCSC) Muungano wa Mashirika ya Umma (Taifa Leo, 09/02/2016), kura, uchaguzi, miradi yamaendeleo, bajeti, seneti, ugatuzi, madiwani, maafisa wakuu wa umma, mataifa ya kigeni (Taifa Leo,12/02/2016), serikali za kaunti, mawaziri, Kanu, demokrasia, upinzani, serikali, changuzi ndogo, upinzani, (Taifa Leo 07/03/2016), Okoa Kenya, Cord, Jubilee, mfumo wa sheria, kura ya maamuzi, haki, upinzani (Taifa Leo 24/03/2016), mswada wa rushwa, janga la kitaifa, serikali kuu. (Taifa Leo, 25/03/2016)*

Mwandishi ametumia msamiati unaohusu elimu ili aweze kufafanua ujumbe ipasavyo. Mifano ya maneno hayo ni*: KCSE, (Mtihani wa Kitaifa wa Shule za upili) Knec (Barasa la Mitihani ya kitaifa ) na mtalaa wa elimu, Wizara ya Elimu, Tume ya Kuajiri Walimu (TSC) Waziri wa Elimu Dkt. Fred Matiangi, shule za umma, shule za kibinafsi, vyama vya walimu, matokeo ya wanafunzi, madarasa , walimu wakuu. (Taifa Leo 21/03/2016)*

Msamiati wa biashara umetumiwa na mwandishi ili kufanikisha ujumbe wake. Mifano ya msamiati huo ni: *kandarasi, fidia, wawekezaji, zabuni, kampuni, madini ya mafuta, masoko, utajiri, raslimali na leseni.(Taifa leo 18/03/2016)*

Msamiati unaorejelea usalama: *polisi, Mamlaka Huru ya Kuchunguza Utendakazi wa Idara ya Polisi [IPOA], raia , makurutu, wanajeshi, Tume ya Kitaifa ya Huduma kwa Polisi [NPSC], malalamishi, haki, vitisho, uchunguzi, ulinzi, uchochezi, ghasia, hisia za chuki.(Taifa leo 10/02/2016)*

**3.6 Matumizi ya takwimu**

Matumizi ya takwimu ilipendekezwa na Van Dijk (1988) na akadhihirisha kuwa takwimu zinatolewa wakati wa kunukuu kutoka kwa wanaohusika. Matukio yaliyoshuhudiwa moja kwa moja, mahojiano kutoka kwa walioshuhudia na kutoka kwa ripoti rasmi zilizopokelewa kutoka kwa watu na taasisi zilizo na nguvu na hadhi ya juu kisiasa. Van Dijk anaongeza kuwa matumizi ya takwimu hudhihirisha usahihi wa ujumbe na huonyesha umuhimu wake. Kwa hivyo takwimu ni mbinu muhimu ya kibalagha.

Mwandishi ametumia takwimu katika mifano hii:

*Lakini wasiwasi ni kuwa wabunge wakipitisha pesa hizo, wawakilishi wa wadi zaidi ya 1300 nao watataka walipwe karibu sh1milioni kila mmojakwa muda huo. Kuna magavana 47 ambao mshahara wao ni sh 1.1 milioni. . . Kwani Kenya ina utajiri kiasi gani, hata iwalipe mishahara zaidi ya watu 1500 kwa miezi minane wakiwa hawafanyi kazi yoyote ya kuwatumikia wananchi?(Taifa Leo* 22/02/2016)

Takwimu zimetumika ili kufichua kiasi cha pesa ambazo wabunge wananuia kulipwa baada ya muda wao wa kuhudumu kumalizika. Msomaji anajulishwa kuwa magavana 47 watataka walipwe sh 1.1 milioni kila mwezi huku wawakilishi wa wadi 1,300 nao walipwe sh1 milioni. Kwa miezi minane mlipa ushuru atagharimika kulipa pesa nyingi sana. Bila shaka, takwimu hizi zitatoa picha halisi ya viongozi ambao wanaweza kutumia kila mbinu kujipatia pesa na mali ya umma hata mahali wasipostahili.

Mwandishi wa tahariri pia ametumia takwimu zifuatazo;

*Wadi zenye ukubwa wa kilomita 30 kwa mraba kuenda chini zilikabidhiwa kifaa kimoja, na zilizo na kilomita kati ya 31 na 500 zikapewa vifaa viwili.*(*Taifa Leo*15/02/2016)

Mwandishi anatumia takwimu ili kuonyesha tofauti kubwa  inayotokana na ugavi usio sawa wa vifaa vya kuandikisha wapigakura. Huu ni wakati ambapo upinzani unalalamika kuwa maeneo yaliyo na wafuasi wengi wa vyama vya upinzani vilipewa vifaa vichache. Kulingana na takwimu tulizopewa, vifaa viwili kwa eneo la kilomita kati ya 31 na 500 ni vichache mno ikilinganishwa na kifaa kimoja kwa eneo la kilomita 30 kwenda chini.

Mbali na takwimu kuhusu vifaa vya kujiandikisha,  mwandishi ametutajia idadi ya vitambulisho katika mfano ufuatao;

*Majuzi tulielezwa kuwa zaidi ya vitambulisho 500,000 viko katika afisi za usajili wa watu kote nchini.(Taifa Leo* 15/02/2016)

Takwimu hizi zinafichua utepetevu katika idara inayoshughulikia vitambulisho. Msomaji atajiuliza ni kwa nini vitambulisho vilivyo tayari kupewa wenyewe, vinaendelea kuhifadhiwa kwenye afisi za idara husika. Kinachozua maswali zaidi ni kwamba huu ni wakati ambapo usajili wa wapigakura unaendelea, kwa nini vitambulisho 500,000 vilivyo tayari viwekwe badala ya kupewa wenyewe ili wajiandikishe?

Mfano mwingine wa matumizi ya takwimu ni:

*Kulingana na madai hayo, maafisa wa NPSC wanaochunguza polisi wamekuwa wakipokea hongo ya kati ya sh300,000 na sh500,000 ili kuruhusu maafisa wenye maadili ya kutiliwa shaka kuendelea kuhudumu. (Taifa Leo* 10/02/2016)

Takwimu za kuonyesha kiasi cha pesa zinazopokezanwa kwa njia ya hongo ni ya kuatua moyo. Mwandishi anaeleza kuwa maafisa wanaochunguza maadili wanapokea hongo cha pesa sh300,000 na sh500,000. Mwandishi anapotupa takwimu hizi, uhalisi kwamba ufisadi umekolea sana katika idara za serikali ni dhahiri.

Takwimu pia zimetumiwa katika mfano ufuatao unaohusu NPSC:

*Tangu mwaka wa 2014 tume ya NPSC ikichunguza maafisa wa ngazi za juu katika idara ya polisi ambapo zaidi ya maafisa 1,200 wameruhusiwa kuendelea kuhudumu na wengine zaidi ya 60 wakaachishwa kazi. (Taifa Leo* 10/02/2016)

Maafisa wa polisi waliochunguzwa na kupatikana na hatia ni wengi sana. Maafisa 60 wameachishwa kazi huku wenzao 1,200 wakiruhusiwa kuendelea na kazi. Shughuli hiyo inaendelea kwa hivyo pengine maafisa wengi zaidi watapatikana na makosa

Mhariri wa *Taifa Leo* ametumia takwimu anapoelezea hali ya maafisa wa polisi;

*Rais Uhuru Kenyatta ameagiza kusajiliwa kwa makurutu 10,000 wapya wa polisi ili kuimarisha hali ya usalama nchini. . . Ripoti hiyo ilisema takriban polisi 58,000 hawana nyumba mwafaka za kuishi hali ambayo ilisababisha maafisa wa polisi kujinyonga na kuchangia mizozo miongoni mwao. (Taifa Leo* 03/03/2016)

Habari kwamba makurutu wengi wanasajiliwa, inawapa moyo wale vijana wanaotafuta kazi, vilevile inaweza kuchukuliwa kwamba ni ishara ya hatua za serikali kuimarisha usalama uliozorota tayari. Mwandishi pia anaeleza kuhusu idadi ya polisi ambao hawana nyumba. Polisi 58,000 in idadi kubwa sana, ufichuzi huu unaipa changamoto serikali ili kuingilia kati na kushughulikia mahitaji ya kimsingi ya polisi.

Mfano mwingine wa matumizi ya takwimu ni ufuatao;

*Tayari kumeripotiwa kashfa za utoaji zabuni za uchimbaji madini hali iliyopelekea aliyekuwa Waziri wa Madini Najib Balala kufutilia mbali kandarasi za kampuni 42... Baadhi ya maafisa wa serikali walidaiwa kupokea hongo ya sh80 milioni ili kutoa leseni kwa kampuni fulani za kuchimba madini.(Taifa Leo 18/03/2016)*

Kinachosikitisha ni kuwa, hata kabla ya madini hayo kuchimbwa, ufisadi umetangulia. Kandarasi za kampuni 42 zilifutiliwa mbali kwa sababu ya kashfa na madai ya hongo kiasi cha sh80 milioni. Matumizi ya takwimu hapa inampa msomaji picha halisi ya ufisadi unaoendelea.

Mbali na maelezo kuhusu kashfa kwenye sketa ya madini mwandishi ametupa mfano mwingine wa matumizi ya takwimu;

*Inasemekana kila shule ilihitajika kutoa sh 2000 mwaka uliopita kufadhili chama hicho, ambayo kwa jumla kitaifa, chama hicho kingepokea sh 65 milioni. (Taifa Leo 29/01/2016)*

Katika mfano huu ulaghai wa viongozi wa chama cha wazazi kinachoongozwa na Musau Ndunda unawekwa wazi. Kwa mujibu wa mhariri, chama hiki si halali lakini kimekuwa kikitoza shule sh 2,000 ili kufadhili shughuli za chama hicho. Tunaarifiwa kuwa jumla ya pesa ambazo chama kingekusanya kwa mwaka mmoja ni sh65 milioni.

Mwisho, takwimu zimetumiwa kuelezea shughuli ya kuwapiga msasa maafisa wa polisi, mwandishi anasema;

*. . . shughuli hiyo inayoendelea ya kuwapiga msasa zaidi ya maafisa 77,400 wa polisi. (Taifa Leo 10/02/2016)*

Idadi ya maafisa wa polisi wanayochunguzwa ni kubwa. Mwandishi amejumuisha takwimu katika maelezo yake ili tujue idadi kamili ya wanaochunguzwa. Mbali na hayo mwandishi anasema kuwa uchunguzi huu ulianza mwaka wa 2014 na bado unaendelea. Labda sababu ya zoezi hili kuchukua muda mrefu ni idadi kubwa (77,400) ya maafisa hao wanaochunguzwa.

**3.7 Uteuzi wa mada**

Mada ya habari ni muhtasari wa yale yanayoandikwa juu ya makala katika gazeti. Mara nyingi mada za habari haziandikwi kama sentensi kamili. Mchanganuzi yeyote anaweza kugundua kuwa vichwa hivi vinaweza kukosa nomino au vitenzi fulani. Sababu ya kuacha maneno hayo inaweza kuwa ni kufanya mada hiyo kuvutia zaidi na isiwe na *maneno* mengi. Maneno yaliyoachwa huweza kuwa ndiyo yanayobeba ujumbe ulio muhimu/mzito. Hivyo basi maneno yaliachwa kimaksudi ili isababishe taharuki na hivyo kuchochea msomaji kuendelea kusoma ili apate ujumbe kamili. Maneno ambayo huachwa kwenye mada ni vihusishi, vitenzi visaidizi, vivumishi vimilikishi na viunganishi.

Mwandishi wa tahariri ya *Taifa Leo* ameteua mada zinazofaa kueleza kwa muhtasari masuala anayozungumzia katika tahariri.

Mifano ifuatayo ya mada za tahariri ya *Taifa Leo* zimechanganuliwa:

i) *Uchochezi: Asasi husika ziwajibike* (*Taifa Leo* 7/1/2016)

Wahariri huteua maneno ambayo yanatoa muhtasari na kwa wakati huo huo, huonyesha mwelekeo wa jumba la habari. Kutokana na mada hii, ni wazi kwamba asasi zinazoshughulikia matamshi ya uchochezi hazijatekeleza kazi zao vizuri, ndio maana zinaelekezwa ziwajibike.

Mfano wa pili wa mada kutoka tahariri ya *Taifa Leo* ni;

ii)*Leopards msiache ufadhili ukateleza* (*Taifa Leo* 1/2/2016)

Mada hii inavutia nadhari ya wapenzi wa soka na hasa mashabiki wa timu za soka nchini. Inamweka msomaji akiwa na hamu (taharuki) ya kutaka kujua vipi Leopards inaweza kuacha ufadhili uteleze. Vinara wa klabu hii bila shaka watafanya lolote liwezekanalo ili wasipoteze ufadhili.

Mfano ufuatao unatumia swali la balagha;

*iii)Tutalipa wabunge sh2b kwa kazi gani?* (*Taifa Leo*22/2/2016)

Mada hii imetumia mbinu ya balagha ili kunasa makini ya msomaji. Kwa kutumia nafsi ya pili '*tutalipa,*' msomaji atahisi kuwa pamoja na mhariri huyu ambaye analalamikia sh2 bilioni zitakazolipwa kwa wabunge. Shilingi bilioni mbili ni pesa nyingi sana hasa kwa sababu ni ya mlipa ushuru. Msomaji hivyo basi, atahisi kama amehusika katika kuandika tahariri hii. Kwa hivyo mhariri amefaulu kwa kiasi kikubwa kumwathiri msomaji kupitia mada aliyoteua.

Mfano wa nne ni;

iv)*Pesa zilizookolewa ziendee maendeleo* (*Taifa Leo* 12/02/16)

Mada hii inatoa maelekezo kwa viongozi wanaohusika na kuandaa bajeti ya matumizi ya fedha za umma. Labda kunao viongozi waliokuwa na mipango ya kutumia pesa hizo kwa njia tofauti kinyume na miradi ya maendelo. Mwandishi pia ametumia mbinu ya taharuki kwa kutumia kishazi tegemezi *zilizookolewa.* Msomaji atataka kujua pesa hizi ziliokolewa kutoka wapi.

### 3.8 Hitimisho

Katika sura ya 3 tumeshughulikia uteuzi wa maneno na virai, sajili za lugha, miundo ya sentensi, toni, uteuzi wa mada na matumizi ya takwimu. Ili kuwasilisha ujumbe na kuonyesha mwelekeo wake, mwandishi ameteua na kutumia virai kama vile, *wito wetu ni kuwa, msimamo wetu ni kwamba, ni vyema, kauli yetu ni kuwa* n.k. Mwandishi ametumia vitenzi vya udhamiriaji kuonyesha uwezekano, ulazima na ubashiri. Miundo tofauti tofauti ya sentensi imetumiwa kwa lengo la kufanikisha ujumbe. Sentensi za miundo mbalimbali zimetumiwa kufanikisha uwasilishaji wa ujumbe.

# SURA YA NNE : MBINU ZA LUGHA NA TAMATHALI ZA USEMI

## 4.1 Utangulizi

Katika sura ya hii, tunachunguza tamathali za usemi na mbinu zingine za lugha. Tunafafanua matumizi ya misemo au nahau, sitiari, tashbihi, maswali ya balagha, kwelikinzani, taswira, kinaya, na kuonyesha vile tamathali hizi zinavyochangia katika kufanikisha ujumbe unaowasilishwa.

## 4.2 Tamathali za usemi

Tamathali za usemi ni fungu la maneno ambalo limegeuzwa maana yake ya kiurejelezi au asilia na kuwa na maana nyingine tofauti au mpya. Mbatia (2001) anaeleza kwamba tamathali ni ukiushi wa kimakusudi wa matumizi ya lugha katika viwango vya maana (semantiki) na mpangilio wa maneno (sintaksia) ili kuleta maana mpya au msisitizo. Matumizi ya tamathali za usemi ni muhimu kwa vile huwezesha ujumbe mkali au nyeti kuwasilishwa bila matokeo ya kuhujumu mpokezi wa ujumbe.

Wamitila (2008) ni mmoja wa wataalamu ambao wameshughulikia dhana hii. Wamitila anazungumzia tamathali za usemi kama ‘lugha ya kitamathali’. Anasema dhana ya tamathali inatumiwa kwa upana ili kujumlisha sifa nyingi za kimtindo ambazo hutumiwa katika kazi za kifasihi. Dhana hii hutumika kuelezea aina ya ukiushi wa kimakusudi katika matumizi ya lugha, na ukiushi huu unaweza kuwa wa kimaana au wa kimuundo. Katika ukiukaji huu, neno au kifungu fulani hutumiwa kwa maana ambayo ni tofauti na maana ya kimsingi.

Lugha ya kitamathali huwa na umuhimu mkubwa katika utunzi wa kazi za kifasihi. Wamitila anabainisha majukumu matatu makuu ya lugha ya kitamathali. Kwanza, ni urembeshaji wa kinachozungumziwa au kurejelewa na lugha hiyo na kukifanya kiwe na mvuto mkubwa wa kisanaa au kiumbuji; pili, ni jukumu la ufafanuaji au uelezaji wa kinachohusishwa na tamathali maalum; na tatu, jukumu la uthabitishaji, yaani kukifanya kinachorejelewa kuwa na uthabiti fulani. Majukumu haya matatu yanaweza kuhusishwa na lengo kuu la kuzua lugha au usemi wenye uwezo wa kushawishi (Wamitila, 2008).

Mbinu zote za kitamathali zina mchango mkubwa katika kuifanya kazi ivutie, iwe na msisitizo na mnato mkubwa. Huvutia nadhari ya hadhira na kuziathiri hisia zao. Hivyo

basi, tamathali za usemi ni mojawapo ya vigezo vya kupimia ubunifu na umbuji katika kazi fulani. Mifano ya tamathali za usemi ni misemo, sitiari, tashbihi, balagha, kwelikinzani (paradoksi), tashihisi, taswira, kinaya na nyinginezo. Mbinu hizi zina uamili wake katika uwasilishaji wa dhamira ya kifasihi.

### 4.3 Misemo/Nahau

Nahau ni aina ya semi ambazo zina maana fiche, maana ya kijuujuu ya maneno yanayounda nahau hizo huwa haina uhusiano na maana iliyokusudiwa nahau yenyewe. Wamitila (2008) anafafanua kuwa, uchanganuzi wa nahau hautegemei maana maalum za maneno yaliyomo kwenye kifungu kinachounga nahau hizo bali maana zinazoeleweka na watumiaji kutokana na kujifunza kwao au uzoefu wao. Mwandishi wa tahariri ametumia nahau kupitisha ujumbe wake. Yafuatayo ni mifano na maelezo ya nahau hizo:

1. *Bila shaka matarajio ya timu hizi mbili kujiinua kurejesha mashabiki viwanjani, kuimarisha msisimko mbali na kuchangia kukuza soka ya kitaifa hasa Harambee Stars, sasa yamepigwa jeki. (Taifa Leo* 01/02 /2016)
2. *Pana ishara tosha kuwa mashirika mengine ya kibiashara nayo yatajitokeza ili kukomboa kabumbu yetu ambayo ilikuwa imeanza kuchungulia kaburi. (Taifa Leo* 01/02/2016)
3. *Hali ambayo bila shaka itawatia shime wadau wengine wa mchezo huu. (Taifa Leo* 01/02/2016)
4. Na *inasemekana waliitisha pesa peupe mchana bila kujali kama ufisadi ni uhalifu. Taifa Leo*(25/01/2016)
5. *NPSC imekuwa ikichunguza maafisa wa ngazi za juu katika idara ya polisi.*(*Taifa Leo* 10/02 /2016)
6. *Wengi walitarajia kuwa halmashauri hiyo ingekaza kamba na kulainisha sekta ya uchukuzi wa umma ambayo imekuwa kama uwanja wa mapigano kwa miaka mingi kwa kukosa sheria*. (*Taifa Leo* 26/01/2016)
7. *Jambo hili limetia doa EACC ambayo imelazimishwa kuchunguza upya madai dhidi ya waziri huyo wa zamani. (Taifa Leo* 19/02/2016)

8. *Mashirika kama Safaricom . . . zinaombwa <u>zijitoe mhanga</u> kuchangia katika makuzi ya kandanda nchini. (Taifa Leo* 30 /01/2016)
9. *Ni bayana kuwa bila Gor na Leopards, basi soka ya Kenya imekufa. Kwa hivyo ni hatua yenye umuhimu kwa mashirika hayo kusaidia kunusuru kandanda yetu isije ikafa na kufukiwa kwenye <u>kaburi la sahau</u> kama ishara zilivyokuwa zimeanza kuonyesha. (Taifa Leo* 30/01/2016)
10. *Tunaunga wito wa tume hiyo (IEBC) na kuomba wanasiasa, serikali na wakenya kuwa <u>mstari wa mbele</u> ili kuhakikisha uchaguzi mkuu ujao utakuwa bora zaidi, wa kuaminiwa, haki na huru. (Taifa Leo* 15/01/2016)
11. *Tumeshuhudia safari za ng'ambo ambazo hazina umuhimu wowote, kwa kiwango ambacho hata baadhi ya mataifa ya kigeni mengine <u>yakapiga marufuku</u> madiwani kuzuru nchi hizo. (Taifa Leo* 12/02/2016)
12. *Changamoto iliyopo sasa ni kuhakikisha kuwa pesa zitakazookolewa kutokana na hatua hiyo, <u>hazitaishia mifukoni mwa watu</u> binafsi. (Taifa Leo* 12/02/2016)
13. *Kilimo kwa miaka mingi kimechukuliwa kuwa <u>uti wa mgongo</u> wa nchi yetu*. (*Taifa Leo* 16/02/2016)
14. *Watu ambao wamekuwa wakinunua kwa niaba ya wanunuzi halisi wamekuwa <u>donda ndugu</u> na chanzo cha kufilisika kwa wakulima kote nchini.* (*Taifa Leo* 16/02/2016)
15. *Awali wabunge hao walijaribu kila mbinu kurefusha muda wabunge la sasa ili angalau wafikishe Disemba, lakini jaribio lao <u>likagonga mwamba</u>*. (*Taifa Leo* 22/02/2016)
16. *Inafaa polisi <u>wawe macho</u> katika kipindi hiki chote ili kiongozi yeyote na wafuasi wao watakaochochea wananchi au kuzua aina yoyote ya mtafaruku wachukuliwe hatua za haraka za kisheria.* (*Taifa Leo* 07/01/2016)
17. *Hali hii pia <u>itawapa maafisa wa polisi motisha</u> ya kufanya kazi. (Taifa Leo* 03/03/2016)
18. *Idara ya polisi inafaa <u>kupiga msasa</u> mbinu zake za kutoa ulinzi kwa naibu wa rais*. (*Taifa Leo* 24/02/2016)

Msemo uliotumkia katika mfano wa 1, *kupiga jeki,* ina maanaya kuinua kwa kutumia kifaa cha kuinulia vitu vizito. Timu za AFC Leopards na Gor Mahia zimeinuliwa kifedha kwa kupewa ufadhili na shirika la kibahati nasibu michezoni la Betway na Sportpesa mtawalia. Inatarajiwa kuwa timu hizi zitafanya vyema katika mashindano yajayo kwa sababu ya msaada waliopewa.

Katika mfano wa 2, hali ya kabumbu nchini Kenya, kulingana na mwandishi huyu ilikuwa imefikia kiwango kibaya ambapo ilikuwa vigumu kuiauni. Mwandishi anapotumia msemo huu wa *kuchungulia kaburini*, msomaji anapata picha halisi ya hali ya kabumbu nchini, kwamba inahitaji msaada wa dharura ili kuweza kuiokoa.

Mwandishi ametumia msemo *tia shime* katika mfano wa 3. Anaeleza kuwa, udhamini wa shirika la kibahati nasibu michezoni la Betway kwa timu ya kandanda ya AFC Leopards utawahimiza wadau wengine kuja kuimarisha timu za soka za hapa nchini.

Msemo *peupe mchana* katika mfano wa 4 unarejelea wakati ambapo maafisa wa polisi waliitisha hongo mchana hadharani bila kuficha. Aghalabu, wanaoitisha na kutoa hongo hufanya hivyo faraghani ili macho ya wengi yasiwanase. Maafisa wa polisi wanaorejelewa katika tahariri hii walitekeleza kitendo hicho hadharani bila kuogopa kuonekana. Hii inaonyesha jinsi ufisadi umekithiri hasa katika idara ya polisi.

Katika mfano wa 5, maafisa wa *ngazi za juu* ni wale wenye vyeo vikubwa. Maafisa wa Tume ya Kitaifa ya Huduma kwa Polisi wamekuwa wakiwafanyia uchunguzi maafisa wa polisi wenye vyeo ili kuchunguza maadili yao.

Msemo *kaza kamba* katika mfano wa 6, unamaanisha kuwa Halmashauri ya Kitaifa na Usafiri (NTSA) inatarajiwa kuhakikisha kuwa sheria zinazohusu usafiri zinafuatwa kikamilifu. Halmashauri hii ilitarajiwa kuwachukulia hatua kali wahudumu wa Matatu wasiofuata sheria za barabarani na kuleta magari mabovu yanayosababisha kelele na kuchafua mazingira.

Mwandishi ametumia msemo mwingine, *limetia doa* katika mfano wa 7. Tume ya Maadili na Kukabiliana na Ufisadi [EACC] ilikuwa imefanya uchunguzi kuhusu sakata ya ufisadi katika shirika la Huduma ya Vijana kwa Taifa [NYS] na kutangaza kuwa Waziri Ann Waiguru hakuwa na hatia. Madai mapya dhidi ya Waiguru yanatia dosari tume ya EACC kwa kuwa kuna dai jingine jipya ambalo halikuwa limechunguzwa awali hata ingawa Ann Waiguru alikuwa ametangazwa kuwa hakuwa na hatia.

Msemo *kujitoa mhanga* umetumiwa katika mfano wa 8, kwa maana ya kutoa usaidizi kwa hiari. Mashirika yaliyo na uwezo wa kutoa ufadhili kwa timu za kandanda za humu

nchini yanahimizwa yatoe msaada unaohitajika bila kuchoka, bila vikwazo, tena kikamilifu, kwa udhamini huo.

Kufukiwa kwenye *kaburi la sahau* ni kusahaulika kabisa. Msemo huu umetumiwa katika mfano wa 9 kurejelia timu za soka humu nchini. Timu za Gor Mahia na AFC Leopards ni timu za kutegemewa nchini Kenya. Timu hizi zilikuwa zimeonyesha dalili za kushindwa kujiendeleza kwa sababu ya kukosa udhamini. Hali hii ingeendelea, mwandishi anahofia kuwa zingeshindwa na ingekuwa vigumu kuziokoa na kuzifufua.

Mwandishi pia ametumia msemo *kuwa mstari wa mbele* katika mfano wa 10, anapoeleza kuhusu matayarisho ya IEBC kwa uchaguzi mkuu ujao. Katika mfano wa 10, anahimiza Wakenya washiriki katika maandalizi hayo kwa kujiandikisha mapema wala wasingojee dakika ya mwisho.

Mwandishi ametumia msemo mwingine katika mfano wa 11, *piga marufuku*. Msemo huu umetumiwa na mwandishi anapoeleza kuhusu ziara za madiwani za kuzuru nchi za ng’ambo; madiwani wamenyimwa kibali cha kuzuru nchi za ng’ambo. Anaarifu kwamba safari hizo zimekuwa nyingi ilhali hazina manufaa kwa wananchi wa Kenya.

Kauli ya kuwa *pesa hazitaishia mifukoni mwa watu binafsi* ni msemo katika mfano wa 12. Ina maana kwamba, viongozi hawatachukua pesa hizo na kujibinafsishia, kwani ni pesa za umma ambazo zapaswa kutumiwa kwa miradi ya maendeleo itakayowafaidi wananchi. Pesa anazozungumzia mwandishi ni zile zitakazookolewa baada ya ziara za madiwani na viongozi wakuu wengine serikalini kusitishwa.

Mwandishi ametumia msemo maarufu unaohusu kilimo, *uti wa mgongo* katika mfano wa 13. Msemo huu umetumiwa kwa maana ya kuwa kilimo katika nchi ya Kenya ni tegemeo muhumu. Bila kilimo kutakuwa na njaa, ukosefu wa ajira na matatizo mengine. Asilimia kubwa ya Wakenya wanategemea kilimo moja kwa moja.

Msemo mwingine *donda ndugu* umetumiwa kueleza hali inayosikitisha katika sekta ya kilimo. Katika mfano wa 14, wanunuzi wanaowapunja wakulima wamekuwapo kwa muda mrefu na kusababisha wakulima kuwa maskini, ndipo mwandishi anafananisha na donda ambalo limekataa kupona. Wamekuwa tatizo kubwa kwa maendeleo na ufanisi wa wakulima.

Wabunge hawakufaulu katika mipango yao ya kutaka kurefusha muda bungeni. Katika jaribio hilo, waliafikiana kuunga mkono pendekezo la mmoja wao kwamba walipwe mshahara wa miezi ambapo hawatakuwa kazini, ndipo jaribio lao *likagonga mwamba*. Mwandishi ametumia msemo huo katika mfano wa 15, kwa maana ya kutofaulu.

Msemo mwingine *wawe macho,* una maana kuwa polisi wanahitajika wawe waangalifu ili waweze kunasa wanasiasa wanaochochea wananchi. Mwandishi ametumia msemo huu katika mfano wa 16 anapoeleza visa vya wanasiasa wanaotumia lugha ya uchochezi.

Mwandishi wa tahariri katika mfano wa 17, anaelezea hali ya makazi ya maafisa wa polisi. Maafisa wakijengewa makao ya kuishi, wataweza kufanya kazi yao vizuri. Kulingana na mwandishi wa tahariri hii, maafisa wakiwa na mahali pazuri pa kuishi, watakuwa na azma ya kufanya kazi yao vizuri, kwa sababu itakuwa *imewatia motisha.*

Katika mfano wa 18, msemo *piga msasa* umetumiwa kwa maana ya kurekebisha na kulainisha. Msasa ni kifaa kinachotumiwa na seremala kwa kulainisha fanicha anazotengeneza. Idara ya polisi inashauriwa kunyoosha na kurekebisha mahali ambapo dosari imeonekana. Idara hii imeonyesha kupuuza ulinzi wa viongozi wakuu serikalini hasa wanapotembea kule mashinani. Rubani wa Naibu wa Rais William Ruto alighadhabishwa na afisa wa kike aliyekuwa akichezea simu badala ya kuimarisha ulinzi uwanjani.

## 4.4 Sitiari

Wamitila (2008) anaeleza kwamba sitiari ni tamathali ya usemi ya ulinganishi usiotumia vilinganishi 'kama', 'mithili ya', 'mfano wa' n.k. Msingi wa sitiari ni uhamishi wa maana. Wamitila anatoa mfano wa sitiari, 'Ujana ni moshi,' kuna uhamishi wa maana ambapo ujana unapewa sifa za moshi. Tamathali hii ya usemi imetumiwa kwa upana katika tahariri ya gazeti la *Taifa Leo*, kama mifano ifuatayo inavyoonyesha:

*1.Bunge linavyorejelea vikao vyake leo, Wakenya wengi wanasubiri kujua jinsi watakavyoendesha shughuli zao, wakiwa wameghubikwa na* <u>*wingu la madai*</u> *ya ufisadi.(Taifa Leo* 09/02/2016)

*2. <u>Chini ya mwavuli</u> wa muungano wa mashirika ya umma (NCSC), viongozi wa mashirika haya walitoa makataa ya wiki mbili kwa tume ya maadili na kupambana na ufisadi (EACC), itoe ripoti yake ya uchunguzi kuhusu wabunge fisadi, la sivyo waelekee kortini kushinikiza kutolewa kwa ripoti. (Taifa Leo* 09/02/2016)

*3. <u>Ufisadi ni zimwi</u> ambalo kuzimwa kwake kunahitaji zaidi ya sheria kali. (Taifa Leo* 25/03/2016)

*4. <u>Ndoto ya wananchi</u> kuhusu kuletewa maendeleo karibu nao yafaa ianze kuonyesha dalili za kutimia. (Taifa Leo* 12/02/2016)

*5.Ujuzi wake kama mkufunzi wa Harambee Stars wa under-23 na klabu ya Mathare United huenda usitoshe kujenga timu yenye uwezo wa <u>kutetemesha mahasimu</u> kwenye mashindano ya kimataifa. (Taifa Leo* 27/02/2016)

*6. Ni <u>maradhi</u> ambayo tayari yamesambaa katika <u>damu</u> ya Wakenya pamoja na viongozi wao na <u>tiba</u> yake yahitaji tathmini ya vigezo vikuu vya kijamii. (Taifa Leo* 25/03/2016)

*7. Kwa jumla mswada huo wa rushwa 2015 una dhamira nzuri ya kuhakikisha ufisadi umezimwa nchini lakini utekelezaji wake huenda ukasalia <u>kitendawili kikubwa</u>.* (*Taifa Leo* 25/03/2016)

*8. Wahudumu wa teksi jijini Nairobi wanafaa kukubali tuko katika enzi za teknolojia na waanze <u>kukumbatia teknolojia</u> za kisasa kuendeleza biashara zao.* (*Taifa Leo* 05/02/2016)

*9. Wanasiasa hao <u>wanapanda hisia za chuki</u> miongoni mwa Wakenya.* (*Taifa Leo* 07/01/2016)

*10. Tutatumai kuwa safari hii Wakenya watatumia <u>silaha</u> muhimu ya kura, kuzuia <u>ulafi</u> huu ambao <u>umekita mipaka.</u>(Taifa Leo* 22/02/2016)

*11. Ni kinaya kwamba tutaendelea kushuhudia matamshi kama haya tukiwa bado hatujaponya <u>vidonda</u> vinavyotokana na athari za chuki za kikabila.* (*Taifa Leo* 07/01/2016)

*12. <u>Tiba</u> ni viongozi kuchukuliwa hatua kali za kisheria. (Taifa Leo* 07/01/2016)

13. Y*eye (Salah) ni* *<u>kafara</u>* *wa ujumbe wa ukweli. (Taifa Leo*19/01/2016)

*14. Kuzinduliwa kwa usajili huo unaashiria kuanza kwa* *<u>safari</u>* *ya kuelekea kwenye uchaguzi mkuu wa 2017. (Taifa Leo* 15/02/2016)

Katika mfano wa 1, madai ya ufisadi yanayolikabili bunge yanalinganishwa na wingu Kwa kawaida, wingu linapotanda angani linaweza kuzuia miale ya jua isifike ardhini. Vilevile, ufisadi unaweza kukinga na kuzuia maendeleo ya aina yoyote yasimfikie mwananchi.

Mwandishi anatumia sitiari ya mwavuli, katika mfano wa 2. Muungano wa mashirika ya umma unalinganishwa na *mwavuli* kwa sababu chini yake muungano huu kuna mashirika mengi.

Katika mfano wa 3 ufisadi umekithiri nchini Kenya kiasi cha kulinganishwa na *zimwi* ambalo si rahisi kuzimwa. Sitiari hii inawafungua watu macho ili wajue kwamba ufisadi unatisha kama zimwi na kwamba ufisadi si tatizo la kupuuzwa bali lahitaji mikakati kabambe ili kuweza kukabiliana nalo.

Katika mfano wa 4, sitiari imetumiwa na mhariri anapolinganisha *ndoto* na matarajio na matamanio ya wananchi. Mwananchi wa kawaida hana uwezo wa kutekeleza na kusababisha maendeleo katika maeneo yao; walio na uwezo ni viongozi mamlakani, ndio maana inasalia kuwa ndoto tu kwa mwananchi.

*Kutetemesha mahasimu* katika mfano wa 5, ni kushinda timu zingine pinzani zinazomenyana na AFC Leopards. Ujuzi wa kocha Stanley Okumbi kuweza kuandaa timu itakayoshinda timu pinzani unatiliwa shaka na mwandishi.

Mwandishi ametumia sitiari ya *maradhi* katika mfano wa 6 ili kuonyesha jinsi ufisadi ulivyo hatari kwa taifa. Ufisadi umeingia na kuathiri imani ya wananchi kama sehemu ya maisha yao, kuondoa ufisadi kunahitaji juhudi kubwa kutoka jamii nzima.

Sitiari ya kitendawili imetumiwa katika mfano wa 7. *Kitendawili* ni fumbo linaloficha maana na ambalo huhitaji kufikiria ili kukitegua. Utekelezaji wa mswada wa rushwa, kulingana na mwandishi, hautakuwa jambo rahisi unahitaji muda na bidii kwa wanaohusika.

Katika mfano wa 8, sitiari ya kukumbatia inachora picha akilini mwa msomaji. Wahudumu wa teksi wanafaa kukaribisha na kukubali kutumia teknolojia ya kisasa katika biashara ya teksi. Mwandishi anatetea kwamba maisha ya kisasa yanategemea sana teknolojia.

Katika mfano wa 9, hisia za chuki zinaenezwa na wanasiasa kupitia matamshi yao ya uchochezi. Mwandishi anaposema kuwa wanasiasa wanapanda hisia za chuki, ina maana kuwa hisia hizo zina uwezo wa kumea na kusambaa, matokeo yake yataonekana baadaye kupitia kwa matendo ya wakenya. Ghasia na migogoro baina ya jamii mbalimbali huwa tokeo la uchochezi wa wanasiasa.

Katika mfano wa 10, mwandishi anatumia sitiari ya *silaha* ambayo wananchi wanapaswa kutumia kuwakabili viongozi waliojawa na tamaa. Kwa kupiga kura na kuondoa viongozi hao wenye tamaa ya kupundukia na kuchagua wengine wapya.

Katika mfano wa 11, *vidonda* ni matokeo ya vita vya kikabila vya baada ya uchaguzi mwaka wa 2007. Watu wengi waliuawa, mali iliharibiwa na wengi kuachwa bila makao. Hadi wa sasa, kuna wakimbizi ambao bado hawajapewa makazi japo waliahidiwa kupewa fidia na serikali miaka mingi iliyopita.

Katika mfano wa 12, neno *tiba* linaashiria suluhisho kwa tatizo la ufisadi. Mwandishi anapendekeza kuwa hatua kali za kisheria zichukuliwe dhidi ya viongozi fisadi.

Kafara katika mfano wa 13, Salah anahusishwa na sadaka ambayo hutolewa ili kutuliza hasira za miungu. Mwandishi anamfananisha Bw Salah na kafara aliyejitolea ili wengine waishi. Salah alijitolea kuokoa abiria kwenye shambulizi la basi huko Mandera mwezi wa Disemba, 2015.

Sitiari nyingine imetumiwa katika mfano wa 14, ambapo zoezi la usajili wa wapiga kura unachukuliwa kama *safari* ambayo imeanza na inatarajiwa kuendelea hatua kwa hatua na ifikie tamati wakati wa kupiga kura mwaka wa 2017.

## 4.5 Tashbihi

Tashbihi ni tamathali ya usemi ambapo vitu viwili hulinganishwa kwa njia ya moja kwa moja. Ulinganishaji huu hutambulishwa na matumizi ya vilinganishi: 'kama', 'mfano wa', 'mithili ya', 'ja', 'kama vile', 'sawa', 'tamthili ya', 'kulingana na', 'fanana na' n.k. Tamathali hii hutumiwa sana katika kazi za kifasihi na huwa na mchango mkubwa katika kuyawasilisha maudhui na mawazo ya mwandishi (Wamitila, 2003). Dhamira moja ya ulinganishi huu ni kusisitiza sifa na kutujengea picha ya aina fulani akilini. Ifuatayo ni mifano ya tashbihi zilizotumiwa katika tahariri ya *Taifa Leo:*

*1. Imefichuka ulaghai huo huchukuliwa <u>kama</u> biashara yenye faida ya mamilioni ya pesa na baadhi ya wananchi. (Taifa Leo* 30/03/2016)

*2. Spika Muturi anapaswa kuonyesha uwajibikaji kuhusu suala hili <u>jinsi</u> Uhuru Kenyatta na jaji mkuu Willy Mutunga walivyofanya kwa maafisa katika idara wanazosimamia moja kwa moja. (Taifa Leo 09/02/2016)*

*3. EACC haifai kuonekana <u>kama</u> jibwa linalobweka bila kung'ata.* (*Taifa Leo* 19/02/2016)

*4. Ikiwa hilo halifanyiki kuna hatari ya nchi kukumbwa na mkosi <u>kama</u> wa 2007.(Taifa Leo* 07/01/2016)

*5. Ingawa tunaomboleza (Bw Salah Farah) <u>kama</u> balozi wa amani, daima tutakumbuka kujitolea kwake.*(*Taifa Leo* 19/01/2016)

*6. Wengi walitarajia kuwa halmashauri hiyo ingekaza kamba na kulainisha sekta ya uchukuzi wa umma ambayo imekuwa <u>kama uwanja wa mapigano</u> kwa miaka mingi kwa kukosa sheria. (Taifa Leo* 26/01/2016)

*7. Matamshi <u>kama</u> hayo ndiyo yalipelekea kutokea kwa ghasia za baada ya uchaguzi tata wa 2007*. (*Taifa Leo* 07/01/2016)

*8. Sharti serikali itoe mikakati na mwongozo wa uchimbaji madini na mafuta kabla ya matapeli wa ughaibuni hawajaibuka na kugeuza Kenya kuwa <u>kama</u> mataifa ya Kiarabu*. (*Taifa Leo* 18/03/2016)

*9. Leopards kwa upande mwingine ikikamilisha ligi kuu ya mwaka jana ikijikokota kama rukwama hasa baada ya mdhamini wake Mumas Sugar kujipata katika mtanziko mkuu wa kifedha.*(*Taifa Leo* 30/01/2016)

Tashbihi imetumiwa katika mfano wa 1 kuelezea tatizo sugu la wizi wa Mtihani wa Kitaifa wa Shule za Upili (KCSE) ulivyozidi kwa miaka ya hivi karibuni, hasa mwaka jana wa 2015. Mwandishi kwa kutumia tashbihi 'kama', analinganisha wizi wa mtihani na biashara yenye mamilioni ya pesa kwa sababu waliohusika na ulaghai huo walipata pesa nyingi sana.

Katika mfano wa 2, mwandishi analinganisha hali inayomkabili Spika Muturi na hali zilizowakabili Uhuru Kenyatta na Willy Mutunga kwa kutumia kilinganishi 'jinsi'. Spika Muturi basi, anapaswa kuwajibika na kuchukua hatua kama vile Uhuru Kenyatta na Willy Mutunga walivyofanya.

Katika mfano wa 3, mwandishi analinganisha EACC na jibwa linalobweka bila kung'ata kwa kutumia kilinganishi 'kama' ili kuonyesha jinsi lisivyo na uwezo wa kuchukua hatua yoyote kwa washukiwa wa ufisadi. Hii ni kwa sababu viongozi na maafisa wa umma waliotajwa kushiriki ufisadi hawajachukuliwa hatua yoyote.

Katika mfano wa 4, mwandishi ametumia tashbihi 'kama' kuwatahadharisha Wakenya wasijiingize kwa mkosi. Mwandishi anatumia ulinganisho wa hali mbili. Wakenya wengi bado wanakumbuka yaliyotendeka mwaka wa 2007, mwandishi anatumia ulinganisho huo ili kutahadharisha dhidi ya kuelekeza nchi kwa mkosi 'kama' wa 2007.

Mfano wa 5, Bwana Salah anafananishwa na balozi, kwa kutumia tashbihi 'kama', balozi ni mwakilishi wa kisiasa wa nchi moja katika nchi nyingine. Kitendo cha Salah kuwaokoa abiria Wakristo katika shambulio dhidi ya basi moja mwezi wa Disemba 2015 katika eneo la Mandera, ni kitendo cha ushujaa.

Katika mfano wa 6 hapo juu, mwandishi anaeleza hali ya sekta ya usafiri nchini na kulinganisha na uwanja wa mapigano. Kulingana na mwandishi hali hii imetokea kwa sababu NTSA, haijaweka msimamo mkali katika sekta ya matatu. Kwa hivyo sekta ya matatu ni *kama* uwanja wa mapigano.

Mfano wa 7 inaonyesha ulinganisho kwa matumizi ya kilinganishi *kama*; matamshi ya uchochezi wa wanasiasa wa wakati huu yanalinganishwa na matamshi ya uchochezi yaliyoshuhudiwa kabla ya uchaguzi wa 2007. Matamshi hayo yalisababisha uhasama wa kikabila, ukazua ghasia za baada ya uchaguzi.

Katika mfano wa 8, mwandishi analinganisha Kenya na mataifa ya Kiarabu, anaeleza kuwa Mataifa ya Kiarabu yana utajiri mkubwa wa mafuta lakini wenyeji wanataabika kwa sababu ya mizozo. Serikali hivyo basi inatahadharishwa mapema isije ikawa *kama* mataifa ya Kiarabu bali iweze kuepuka mizozo inayoweza kusababishwa na mafuta miaka ijayo.

Matumizi ya tashbihi 'kama' katika mfano wa 9, inajenga taswira ya hali ilivyokuwa imefikia kwa timu ya Leopards, kwamba mambo hayakuwa yakisonga vile ilivyohitajika kwa sababu ya ukosefu wa fedha. Mwendo wa rukwama ni wa polepole sana kwani inategemea kusukumwa. Hii inamaanisha kuwa shughuli za timu hiyo zilikuwa zimekwama.

### 4.6 Maswali ya balagha

Hii ni tamathali ya kuuliza maswali ambayo hayahitaji majibu. Wamitila (2008) anaelezea kuwa maswali ya balagha ni mbinu ya matumizi ya maswali ambayo hayahitaji majibu kwa vile majibu yake yako wazi na yanachochea fikra au hisia kwa upande wa msomaji au msikilizaji. Huwa ni mbinu nzuri ya kumfikirisha msomaji, kumshawishi kuhusu jambo au hali fulani; na pia kusisitiza usemi. Mhariri wa *Taifa Leo* ametumia maswali ya balagha yafuatayo:

*Kwani Kenya ina utajiri kiasi gani, hata iwalipe mshahara zaidi ya watu 1,500 kwa miezi minane wakiwa hawafanyi kazi yoyote ya kuwatumikia wananchi?(Taifa Leo* 22/02/2016)

Katika mfano huu mwandishi wa tahariri ya *Taifa Leo* anaeleza mipango ya wabunge wa Taifa la Kenya, wanaotaka walipwe mshahara kwa miezi minane baada ya muda wao kukamilika. Swali hili linasaili kiwango cha utajiri wa taifa la Kenya, na iwapo itaweza mzigo wa kuwalipa watu wasiofanya kazi. Swali hili litamkumbusha msomaji na hasa Mkenya wa kawaida, afikirie kuhusu shida ambazo wananchi wa kawaida

hupitia zikiwemo ukosefu wa ajira na umaskini. Na kwa hakika, Kenya haina utajiri wowote. Mwandishi anaendelea kumchochea msomaji kwa maswali zaidi;

*Sasa inakuaje wabunge wanaidhinisha walipwe mshahara kwa miezi minane ambapo Wakenya watakuwa wameshaamua kuwa mkataba wao umemalizika?(Taifa Leo* 22/02/2016)

Mbali na mishahara ya wabunge, mbinu hii pia imetumika kuhoji swala kuhusu madiwani ambao wanapinga mswada unaolenga kuinua kiwango chao cha elimu. Mhariri anauliza;

*Ni mfano gani wanaotaka kuwaonyesha vijana? Kwamba unaweza kufanikiwa bila ya masomo ya maana? (Taifa Leo* 27/01/2016)

Maswali haya yanalenga kumfikirisha msomaji, iwapo elimu itakuwa na manufaa tena ilhali viongozi hawaoni umuhimu wake. Msomaji anapoyatafutia majibu maswali hayo, mwandishi anahitimisha kwa kueleza umuhimu wa masomo kwa madiwani.

Kwa ujumla, mwandishi wa tahariri ya *Taifa Leo* anatumia maswali hayo ya balagha kuwasilisha maswala mazito. Maswali haya pia humwacha msomaji akifikiria kuhusu mambo yaliyotajwa na mwandishi.

### 4.7 Kweli kinzani

Wamitila (2008) anasema kwamba tamathali hii hutumiwa kurejelea kauli ambayo inaonekana kujipinga kijuujuu ingawa inapochunguzwa kwa makini inaonyesha ukweli fulani. Ni kauli iliyo na ukweli wenye ukinzani. Wamitila anaongeza kuwa, dhima kuu ya kwelikinzani ni kumshtukiza msomaji na kumfanya atafakari kuhusu kauli au elementi zinazoleta ukinzani katika kauli inayohusika.

Mwandishi wa tahariri ya *Taifa Leo* ametumia mbinu hii ya kweli kinzani, na kudhihirishwa na mifano ifuatayo:

*Wito wetu ni kuwa hatua ichukuliwe kuepusha ghasia kwa sababu hali kama hiyo inaweza kutikiza* <u>*uthabiti telezi*</u> *tunaofurahia nchini kwa sasa*. (*Taifa Leo* 24/03/2016)

Ukinzani wa maneno unadhihirika kwa matumizi ya maneno ‘uthabiti’ inayomaanisha iliyo imara na ‘telezi’ inayomaanisha isiyo imara. Hali hii inarejelea taharuki iliyoshuhudiwa nchini Kenya kutokana na ghasia za baada ya uchaguzi wa 2007. Hali sasa ni thabiti kwani tunashuhudia amani nchini, lakini ni telezi kwa sababu inaweza kubadilika wakati wowote kutegemea matamshi na uchochezi wa wanasiasa. Iwapo wanasiasa wataeneza uchochezi kwa wananchi walio na amani, hali itabadilika haraka sana na kuwa ya vita.

*Ukweli mchungu ni kuwa kwa sasa Kenya haina chakula cha kutosha kulisha raia wake (Taifa Leo* 27/03/2016)

Ni matarajio ya kila Mkenya kuwa Kenya ina uwezo wa kulisha raia wake. Ukweli unaobainika ni kuwa Kenya haina uwezo huo, ukweli huu unasababisha uchungu ikizingatiwa kuwa kuna ardhi na raslimali ya kutosha kuzalisha chakula kinachotosha kulisha taifa zima na hata kingine kuuzwa kwa mataifa jirani. Mfano mwingine wa kweli kinzani ni:

*Ukweli mchungu ni kuwa raia wa kawaida ndio wanapata hasara kubwa kutokana na ufisadi baada ya kukosa huduma muhimu kutoka kwa serikali.(Taifa Leo* 25/03/2016)

Ukinzani unatokea katika matumizi ya maneno ukweli na mchungu, kwa kawaida huwa tunatarajia ukweli uweze kuleta afueni na kuokoa hali ambazo zilikuwa zimekandamizwa na uongo, lakini katika kauli hii, ukweli unasababisha uchungu. Maneno hayo yanapingana kijuujuu lakini kwa undani, maana na matumizi yanakubalika.

## 4.8 Tashihisi

Tashhisi ni tamathali ya usemi ambapo vitu visivyokuwa na uhai ama vyenye sifa za kidhahania vinapewa sifa za binadamu. Katika hali hii, kitu kisicho binadamu, iwe ni mnyama au mdudu hupewa sifa ya binadamu. Hii ni kwa kuwa maana ya tashihisi ni kunafsisha au kufanya kitu kuwa na maumbile au mahasa kama vile nafsi ya mtu (Kuhenga, 1977:15). Mwandishi wa tahariri ya *Taifa Leo* ametumia mbinu ya tashihisi kwa mifano ifuatayo:

*Baada ya AFC Leopards kutapatapa sana msimu uliopita bila udhamini, pana haja ya jitihada zote kufanywa ili kuhakikisha kuwa ufadhili <u>unaobisha mlangoni</u> pa klabu hiyo hautelezi kamwe.( Taifa Leo* 01/02/2016)

Kulingana na mwandishi wa tahariri hii, ufadhili unabisha mlangoni pa klabu ya AFC Leopards. Ufadhili umepewa uwezo wa kibinadamu wa kubisha mlango. Iwapo ufadhili huu hautachukuliwa kwa wakati unaofaa unaweza kupotea. Inawahimiza wasimamizi wa timu hii kuwa waangalifu wasije wakapoteza udhamini huo.

Mfano mwingine wa tashihisi katika tahariri ya *Taifa leo* ni:

*Yakini huu ni mwanzo wa mambo mema <u>yanayosubiri</u> soka yetu. (Taifa Leo 01/02/2016)*

Mambo mema yamepewa uwezo wa kibinadamu wa kusubiri. Mwandishi anaeleza kuwa mashirika mengine ya kibiashara yatajitokeza ili kuokoa kabumbu ya humu nchini.

## 4.9 Taswira

Taswira ni matumizi ya lugha kwa namna inayojenga picha ya hali au jambo fulani kwa msomaji. Picha hizi hujengwa akilini mwa msomaji kwa maelezo fulani na huweza pia kujengwa kwa matumizi ya tamathali za usemi kama tashbihi na sitiari. Lengo la kutumia taswira ni kumfanya msomaji aelewe vile mtu au kitu kinavyoonekana na pia kutoa msisitizo fulani. Mwandishi wa tahariri ya *Taifa Leo* ametuchorea picha kwa maelezo yafuatayo;

*Wakulima humu nchini wamekuwa <u>wakimenyeka juani</u>, huku wahuni wachache <u>wakifurahia jasho lao kivulini</u>. (Taifa Leo 16/02/2016)*

Maelezo haya ya mwandishi kuhusu wakulima yanajenga picha akilini mwa msomaji. Tunaona picha ya wakulima wakiwa shambani huku jua kali likiwaunguza ilhali hawatafurahia matunda ya jasho lao, badala yake watu wengine watakuja kufaidika kutokana na jasho lao. Wale wanaofurahia wanaweza kuwa ni wafanyi biashara

wanaowapunja wakulima kwa kununua mazao kwa bei ya chini na kwenda kuuza kwa bei ya juu.

Mwandishi ametuchorea picha nyingine kwa mfano ufuatao:

*Wananchi wamechoshwa na jinsi wanavyozungushwa kwenye mviringo wa madai ya ufisadi kila mara bila kuona mtu yeyote akiadhibiwa kisheria. (Taifa Leo 19/02/2016)*

Ufisadi umekuwa neno la kawaida kusikika kila uchao katika vyombo vya habari humu nchini. Madai mapya ya ufisadi unaotaja shirika la huduma kwa Vijana kwa Taifa (NYS) yametoa picha mbaya. Awali EACC ilikuwa imewaachilia maafisa wa tume hiyo huku ikisema kwamba hawakupatikana na hatia. Tume ya Maadili ya Kukabiliana na Ufisadi inawazungusha Wakenya kwenye mviringo ambao hauna mwisho, uchunguzi unafanywa bila kuona matokeo yake wala hatuoni hatua za kisheria zikichukuliwa dhidi ya wakosaji. Kwa hakika ni kama Wakenya wanazungushwa kwenye mviringo. Mbali na hayo, kunayo taswira nyingine ya sekta ya matatu kama inavyoelezwa kwenye mfano ufuatao:

*Wengi walitarajia kuwa halmashauri hiyo ingekaza kamba na kulainisha sekta ya uchukuzi wa umma ambayo imekuwa kama uwanja wa mapigano kwa miaka mingi kwa kukosa sheria. (Taifa Leo* 26/01/2016)

Mwandishi anatueleza namna sekta ya uchukuzi imekuwa kama uwanja wa mapigano. Kwenye uwanja huu, kuna magari ambayo husababisha kelele na kuharibu mazingira ya jiji kwa sababu ya eksozi zilizoharibika. Picha ya magari yaliyo na michoro ya kuogofya, uendeshaji magari kwa kasi na ukosefu wa nidhamu barabarani, inakamilisha taswira ya uwanja wa mapigano.

## 4.10 Kinaya

Kinaya hujengwa kwenye msigano au mgongano fulani kati ya hali halisi na matarajio ya wanaohusika (Wamitila , 2008). Mwandishi wa tahariri ya *Taifa leo* ameonyesha hali za kinaya kwenye masuala anuai aliyozungumzia. Yafuatayo ni baadhi ya mifano:

*Waziri alisema ni jambo la kuhuzunisha kwamba wakulima ambao ndio wanaomenyeka zaidi katika shughuli ya kuwatafutia watu riziki, huishia kuwa hohehahe bila ya pesa*

*mfukoni. Kinyume chake, watu ambao hawajui hata jembe linavyoshikwa, ndio wanaofurahia manoti na faida kubwa. (Taifa Leo 16/02/2016)*

Katika mfano huu, ni kinyume cha matarajio yetu kuwa mkulima anateseka na kukosa pesa ilhali yeye ndiye hufanya kazi nyingi zaidi za kuwatafutia watu riziki. Mwandishi anaeleza kuwa watu wasioshughulika shambani ndio wanaostarehe na kufaidika kutokana na kazi ya mkulima. Ingehalisi kuwa, baada ya mkulima kuteseka shambani, aje afaidike na kufurahia jasho lake.

Hali nyingine ya kinaya imebainika kwenye tahariri ya *Taifa Leo* kwa mfano ufuatao:

*Ni kinaya kwamba tunaendelea kushuhudia matamshi kama haya huku tukiwa hatujapona vidonda vinavyotokana na athari za chuki za kikabila. (Taifa Leo 27/01/2016)*

Katika mfano huu, viongozi wa kisiasa wamesikika wakitoa matamshi ya uchochezi mmoja baada ya mwingine. Mwandishi amemnukuu mwanasiasa Suleiman Shahbal akisema kwamba, serikali inapanga kushinda katika Uchaguzi Mkuu wa 2017 'kwa njia zozote zile'. Wakati Shahbal akitamka maneno hayo, Naibu wa Rais William Ruto alikuwepo ila hakusema lolote. Ni matarajio yetu kuwa Naibu wa Rais angepinga madai hayo, yeye akiwa kiongozi wa mamlaka ya juu zaidi baada ya Rais. Pia, kiongozi wa upinzani Bw. Raila Odinga alidai kwamba serikali ina njama za kuiba kura katika uchaguzi mkuu ujao. Matamshi haya yanaweza kuchochea raia au wafuasi wa chama cha upinzani.

Mfano mwingine wa kinaya ni huu:

*Hata hivyo ukali wa tangazo hilo haukudhihirika, kwani ukawaida katika sekta ya uchukuzi uliendelea kudhihirika jana (Taifa Leo 26/01/2016).*

Ni kinaya kuwa NTSA linatoa tangazo kali na kukosa kifuailia. Halmashauri ya Kitaifa ya Usafiri na Uchukuzi ilitoa tangazo kwamba ingeanza msako mkali dhidi ya magari yanayokiuka sheria za trafiki. Baada ya tangazo hilo wengi walitarajia kwamba ingekaza kamba na kuhakikisha kwamba sheria inafuatwa kikamilifu. Hata hivyo, ukali wa tangazo hilo haukudhihirika, ukawaida uliozoelewa na Wakenya uliendelea. Mwandishi anatukumbusha hali kama hii na wakati wa Waziri wa Uchukuzi marehemu

John Michuki, ambaye alihakikisha kanuni zimefuatwa kikamilifu licha ya malalamishi mengi kutoka kwa wenye matatu.

Mbali na hayo, mwandishi ameonyesha hali nyingine ya kinaya anaposema;

*Hatua ya madiwani kupinga mswada unaolenga kuinua kiwango chao cha elimu ya wanaotaka wadhifa huo na ya kuvunja moyo. (Taifa Leo 27/01/2016)*

Ni kinaya kwamba madiwani wanapinga mswada unaolenga kuinua kiwango cha elimu kuwa diploma ama digrii kuanzia uchaguzi mkuu wa 2017. Madiwani wana majukumu mazito, wanapaswa kutayarisha miswada na kuyapitisha kwa manufaa ya watu wa kaunti husika. Isitoshe, wao pia ni mfano wanaoigwa na vijana kwani wanapata mshahara mzuri. Kwa hivyo katika hali halisi, tungetarajia waunge mkono mswada huo wakiwa viongozi ili wawe mifano ya kuigwa na wengi.

Hali ya kinaya inadhihirika pia katika mfano ufuatao wa tahariri ya *Taifa Leo:*

*Kinachoshangaza zaidi ni kuwa Wizara ya Elimu ilikuwa imeagiza wakurugenzi wa elimu katika kila kaunti kukabidhi chama hicho pesa za kuendeleza shughuli zake za kuwakilisha wazazi, katika mwaka wa 2013. (Taifa Leo 29/01/2016)*

Matarajio ya wananchi wa Kenya ni kuwa serikali inaweza kudhibiti shughuli za vyama na kuhakikisha kuwa vyama hivyo haviwatapeli na kuwapora wazazi. Ni kinaya kwa chama cha Kitaifa cha Wazazi (KNAP) kuendeleza shughuli zake ilhali ni shirika lisilo halali. Shirika hili likiongozwa na Bw Musau Ndunda limekuwa likiwatoza wazazi pesa mwaka wa 2013. Shirika hili limeingilia shughuli katika sekta ya elimu; sekta yenye umuhimu mkubwa kitaifa, kwa njia isiyo halali na serikali haijatambua licha ya malalamishi kutoka kwa washika dau.

Mbali na hayo mhariri wa *Taifa Leo* ameeleza yafuatayo kuhusu maafisa wa NPSC;

*Kulingana na madai hayo, maafisa wa NPSC wanaochunguza polisi wamekuwa wakipokea hongo ya kati ya sh300,000 na sh500,000 ili kuruhusu maafisa wenye maadili ya kutiliwa shaka kuendelea kuhudumu. (Taifa Leo* 10/02/2016)

Ni kinaya kwamba maafisa wa tume ambalo limepewa mamlaka ya kuchunguza maadili ya maafisa wa polisi, kudaiwa kuwa wanapokea hongo. Tume ya Kitaifa ya

Huduma kwa Polisi (NPSC), inachunguza maadili ya maafisa wa ngazi za juu katika idara ya polisi, tangu mwaka wa 2014. Hata hivyo kuna madai kuwa baadhi ya maafisa wa tume hiyo (NPSC) wamekuwa wakipokea hongo kutoka kwa maafisa wa polisi ambao maadili yao ni ya kutiliwa shaka. Hali hii inaonyesha kiwango ambacho ufisadi umewaingia wafanyakazi wa serikali nchini Kenya; maadili yao ni ya kutiliwa shaka.

Mwisho, mhariri wa *Taifa Leo* anaeleza kinaya kuhusu vitendo vya polisi Uganda;

*Kwanza, polisi walionekana wakitumia nguvu kuwahangaisha wafuasi wa Dkt Besigye, huku wakimkamata mara tatu kwa wiki moja, wakitaja hatua yao katili kama " kulinda usalama wa taifa." (Taifa Leo 21/02/2016)*

Polisi wanawahangaisha wafuasi wa Dkt Besigye, huku wakimkamata mara tatu kwa wiki, kinaya ni kwamba walitaja hatua hiyo katili kama 'kulinda usalama wa taifa.' Kwa hakika, usalama wa taifa hautadumishwa iwapo kiongozi wa upinzani atakamatwa na kutiwa kizuizini huku wapinzani wake wakihangaishwa. Kitendo cha polisi hao kingeweza kuzua mgogoro hata zaidi.

## 4.11Hitimisho

Katika sura hii, tumeshughulikia matumizi ya lugha na tamathali za usemi. Tumeangazia tamathali mbalimbali za usemi zikiwemo sitiari, nahau/misemo, tashbihi, kinaya, taswira, tashihisi, maswali ya balagha na kweli kinzani. Mtunzi amezitumia tamathali hizi ili kutoa mvuto wa kisanaa na kupitisha ujumbe wake kwa njia teule inayoeleweka. Tamathali hizi zina majukumu kadha: zimetumiwa kuibua hisia, kuhuisha, kurembesha na kufafanua maana.

Mhariri amefaulu pakubwa kutumia tamathali hizi za usemi na zimefanikisha uwasilishaji wa maudhui kwa msomaji pamoja na kuonyesha mtazamo na mwelekeo wa mhariri wa gazeti la *Taifa Leo.*

# SURA YA TANO: MUHTASARI, MATOKEO NA MAPENDEKEZO

## 5.1 Utangulizi

Sura hii ndiyo sura ya mwisho kwenye utafiti huu. Uchunguzi huu ulishughulikia mtindo na matumizi ya lugha katika tahariri ya gazeti la *Taifa Leo.* Sura hii inatoa muhtasari, matokeo ya uchunguzi na hatimaye kutoa mapendekezo ya tafiti za baadaye.

## 5.2 Muhtasari

Utafiti huu ulinuia kuchanganua mtindo katika tahariri ya gazeti la *Taifa Leo*. Katika sura ya kwanza, tumeshughulikia maswala ya kimsingi yanayojenga utafiti; tatizo la utafiti, malengo ya utafiti, sababu ya kuchagua mada, nadharia tete, upeo na mipaka, msingi wa nadharia, yaliyoandikwa kuhusu mada na njia za utafiti tulizotumia.

Katika sura ya pili, dhana ya tahariri imeshughulikiwa; aina za tahariri, sifa za tahariri muundo wa tahariri, majukumu ya tahariri na uhusiano kati ya tahariri na habari. Katika sura ya 3 tumeshughulikia mtindo wa tahariri. Nadharia tete ya kwanza ilisema kuwa mwandishi wa tahariri huteua maneno na virai kwa lengo maalum ili kuonyesha mwelekeo wa mhariri kuhusu swala linalozungumziwa. Utafiti wetu umebainisha kuwa maneno maalum yanateuliwa na mhariri ili kutoa mapendekezo, kukashifu, kuhimiza kupongeza n.k. Tahariri za kuhakiki ndizo zimeonekana kuteua maneno maalum ili kuonyesha msimamo wao kwa kupinga au kuunga mkono swala fulani. Vitenzi 'inafaa' 'inapasa' vimetumika kutoa mapendekezo kwa njia ya ulazima.

Nadharia tete ya pili ilitathmini mbinu za lugha na tamathali za usemi, ambayo imeshughulikiwa katika sura ya nne. Katika utafiti wetu, tumegundua kwamba tamathali za usemi na mbinu nyingine za lugha zimetumiwa na mwandishi wa tahariri ya *Taifa leo*. Sitiari, misemo/nahau na tashbihi ndizo tamathali zilizotawala katika tahariri ya gazeti la *Taifa leo* tulizochunguza. Sababu za kutumia sitiari na tashbihi ni kuwa inasaidia kujenga picha kwa kuhusisha kitu kimoja na kingine. Misemo mingi imetumiwa ili kupamba lugha. Tamathali zingine ni kwelikinzani, tashihisi na kinaya.

Mbinu za lugha kama maswali ya balagha na taswira zimetumiwa ili kufanikisha uelewekaji wa ujumbe.

Katika uchunguzi wetu tuligundua kuwa methali moja tu ndiyo iliyopatikana katika data tuliyochunguza. Methali hiyo ni, *kutoa ni moyo usambe ni utajiri (Taifa Leo 30/1/2016).* Mhariri hajatumia methali nyingi, labda kwa sababu methali zina maana ya ndani na wasomaji hawatapata nafasi ya kutafuta maana yake kwenye kamusi. Mhariri analenga hadhira ambayo inahitaji lugha nyepesi isiyotatanisha.

**5.3 Matokeo**

Tumetambua kuwa tahariri ya gazeti la *Taifa Leo* hutumia mtindo wa pekee ili kuwafikia wasomaji wake kwa njia rahisi isiyo na utata. Mhariri huteua maneno akiwa na lengo la kufikia hadhira anayoifahamu. Tahariri hizi zimezungumzia maswala yanayoathiri mwananchi wa kawaida, kwa hivyo msomaji anajihusisha na maswala yanayozungumziwa kwenye tahariri hizo. Mhariri wa *Taifa Leo* ameandika tahariri zenye urefu usiochosha msomaji, huku akitumia sentensi zenye miundo tofauti tofauti: sentensi sahili, sentensi ambatano na sentensi changamano, kulingana na ujumbe unaopitishwa. Mhariri ameibua maswala mbalimbali na kuyashughulikia/ kuyajadili kwa uwazi bila kutumia maneno mengi yanayorudiwa rudiwa ambayo yatamchosha msomaji. Mhariri ametumia vitenzi visaidizi ‘pasa’ ‘faa’ na ‘weza’ kutoa mapendekezo yake. Pamoja na hayo, virai kama vile: ‘wito wetu ni kuwa’, ‘ni wazi kwamba,’‘si siri kuwa’, na vingine, vimetumiwa na mhariri kueleza mtazamo wake.

Mada za tahariri ya *Taifa Leo* huwa na sehemu zote amilifu za sentensi; kiima na kiarifa. Mada hizi hutoa muhtasari wa yaliyomo kwenye tahariri hiyo. Mwandishi anateua msamiati kulingana na sajili husika. Kwa mfano, msamiati wa mchezo unatawala katika tahariri ya michezo. Uteuzi huu unafanikisha uwasilishaji wa ujumbe unaokusudiwa na mwandishi.

Tahariri za *Taifa Leo* hutekeleza mambo muhimu katika jamii; hukashifu maovu, hupongeza, huonya na kutoa ufafanuzi wa maswala tata. Majukumu haya yamewezekana kwa sababu mwandishi ametumia lugha kwa ubunifu mkuu.

Msamiati unateuliwa na mwandishi wa tahariri ili kufanikisha ujumbe kwa njia rahisi inayoeleweka. Maneno ya kawaida hutumiwa na tamathali ambazo ni rahisi kwa msomaji yeyote kufahamu, maana nia ni kuwasiliana.

### 5.4 Mapendekezo

Utafiti huu ulichunguza mtindo wa lugha na matumizi ya lugha katika tahariri ya gazeti la Taifa Leo. Tulichanganua tahariri zote; za kuhakiki, kusifu, kufafanua n.k. Miongoni mwazo ni tahariri za kushawishi na  kuhimiza. Utafiti mwingine unaweza kufanywa kwa kuangazia maudhui yanayowasilishwa katika  tahariri ya gazeti hili.

Utafiti wetu ulijikita kwenye uchanganuzi wa tahariri ya *Taifa leo*, gazeti ambalo ni la Kampuni ya Nation Media Group, utafiti linganishi wa kimtindo unaweza kufanywa kwa gazeti la *Daily Nation* na *Taifa Leo.*

# MAREJELEO


Agu, I. E. (2008). "*A Lingusitic-Stylistic Analysis of Soyinka's The Interpreters*". Unpublished PhD Thesis, Federal University of Technology Yola.

Albright, S. (2006). "Sights and Sounds of a Newspaper's Editorial", *Nieman Reports*, PP 70-71. from www.nieman.harvard.edu/reports/article/100306/sights-and-sounds-of-anewspapers-editorials.aspx . Retrieved on January 28, 2016

Ate, A. A. (2008). *JLS 713: Editorial Writing.* Retrieved April 18, 2016 from http://www.nou.edu.ng/noun/NOUN_OCL/pdf/jls%20725.pdf

Belmonte, A, I. (2008). "Newspaper Editorials and Comment Articles: A Cinderella Genre?", in Belmonte, A. I. (ed.) *Different Approaches to Newspaper Opinion Discourse.* Retrieved on January 27, 2016 from http://dialnet.unirioja.es/servlet/articulo?codigo=2546733.

Bhatia, V. K. (1993). *Analzing Genre: Language use in Professional Setting.* London: Longhorn.

Bonyadi, A. (2011). Linguistic Manifestation of Modality in Newspaper Editorials. *International Journal of Linguistics.* Vol. 3 Issue 1:E30 Pg 1-13. Retrieved on January 12, 2016 from www.macrothink.org/ijl.

Crystal, D. na Davy, D. (1969). *Investigating English Style.* London: Longman.

Elyazale, N. (2014), Characteristics of Newspaper Editorials: 'Chouftchouf' in 'Almassae' Moroccan Newspaper as a Case Study. *New Media and Mass Communication*. Vol. 32 Retrieved on January 12, 2016 from www.iiste.org

Etim, A. (1996). *Editorial Writing*. Port Harcourt: Sunray Books.

Finch, G. (2000). *Linguistic Terms and Concepts.* London: MacMillan Press Ltd.

Fowler, R. (1986). *Linguistic Criticism.* Oxford: Oxford University Press.

Greenberg, J. (2000). "Opinion Discourse and Canadian Newspapers: The case of the Chinese 'Boat People',"*Canadi San Journal of Communication Corporation*, Vol 25, No 4, PP. 517-537.

Habwe, J. na Karanja, P. (2004). *Misingi ya Sarufi ya Kiswahili.* Nairobi: Phoenix Publishers.

Hallock, S. (2008). “Same as It Ever Was Editorial Writers Grapple with Same Politics 100 Years Ago”, *ST Review Louis Journalism*, PP. 22-23, http://findarticles.com/p/articles/mi_hb6666/is_302_38/ai_n29406391. Retrived on February 4, 2016.

Heybels, S. & Weaver R. L. (2011). *Communicating Effectively*. New York: McGraw-Hill.

Hudgson, F, W. (1996). *Modern Newspaper Practice: A Prime on the Press*. Oxford: Focal Press.

Indangasi, H. (1998). *Stylistics*. Nairobi: Nairobi University Press.

Iribemwangi, P. I. na Mukhwana, A. (2011). *Isimujamii*. Nairobi: Focus Publishers.

Kitsao, J. (1975). *A Sytlistic Approach for the Study of Written Swahili Prose Texts.* Tasnifu ya uzamili (haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Nairobi.

Koubali, J. (2007). *News and Editorials in the British Press: A Corpus Based Study*. Rabat: Manibel Print.

Kress, G. (1983). Linguistics and Ideological Transformation in News Reporting in D. Howard and P. Walton (eds). *Language, Image, Media.* Oxford: Blackwell, Pg 120-138

Kroupová, I. 2012. *Earthquake in Japan (2011) in Tabloid and Broadsheet Press: Comparative Discourse Analysis.* Bachelor’s thesis, Masaryk University.

Kuhenga, C. (1977). *Tamathali za Usemi*. Nairobi: East African Literature Bureau.

Leech, G. & Short, M. (1989). *Style in Fiction*. Longman: New York.

Leech, G. & Short, M. (1981). *Style in Fiction: A Linguistic Introduction to English Fictional Prose*. London: Longman

Loughran, G. (2010). *Birth of a Nation*. London: I. B. Taurus & Co Ltd.

Lugwiri, P. O. (2011). “Sitiari, Taashira na Tashbiha katika uwasilishaji wa dhamira katika *Utenzi wa Tambuka*: Uhakiki wa Kimtindo”. Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Nairobi. Haijachapishwa.

Lyons, J. (1981). *Language and Linguistics: An Introduction*. Cambridge: Cambridge University Press.

Massamba D. P. B., Kihore, Y. M. na Msanjila, Y.P. (2004). *Fonolojia ya Kiswahili Sanifu (FOKISA): Sekondari na Vyuo*. Dar es Salaam : TUKI.

Mbatiah, M. (2001) *Kamusi ya Fasihi*. Nairobi: Standard Text-books Graphics and Publishing.

Mogambi, H. (2011). *Patterns of Production and Consumpion of Local Language Radio in Kenya: A Comparative Study of Rural Audiences.*University of Nairobi, Unpublished PhD Thesis.

Okoro, N & Agbo, B. (2003). *Writing For the Media Society.* Nsukka: Prize Publishers.

Omari, J. O. & Meitamei, A. ( 2014). Taifa Leo Newspaper as a Tool for Teaching and Learning Swahili Language in Secondary Schools in Kenya. *International Journal of Science and Research*, Vol 3, Issue 12. Pg. 2546-2550.

Otuoma, D. A. (2015). *Mitindo na Maudhui katika Uchanganuzi wa Vibonzo kwenye Gazeti la Taifa Leo.* Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Nairobi. Haijachapishwa.

Richardson, J. E. (2007). *Analyzing Newspapers. An Approach from Critical Discourse Analysis*. New York: Palgrave Macmillan.

Soi, F. C. (2014). *A Stylistic and Pragmatic Study of Kipsigis Proverbs*. Tasnifu ya Uzamili (M. A), Chuo Kikuu cha Nairobi. Haijachapishwa.

Susinskiene, S. (2010). Nominalization as a Cohesive Device in British Newspaper Editorials. *Filologija*. Pg 143-150.

Syambo, B. na Mazrui, A. (1992). Uchambuzi wa Fasihi. Nairobi: East African Education Publishers.

The Washington Post (2003). The Washington Post Company. Vol.1 Issue 4, Pg 1-15

TUKI (2004). Kamusi ya Kiswahili Sanifu. Nairobi: Oxford University Press.

TUKI (2006). *Kamusi ya Kiingereza-Kiswahili. Toleo la Tatu*. Dar-es- Salaam: TUKI.

Van Dijk, T. A. (1988). *News Analysis: Case Studies of International and National News in the Press.* New Jersey: Lawrenc Erlbaum Associates.

Van Dijk, T. A. (1992). "Racism and Argumentation: Race and Riot Rhetoric in Tabloid Editorials", in F, H VanEmeren.et al (eds.), *Argumentation Illuminated.* Dordrecht: Foris. PP. 242-259.

Van Dijk, T. A. (1995). "Discourse, Opinions and Ideologies", *Current Issues in Language and Society*. Vol 2, No. 2, PP. 1-23.

Van Dijk, T. A. (1996). "Opinion and Ideologies in Editorials", Paper for the Fourth Annual International Symposium of Critical Discourse Analysis, December 14-16, Athens. Retrieved on December 16, 2015 from http://www.discourse.org/unpublishedarticles/opinion%20ideologies%20in%20editorials.htm.

Van Dijk, T. A. (1998). *Ideology: A Multidisciplinary Approach*. London: Sage Publications.

Wamitila, K. W. (2003). *Kamusi ya Fasihi: Istilahi na Nadharia*. Nairobi: Focus Publications Ltd.

Wamitila, K. W. (2008). *Kanzi Ya Fasihi: Misingi ya Uchanganuzi wa Fasihi*. Nairobi: Vide Muwa Publishers Ltd.

Wekesa, N. B. (2012). Assessing Argumentative Normativity in the English Medium Kenyan Newspaper Editorials from a Linguistic-Pragmatic Approach. *International Journal of Humanities and Social Sciences*.Vol. 2 Issue 21, Pg. 133-144.

# VIAMBATANISHO

TAIFA LEO Alhamisi, Januari 7, 2016

TAIFA LEO
Nation Centre • Kimathi Street • Nairobi

## Uchochezi: Asasi husika ziwajibike

MATAMSHI ya mwanasiasa Suleiman Shahbal kwamba Serikali inapanga kushinda katika Uchaguzi Mkuu wa 2017 'kwa njia zozote zile' ni hatari kwa nchi.

Uhalali wa matamshi hayo unapaswa kuchunguzwa, ikizingatiwa kwamba tayari wanasiasa wameanza kampeni za kichinichini za uchaguzi huo.

Kilichoshtua zaidi ni kuwa alipotoa kauli hiyo Naibu Rais William Ruto alikuwepo ila alimtazama tu bila kusema lolote.

Kimsingi, kilichotarajiwa ni kwamba angaa Bw Ruto angechukua nafasi hiyo kuyapinga na kusema kwamba huo si msimamo wa Serikali ya Jubilee. Hata hivyo, kimya chake kinaashiria kwamba huenda anaunga mkono matamshi hayo.

Si mara moja tumewaona wanasiasa wakitoa matamshi ya uchochezi huku asasi husika zikikosa kuwachukulia hatua.

Kando na Bw Shahbal, kinara wa Cord amedai kwamba Serikali ina njama za kuiba kura katika uchaguzi mkuu ujao.

Ijapokuwa kiuhalisia matamshi hayo kutoka mirengo hiyo miwili inaashiria ushindani wa kisiasa, kilicho wazi ni kwamba wanasiasa hao wanapanda hisia za chuki miongoni mwa Wakenya.

Bw Odinga alifeli kutoa ushahidi wa madai yake, sawa na vile Bw Ruto alikosa kueleza msimamo wa serikali kuhusu matamshi ya Bw Shahbal.

Ni kinaya kwamba tunaendelea kushuhudia matamshi kama haya huku tukiwa bado hatujaponya vidonda vinavyotokana na athari za chuki za kikabila. Matamshi kama haya ndiyo yaliyopelekea kutokea kwa ghasia za uchaguzi tata wa 2007.

Zaidi ni kuwa, kabla ya kutokea kwa machafuko hayo, viongozi wa kisiasa walikuwa wakizunguka kote nchini wakitoa matamshi ya uchochezi bila kuchukuliwa hatua zozote.

Changamoto kuu ni kwa Tume ya Uwiano na Utangamano wa Kitaifa (NCIC) kufahamu kwamba inafeli katika wajibu wa kuendeleza maelewano miongoni mwa jamii mbalimbali nchini.

Tiba ni viongozi kuchukuliwa hatua kali za kisheria. Ikiwa hilo halitafanyika, kuna hatari ya nchi kukumbwa na mkosi kama wa 2007.

Ni Gazeti la Kampuni ya Nation Media Group
Mkurugenzi Mkuu: JOE MUGANDA
Mhariri Mkuu: TOM MSHINDI
Mhariri Msimamizi: NICHOLAS MUEMA

TAIFA LEO
Nation Centre • Kimathi Street • Nairobi

# IEBC iwashirikishe wote inapojiandaa

TUME Huru ya Uchaguzi na Mipaka (IEBC) imetangaza ratiba yake ya kuandaa uchaguzi mkuu wa 2017.

Ratiba hiyo ilipasa kuanza mapema lakini kutokana na changamoto la kukosa pesa hilo halikuwezekana.

Baada ya kutangaza ratiba hiyo, IEBC ilisema kwamba iko tayari kuandaa uchaguzi huru na wa haki na imewataka Wakenya kuiunga mkono kufanikisha shughuli hiyo muhimu kwa nchi.

Tunaunga wito wa tume hiyo na kuwaomba wanasiasa, Serikali na Wakenya kuwa msitari wa mbele ili kuhakikisha uchaguzi mkuu ujao utakuwa bora zaidi, wa kuaminiwa, haki na huru.

Wanasiasa na hasa wabunge, wanapasa kuhakikisha IEBC imepewa pesa za kutosha ili kufanya maandalizi ya kubambe. Aidha, wanasiasa wa vyama tofauti wanapasa kuwahimiza wafuasi wao kujisajili kuwa wapiga kura na kudumisha amani kabla na hata baada ya uchaguzi.

Tume hii imeshatangaza kwamba ilipewa robo ya pesa ilizokuwa imeomba ili kusimamia uchaguzi ujao. Serikali ina jukumu la kutoa pesa kwa IEBC tena kwa wakati ili isilaumiwe kwa kuhujumu tume hiyo.

Serikali imekuwa ikilaumiwa kwa kuchelewa kutoa pesa kwa tume hiyo hatua ambayo inaweza kufanya ilaumiwe maandalizi ya kutosha yakikosa kufanyika.

Hii ni pamoja na kuhakikisha vijana wote waliofikisha umri wa miaka kumi na minane wamepata vitambulisho vya kitaifa.

Wakenya nao wanapasa kujitokeza kwa wingi kujisajili kushiriki kwenye uchaguzi msimu wa maandalizi. Kila mmoja anapasa kumhimiza mwenzake aliye na kitambulisho cha kitaifa kujitokeza katika vituo vya kujisajili IEBC itakapoanza kuandikisha wapiga kura wapya.

Kwa upande wake, IEBC inapaswa kushirikisha mirengo tofuati ya kisiasa katika maandalizi hayo ili isionekane kuegemea upande mmoja. Ikifanya hivi, vyama vya kisiasa havitakuwa na mwanya wa kulaumu utendakazi wake.

Wito wetu ni kwa kila Mkenya kutekeleza wajibu wake ili kufanikisha uchaguzi mkuu wa kwanza chini ya mfumo wa utawala wa ugatuzi.

Ni Gazeti la Kampuni ya Nation Media Group
Mkurugenzi Mkuu: JOE MUGANDA
Mhariri Mkuu: TOM MSHINDI
Mhariri Msimamizi: NICHOLAS MUEMA

19/01/2016

**TAIFA LEO**

Nation Centre • Kimathi Street • Nairobi

# Kitendo cha Salah ni mfano kwa tuliobaki

KIFO cha Bw Salah Farah, aliyewaokoa abiria Wakristo katika shambulio dhidi ya basi moja mwezi Desemba mwaka uliopita katika eneo la Mandera ni cha kuhuzunisha.

Bw Farah, ambaye mwenyewe ni Mwislamu, aliweka tofauti zote za kidini na kushiriki kishujaa katika tukio hilo ambalo lilisifiwa na kila mmoja nchini na kote duniani.

Kifo chake ni cha shujaa ambaye tunapaswa kumwenzi kwa kudhihirisha kwamba dhana ambazo zimekuwepo kuhusu dini fulani na ugaidi si za kweli.

Bw Farah na wenzake waliohusika katika kitendo hicho walidhihirisha kuwa ni watu wachache ambao wamekuwa wakibuni itikadi mbaya kuhusu Uislamu na ugaidi. Alitufunza kuwa hakuna tofauti zozote kati ya Waislamu na Wakristo; wote ni ndugu.

Kutokana na kifo chake, kile tutafanya kumpa hekima anayostahili ni kuendesha kudumisha ujumbe aliyotupa; kwamba sote tu ndugu.

Alidhihirisha kwamba propaganda za 'uhasama' ambazo zimekuwa zikiendeshwa na baadhi ya viongozi wa dini hizi zote mbili hazina umantiki wowote.

Kwa hayo, ni jukumu letu kujitwika jukumu la kufahamu kwamba vita dhidi ya ugaidi huenda zisifauli kwa kutumia mitutu ya bunduki.

Vita hivyo, ambavyo msingi wake ni uenezaji wa chuki zisizofaa za kikabila na kidini vitafaulu kwa kueneza ukweli halisi kwamba watu wachache ndiyo wanaozieneza kwa lengo la kujinufaisha wao wenyewe.

Twapaswa kufahamu kuwa athari za ugaidi zinamwathiri kila mmoja. Kwa hivyo, kila mmoja wetu anafaa kuchukua jukumu la kuhakikisha tumeendeleza uwiano na utangamano. Kwa njia hiyo, tutawakabili wale wachache wanaotaka kuvuruga amani iliyopo miongoni mwetu.

Ingawa tutamwomboleza kama balozi wa amani, daima tutakumbuka kujitolea kwake. Yeye ni kafara ya ujumbe wa ukweli.

Ni Gazeti la Kampuni ya Nation Media Group
Mkurugenzi Mkuu: JOE MUGANDA
Mhariri Mkuu: TOM MSHINDI
Mhariri Msimamizi: NICHOLAS MUEMA

TAIFA LEO Jumatatu, Januari 25, 2016

TAIFA LEO

Nation Centre • Kimathi Street • Nairobi

# Kuwe na sera maalum kukabiliana na ufisadi

KAULI ya rais Uhuru Kenyatta kwamba aliwashuhudia maafisa wawili wa polisi wa trafiki wakichukua mlungula barabarani, ni ushahidi tosha wa jinsi maafisa wa umma wanavyoifilisi nchi kupitia ufisadi.

Maafisa hao wa Mombasa walikosa hata kuheshimu kuwepo kwa rais na wakuu wengine wa serikali katika mji wao, na inasemekana waliitisha pesa peupe mchana bila kujali kama ufisadi ni uhalifu.

Kitendo cha maafisa hao hakikustahili, lakini kinatilia nguvu ripoti mbalimbali za mashirika ya Kimataifa kama Transparency International (TI), kwamba kuna uozo na ufisadi katika idara ya polisi Kenya.

Kwa hivyo, kauli ya Rais Kenyatta kwamba hatavumilia ufisadi wa aina hiyo, inafaa kuungwa mkono na Wakenya wote. Tunapounga mkono hatua ya kuwafuta kazi maafisa wa polisi walionaswa, tunashauri kuwe na mikakati na sera rasmi za jinsi ya kukabiliana na jinamizi la ufisadi nchini.

Kufutwa kwa maafisa hao ni tukio moja tu. Kuna visa vingi vya ufisadi vinavyoendelea nchini ambavyo Wakenya wanavishuhudia, lakini hawana namna ya kuvikemea wala kuchukua hatua.

Japokuwa kuwafuta kazi wanaoshukiwa kuwa wafisadi ni hatua nzuri, ipo haja ya kuzifanya taasisi zote za umma zinazohusika na suala hili kuwa na nguvu ipasavyo. Kwa mfano kuwe na sheria itakayowapa nguvu wananchi kuwanasa washukiwa wa ufisadi, bila kuwepo hatari ya watu kuwasingizia wengine uongo. Aidha, Tume ya Maadili na Kupambana na Ufisadi (EACC), afisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka ya Umma pamoja na Mahakama, ziwe na utaratibu unaotambuliwa na raia kuhusu usikizaji na uamuzi kuhusiana na kesi za ufisadi.

Iwapo kutakuwa na sera maalum ambazo kila mwananchi atazitambua, basi hakutakuwa na haja ya kusubiri hadi rais azuru eneo, kabla ya kuwachukulia hatua wanaojihusisha na ufisadi. Sera hizo, zitawapa nguvu wananchi kuripoti visa kama hivyo kwa taasisi husika.

Ni Gazeti la Kampuni ya Nation Media Group
Mkurugenzi Mkuu: JOE MUGANDA
Mhariri Mkuu: TOM MSHINDI
Mhariri Msimamizi: NICHOLAS MUEMA

TAIFA LEO
Nation Centre • Kimathi Street • Nairobi

# NTSA ionyeshe makali yake kwa wahudumu

TANGAZO la Halmashauri ya Kitaifa na Usafiri na Uchukuzi (NTSA) kwamba ingeanza msako mkali dhidi ya magari yanayokiuka sheria za trafiki kuanzia jana lilipokelewa vizuri na umma.

Wengi walitarajia kuwa halmashauri hiyo ingekaza kamba na kulainisha sekta ya uchukuzi wa umma, ambayo imekuwa kama uwanja wa mapigano kwa miaka mingi kwa kukosa sheria zinazoidhibiti.

Hata hivyo, 'ukali' wa tangazo hilo haukudhihirika, kwani ukawaida Wakenya wamezoea katika sekta ya uchukuzi uliendelea kudhihirika jana.

Tulitarajia kuona makali ya NTSA. Wengi walikuwa na matumaini kuwa magari ya umma yangeondoa eksozi ambazo huwa zinasababisha kelele na kuwaharibia mazingira wananchi.

Wengi walitarajia kuwa kwa onyo hilo, matatu ambazo zina michoro ya kuogofya hazingejitokeza barabarani.

Na licha ya kuwa wahudumu wengi walionekana kutojitokeza kuwabeba abiria jana, kile kilijitokeza ni kuwa onyo hili la NTSA halikuchukuliwa kwa uzito. Ijapokuwa hatuielekezi lawama moja kwa moja, kauli yetu ni kuwa ukali wa kauli yake ulipaswa kudhihirika kuanzia jana.

Ikumbukwe kuwa alipotoa kauli yake ya kulainisha sekta ya matatu mnamo 2003, aliyekuwa Waziri wa Uchukuzi marehemu John Michuki alishikilia kuwa gari lolote ambalo lilitarajia kuhudumu barabarani lazima lingetimiza kanuni zilizowekwa.

Baadhi ya kanuni hizo ni hitaji la kuwa na vidhibiti mwendo pamoja na mikanda ya usalama.

Kutokana na ukakamavu wake, wamiliki wengi wa magari walilazimika kutii agizo hilo, licha ya lalama walizotoa.

Tangu leo, matokeo ya msimamo mkali wa Bw Michuki yangali dhahiri. Msimamo wa Bw Michuki unapaswa kuwa funzo kuu kwa maafisa wakuu wa NTSA, kuwa ni hadi pale watakapokuwa na msimamo mkali ndipo nidhamu itarejea katika sekta ya matatu.

Ni Gazeti la Kampuni ya Nation Media Group
Mkurugenzi Mkuu: JOE MUGANDA
Mhariri Mkuu: TOM MSHINDI
Mhariri Msimamizi: NICHOLAS MUEMA

TAIFA LEO Jumatano, Januari 27, 2016

TAIFA LEO
Nation Centre • Kimathi Street • Nairobi

# Madiwani wafikirie upya kuhusu elimu

HATUA ya madiwani kupinga mswada unaolenga kuinua kiwango chao cha elimu ya wnaaotaka wadhifa huo ni ya kuvunja moyo.

Mswada huo unatoa pendekezo kuwa madiwani wawe na elimu ya kiwango cha diploma ama digrii kuanzia Uchaguzi Mkuu wa 2017.

Hata hivyo, wameungana pamoja kuupinga kwa visingizio kuwa uwezo wa uongozi haulingani kwa vyovyote vile na kiwango cha elimu alicho nacho mtu. Madiwani pia wamedai kuwa mswada huo ni njama za Bunge la Kitaifa la kuwahujumu.

Madiwani hawa huenda wnaasema kweli, lakini wanapaswa kufahamu kuwa nyakati zimebadilika. Elimu imekuwa mhimili mkuu wa uendeshaji wa shughuli mbalimbali nchini na kote duniani.

Japo ni kweli kuna hali za kipekee ambapo baadhi ya viongozi bora si lazima wawe wamesoma, ukweli ni kuwa elimu huwa muhimu sana katika uimarishaji wa utendakazi wa viongozi wanaochaguliwa.

Kwanza, majukumu yao yanahitaji wawe na elimu ya kutosha. Wanapaswa kujadili na kupitisha miswada muhimu inayohusu usimamizi na uendeshaji wa Serikali za Kaunti. Pia wana usemi mkubwa kuhusu jinsi fedha ambazo serikali hizo zinatengewa na Serikali Kuu zinapaswa kutumiwa.

Ni muhimu kwa miswada inayowasilishwa kuwa mizuri na yenye manufaa kwa wakazi wa kaunti husika. Hili ni jukumu ambalo linahitaji uelewa mpana wa utaratibu mzima wa utayarishaji wa mswada husika, na jinsi utakuwa na manufaa kwa walengwa wakuu.

Kando na hayo, majukumu yao ni mazito na yenye umuhimu mkubwa kuliko madiwani wa zamani. Wengi, hasa vijana, wanawachukulia kama mifano ya kuigwa katika jamii. Madiwani wanalipwa vizuri na maisha yao yameimarika. Ni mfano gani wanaotaka kuwaonyesha vijana? kwamba unaweza kufanikiwa bila ya masomo ya maana?

Kwa hivyo, yawapasa kutambua kuwa kuinuliwa kwa kiwango cha elimu, kutakuwa na manufaa kwao binafsi pamoja na uongozi mzima wa Serikali za Kaunti.

Ni Gazeti la Kampuni ya Nation Media Group
Mkurugenzi Mkuu: JOE MUGANDA
Mhariri Mkuu: TOM MSHINDI
Mhariri Msimamizi: NICHOLAS MUEMA

TAIFA LEO
Nation Centre • Kimathi Street • Nairobi

# Ugaidi: Kenyatta na Buhari wajadiliane

ZIARA ya Rais wa Nigeria Muhamadu Buhari nchini ina umuhimu mkubwa wakati huu mataifa haya mawili yanapoendeleza juhudi za kujinasua kutoka mikononi mwa magaidi.

Kuna haja ya mataifa haya mawili kwa usaidizi wa jamii ya kimataifa pamoja na Muungano wa Afrika, kuafikiana kuhusu mbinu mwafaka za kupunguza maafa kutokana na ugaidi.

Vyanzo vya kuchipuka kwa mashambulizi ya kigaidi katika mataifa haya mawili ni sawa, hivyo suluhu la pamoja la kulinda raia wa mataifa haya ni muhimu.

Nchini Nigeria, chanzo cha kundi la Boko Haram ni umaskini licha ya taifa hilo kuwa na utajiri mkubwa zaidi wa mafuta barani. Wapiganaji wa Boko Haram wanalenga vijana wasiokuwa na kazi kuwasajili katika vitendo vya ugaidi.

Maeneo 12 ya Kaskazini Mashariki mwa Nigeria ambapo Boko Haram limekita mizizi, yameorodheshwa kuwa na umaskini maradufu ikilinganishwa na maeneo mengine nchini humo.

Tayari serikali ya Rais Buhari imepunguza matumizi ya jeshi kupambana na ugaidi na badala yake kuanzisha sera za kupunguza umaskini na kutoa nafasi zaidi za ajira kwa vijana.

Kwa upande wake, Kenya ambapo kundi la Al shabaab linaendeleza mashambulizi dhidi ya raia na jeshi, kumezuka mjadala mkali iwapo kuendelea kuwa Somalia kwa wanajeshi wake kunasaidia kupunguza mashambulizi ya kigaidi.

Kando na matumizi ya kijeshi, Rais Buhari na mwenyeji wake Rais Uhuru Kenyatta wanapaswa kubadilishana mawazo kuhusu kuenea kwa misimamo mikali ya kidini hasa Uislamu.

Makundi yote mawili, Boko Haram na Al shaabab yanatumia dini na hisia za kisiasa kugawanya jamii kwa lengo la kueneza misimamo yao mikali na potovu.

Buhari na Kenyatta wana adui sawa hatari na sharti waungane na kubadili mbinu za kumuangamiza.

Ni Gazeti la Kampuni ya Nation Media Group
Mkurugenzi Mkuu: JOE MUGANDA
Mhariri Mkuu: TOM MSHINDI
Mhariri Msimamizi: NICHOLAS MUEMA

TAIFA LEO
NATION CENTRE KIMATHI STREET NAIROBI
29/01/2016

# Serikali ifafanue kukihusu chama

SERIKALI inafaa iombe msamaha na kufafanulia wazazi na walimu jinsi shirika lisilo halali liliruhusiwa kuingilia shughuli za elimu kwa miaka mingi.

Hii ni kufuatia hatua ya Waziri wa Elimu Dkt Fred Matiang'i kupiga marufuku Chama cha Kitaifa cha Wazazi (KNAP) kujihusisha na uchaguzi wa wawakilishi wa wazazi shuleni na pia kupokea pesa kutoka kwa shule za umma.

Kwa muda mwingi wadau katika sekta ya elimu walikuwa wakilalamika kuwa hawaelewi jinsi chama hicho kilibuniwa, huku baadhi ya wazazi pia wakishangaa ni lini uchaguzi uliitishwa kumchagua Bw Musau Ndunda kuwakilisha masilahi yao.

Hii ni licha ya Bw Ndunda ambaye ndiye katibu mkuu wa muda mrefu wa chama hicho kusisitiza wakati huo wote kuwa, chama chake ni halali. Kufikia jana, alikuwa hajazungumzia suala hilo.

Tangu chama hicho kijulikane, hakijawahahi kutangazwa mkutano wa mwaka wala kuitishwa kwa uchaguzi. Iwapo kimewahi kufanya hivyo, basi si kwa kutangaziwa umma. Jambo hili halieleweki kwa sababu, Msajili wa Vyama vya aina yoyote, huweka kanuni, ikiwemo chama kufanya japo mkutano mmoja kwa mwaka.

Kinachoshangaza zaidi ni kuwa Wizara ya Elimu ilikuwa imeagiza wakurugenzi wa elimu katika kila kaunti kukabidhi chama hicho pesa za kuendeleza shughuli zake za kuwakilisha wazazi, katika mwaka wa 2013.

Inasemekana kila shule ilihitajika kutoa Sh2,000 mwaka uliopita kufadhili chama hicho, ambayo kwa jumla kitaifa, chama hicho kingepokea Sh65 milioni.

Hatua ya kupiga breki shughuli za chama hicho haitoshi, kwa kuwa bado kuna maswali mengi ambayo wazazi na wadau wengine katika sekta ya elimu wangependa wajibiwe na serikali baada ya kuwaomba msamaha.

Wizara ya Elimu lazima ijitokeze na kueleza ilikuwa vipi hadi sheria ikakiukwa kuwezesha chama hicho kuendeleza shughuli zake.

Maafisa wa serikali waliohusika katika kukiruhusu kuhudumu lazima wachunguzwe ili ifichuliwe kama kulikuwa na njama yoyote kati yao na chama hicho.

Haieleweki jinsi chama kinaweza kuingilia shughuli katika sekta yenye umuhimu mkubwa kitaifa kama elimu kwa njia isiyo halali, na serikali haitambui hilo kwa miaka hiyo yote licha ya malalamishi kutoka kwa wadau wakuu.

Ni Gazeti la Kampuni ya Nation Media Group
Mkurugenzi Mkuu: **JOE MUGANDA**
Mhariri Mkuu: **TOM MSHINDI**
Mhariri Msimamizi: **NICHOLAS MUEMA**

TAIFA LEO
NATION CENTRE KIMATHI STREET NAIROBI
30/01/2016

# Shime kwa wenye nia ya kuauni timu

Ni jambo la kutia moyo kuwa mashirika sasa yameanza kujitokeza kudhamini baadhi ya klabu za nchini humu ambazo zimekuwa zikisaka hisani kama hiyo bila mafanikio.

Tunayatia shime mashirika hayo yajipe ujasiri huo na kufanyia Wakenya heri hiyo kuu ambayo wametamani sana kwa muda mrefu. Duru zinasema kuwa mashirika yanayojihusisha na ubashiri wa matokeo ya michezo ndiyo yaliyo katika mstari wa mbele kuokoa klabu zetu hasa Gor Mahia na AFC Leopards zinazozidi kutikisika kutokana na ufilisi wa kimapato.

Ni bayana kuwa bila Gor na Leopards, basi soka ya Kenya imekufa. Kwa hivyo, ni hatua yenye umuhimu mkubwa kwa mashirika hayo kusaidia kunusuru kandanda yetu isije ikafa na kufukiwa kwenye kaburi la sahau kama ishara zilivyokuwa zimeanza kuonyesha.

Gor kwa upande mmoja ilikuwa imeanza kutishia kutoshiriki mechi za Klabu Bingwa Afrika (Caf) kutokana na uchechefu wa pesa nayo Leopards kwa upande mwingine ikikamilisha ligi kuu ya mwaka jana ikijikokota kama rukwama hasa baada ya mdhamini wake, Mumias Sugar kujipata katika mtanziko mkuu wa kifedha.

Hivyo basi tunachukua fursa hii kuhimiza SportPesa, betway, mCHEZA miongoni mwa mashirika mengine ya ubashiri kuchukua fursa hii kuzifaa timu zetu kama mojawapo ya njia za kutafuta wateja zaidi kwa madhumuni ya kujikuza kiuchumi.

Hata hivyo, itakuwa aula zaidi ikiwa mashirika mengineyo, mbali na haya ya ubashiri, kujitokeza kuzipiga jeki timu zetu, si Leopards na Gor tu, bali hata zile zinazoshiriki kabumbu ya daraja za chini.

Hii itakuwa kwa moyo wa kuimarisha soka ya mashinani kama njia ya kuwatafutia vijana ajira.

Mashirika kama Safaricom, EABL, benki kongwe na kwasi nchini kama vile KCB, Co-op Bank na Equity zinaombwa zijitoe mhanga kuchangia katika makuzi ya kandanda nchini.

Kwa msingi huo, shukrani kuu ziwaendee tena SportPesa kwa kujitwika jukumu faafu zaidi la kudhamini ligi kuu ya Kenya ambayo inajizatiti kujinyanyua. Lakini iwapo shirika hili litajitolea kusaidia klabu binafsi, pia lifahamu kuwa litakuwa limewafanyia Wakenya afua kubwa isiyomithilika.

Ingawa kutoa ni moyo usambe ni utajiri. Betway (si kwa kupuuza SportPesa au mCHEZA), ambalo ni shirika kubwa la kimataifa na lenye uwezo mkubwa kifedha, bila shaka litafaa zaidi iwapo litatoa ufadhili mnono kwa klabu hizi.

Ni Gazeti la Kampuni ya Nation Media Group
Mkurugenzi Mkuu: **JOE MUGANDA**
Mhariri Mkuu: **TOM MSHINDI**
Mhariri Msimamizi: **NICHOLAS MUEMA**

TAIFA LEO

NATION CENTRE KIMATHI STREET NAIROBI 01/02/2016

# Leopards msiache ufadhili ukateleza

BAADA ya AFC Leopards kutapatana sana msimu uliopita bila udhamini, pana haja ya jitihada zote kufanywa ili kuhakikisha kuwa ufadhili unaobisha mlangoni pa klabu hiyo hautelezi kamwe.

Hii ni baada ya vinara wawili wa klabu hii, mwenyekiti wa mpito Matthews Opwora na naibu wake Dan Mule, kutia sahihi mikataba tofauti ya udhamini na shirika la kibahati nasibu michezoni la Betway.

Dosari hiyo katika harakati ya kuidhinisha ufadhili ilisababisha suala zima kupelekwa katika korti ya kusuluhisha migogoro ya kispoti ambapo iliamuliwa kuwa udhamini huo si halali.

Hata hivyo, pameibuka dalili za dosari hiyo kufutwa ambapo sasa mkataba mnyoofu unatazamiwa kutiwa saini hapo Jumanne.

Ni maombi yetu kuwa mtafaruku wa kiuongozi ambao umekuwa ukitinga klabu hii sasa utamalizwa kabisa kwa ajili ya manufaa ya mashabiki na makuzi ya kandanda nchini humu.

Inapozingatiwa kuwa shirika hili ni la kimataifa, inakuwa busara kuonyesha ulimwengu ukomavu kwa kuafikiana katika mambo muhimu, hali ambayo bila shaka itawatia shime wadau wengine wa mchezo huu, si nchini tu bali duniani kote, kuja Kenya kusaidia kuzifanya timu zetu pamoja na soka thabiti.

Waama udhamini wa takribani Sh30 milioni kwa mwaka utakuwa auni kubwa kwa timu hii ambayo ililazimika kujiendesha bila senti ya maana pindi mdhamini wake wa awali Mumias Sugar alipojiondoa mwaka jana.

Leopards pamoja na Gor Mahia ambayo nayo ilipata udhamini afua wa SporPesa (Sh60 milioni kwa mwaka), zinapoinuka, inakuwa fahari ya Wakenya wote kwani ndizo klabu zinazoshabikiwa zaidi nchini humu.

Bila shaka matarajio ya timu hizi mbili kujiinua, kurejesha mashabiki viwanjani, kuimarisha msisimko mbali na kuchangia kukuza soka ya kitaifa hasa Harambee Stars, sasa yamepigwa jeki.

Yakini huu ni mwanzo wa mambo mema yanayosubiri soka yetu. Pana ishara tosha kuwa mashirika mengine ya kibiashara nayo yatajitokeza ili kukomboa kabumbu yetu ambayo ilikuwa imeanza kuchungulia kaburi.

Juu ya yote heko kubwa kwa SportPesa na Betway kwa kuonyesha hisani hiyo inayostahili kuigwa na mashirika mengine mengi nchini na kimataifa.

Ni Gazeti la Kampuni ya Nation Media Group
Mkurugenzi Mkuu: **JOE MUGANDA**
Mhariri Mkuu: **TOM MSHINDI**
Mhariri Msimamizi: **NICHOLAS MUEMA**

TAIFA LEO

NATION CENTRE KIMATHI STREET NAIROBI

05/02/2016

# Wenye teksi wajue teknolojia

WAHUDUMU wa teksi jijini Nairobi wanafaa kukubali tuko katika enzi za kiteknolojia na waanze kukumbatia teknolojia za kisasa kuendeleza biashara zao.

Mizozo kati yao na kampuni mpya ya Uber ambayo imeshuhudiwa katika siku za hivi majuzi inatokana pakubwa na kuwa mbinu zao za biashara hazitaweza kustahimili mbinu za kisasa zinazotumiwa na kampuni hiyo.

Imedhihirika kuwa teknolojia hupelekea kurahisisha utoaji wa huduma na hata wakati mwingi hupunguzia wateja gharama ya kupokea huduma tofauti.

Kampuni ya Uber ambayo ina mizizi yake katika mataifa ya magharibi, tayari imedhihirisha kuwa huduma za teksi zinaweza kutolewa kwa bei nafuu zaidi kwa kutumia mbinu za kisasa.

Wahudumu ambao wamekuwepo kwa muda mrefu wamekuwa wakitoza pesa nyingi za nauli kutoka kwa wateja wao.

Kampuni hiyo mpya imetumia mbinu za kisasa kujipunguzia gharama za matumizi katika biashara na hivyo basi kupunguza ada inayotozwa kutoka kwa wateja wao.

Badala ya kuanzisha mizozo, wahudumu wa teksi wa kawaida wanahitajika kujifunza kuhusu mbinu ambazo kampuni hiyo inatumia. Kisha watafute mbinu zao bora za kushindana nao kama wanaona hawawezi kutumia zile za kiteknolojia.

Si siri kuwa kila mwananchi hutaka huduma bora kwa bei nafuu. Kwa hivyo mradi tu Uber itakuwa inaendesha biashara zake kwa kufuata sheria za nchi, bila shaka wengi watakuwa wakitafuta huduma zake.

Mvutano ambao umetokea unaibua kumbukumbu za wakati ambapo huduma za kutuma na kupokea pesa kwa njia ya simu zilizinduliwa nchini na kampuni ya Safaricom.

Benki nyingi zilipinga mtindo huo wa utoaji wa huduma za pesa na kulalamika biashara zao zingeathirika vibaya.

Hii leo benki zimejifunza kushirikiana na kampuni hiyo kwa njia ambayo pia nazo zinafaidika kutokana na huduma hizo zilizochochewa na teknolojia za kisasa.

Jambo la muhimu ni kuwa kila mwananchi, si wahudumu wa teksi pekee, anapaswa kukubali tuko katika enzi za kiteknolojia. Hivyo basi, kila tunachofanya kinafaa kifanywe tukijitayarisha kwa mabadiliko ambayo yatazidi kutokea na kuathiri shughuli zetu.

Ni Gazeti la Kampuni ya Nation Media Group
Mkurugenzi Mkuu: **JOE MUGANDA**
Mhariri Mkuu: **TOM MSHINDI**
Mhariri Msimamizi: **NICHOLAS MUEMA**

TAIFA Jumapili
NATION CENTRE KIMATHI STREET NAIROBI.
07/02/2016

# Visa vya wanandoa kuumizana ni aibu

ONGEZEKO la visa vya dhuluma za kimapenzi nchini limeibua wasiwasi kuhusu uthabiti wa taasisi ya ndoa na hata mustakabali wake.

Katika siku za hivi karibuni, tumeshuhudia visa kadhaa ambapo wanandoa ama wapenzi wamekuwa wakipigana, kwa kiasi cha kujeruhiana wao kwa wao.

Kwa mfano, kisa ambacho kilizua hisia kali ni kile cha mwanamke wa miaka 21, aliyetambuliwa kama Kawira, ambaye alinaswa na video akipigwa vibaya na mumewe.

La kushangaza ni kwamba, mwathiriwa alikuwa akipigwa licha ya kuwa mjamzito. Zaidi ni kuwa, majirani wake walitazama ukatili huo ukiendelea bila kuchukua hatua zozote.

Wengine wamelazwa hospitalini kutokana na majeraha waliopata katika matukio hayo.

Kwenye baadhi ya matukio, sababu kuu za mivurugano hiyo zimekuwa ndogondogo; ambazo zingeweza kusuluhishwa.

Kijumla, tunaloshuhudia ni mwelekeo ambao unaashiria uwepo wa mtikiso mkubwa wa kimaadili na kuaminiana miongoni mwa wanandoa ama wapenzi.

Yasikitisha kuwa visa hivi vimekuwa vikiongezeka licha ya asasi husika kuahidi kuchukua hatua dhidi ya wanaohusika.

Kinachoibuka kutokana na mkondo huu ni kuwa kuna umuhimu mkubwa wa uwepo wa uhamasisho wa jinsi wanandoa wanapaswa kuishi.

Hii ni kwa sababu madhara yanayotokea kutokana na visa hivi ni makubwa na hatari. Moja ni kuwa katika visa ambapo mwanandoa anafariki kutokana na dhuluma kama hizi, huwa kuna uwezekano mkubwa kwa watoto wachanga kuachwa bila msingi ufaao wa kiulezi.

Kwa upana, watoto hao huanza kukumbwa na changamoto za kimaisha wakiwa wangali wachanga.

Na katika matukio ambapo wao hufahamu kilichosababisha kutengana kwa wazazi wao, mara nyingi huwa wanaathiriwa na changamoto kama hizo.

Kutokana na haya, wito wetu ni kwa watu walio katika mahusiano ama ndoa kutathmini njia mwafaka za kusuluhisha tofauti zao kabla ya kuchukua sheria za kuadhibiana wao kwa wao.

Changamoto nyingine ni kwa asasi husika kushiriki kikamilifu ku waelimisha wanandoa jinsi ya kushughulikia tofauti zao.

Ni Gazeti la Kampuni ya Nation Media Group
Mkurugenzi Mkuu: **JOE MUGANDA**
Mhariri Mkuu: **TOM MSHINDI**
Mhariri Msimamizi: **NICHOLAS MUEMA**

TAIFA LEO

NATION CENTRE KIMATHI STREET NAIROBI 9/02/2016

# Wabunge wafisadi pia nao wafuatwe

BUNGE linaporejelea vikao vyake leo, Wakenya wengi wanasubiri kujua jinsi watakavyoendesha shughuli zao, wakiwa wamegubikwa na wingu la madai ya ufisadi.

Siku ya Jumapili, mashirika ya umma yalizindua kampeni ya kushinikiza hatua za kisheria zikuchukuliwe dhidi ya wabunge waliohusishwa na kashfa mbalimbali za ufisadi jinsi inavyofanyika katika serikali kuu na idara ya mahakama.

Chini ya mwavuli wa Muungano wa Mashirika ya Umma (NCSC), viongozi wa mashirika hayo walitoa makataa ya wiki mbili kwa Tume ya Maadili na Kupambana na Ufisadi (EACC), itoe ripoti yake ya uchunguzi kuhusu wabunge fisadi, la sivyo waelekee kortini kushinikiza kutolewa kwa ripoti iliyowahusisha na ufisadi.

Walisema ripoti hiyo ikitolewa kwa umma itakuwa rahisi kwa NCSC kuwashtaki wabunge waliotajwa kwayo ili "kuzuia wizi wa mali ya umma".

Na kwa hakika mashirika hayo yana hoja muhimu katika suala hili. Wakati mawaziri wa serikali walipotajwa katika kashfa za ufisadi, walisimamishwa kazi, watashtakiwa na hata kufutwa kazi. Wakati huu katika idara ya mahakama, Jaji wa Mahakama ya Juu Philip Tunoi anapigwa anamulikwa kuhusiana na uovu sawa na huo.

Kinachoshangaza ni kwamba, wabunge wanapotuhumiwa katika masuala ya ufisadi, au wanapotajwa kwenye ripoti ya EACC, hakuna anayeshughulika kuwaandama.

Inafahamika kuwa ripoti ya EACC iliwasilishwa kwa Spika wa Bunge la Kitaifa, Bw Justin Muturi mwaka jana. Awali, Bw Muturi alikiri madai ya kwamba baadhi ya wabunge waliitisha pesa za matuta, au kuandikisha kuwa walihudhuria vikao ilhali ni uongo.

Lakini wabunge hao walipotisha kumchukulia hatua, alibadili msimamo wake na kuwatetea akisema ripoti hiyo haikuwa na uzito.

Itakuwa vigumu kushinda vita ufisadi ikiwa wabunge wanaoshiriki uovu huo hawatachukuliwa hatua za kisheria.

Spika Muturi anapaswa kuonyesha uwajibikaji kuhusu suala hili jinsi Rais Uhuru Kenyatta na Jaji Mkuu Willy Mutunga walivyofanya kwa maafisa katika idara wanazosimamia moja kwa moja.

Kuwaruhusu wabunge kuendelea kufuja pesa za mlipa ushuru bila ya kujali kuchukuliwa hatua, kutafanya Wakenya waamini kuwa ufisadi ni jambo la kawaida. Hili ni jambo ambalo lisiposhughulikiwa ipasavyo, litaangamiza kabisa uchumi, maadili na utaifa wa Kenya.

Ni Gazeti la Kampuni ya Nation Media Group
Mkurugenzi Mkuu: **JOE MUGANDA**
Mhariri Mkuu: **TOM MSHINDI**
Mhariri Msimamizi: **NICHOLAS MUEMA**

TAIFA LEO

NATION CENTRE KIMATHI STREET NAIROBI 10/02/2016

# NPSC: Madai ya hongo ni hatari

MADAI kuwa baadhi ya maafisa wa Tume ya Kitaifa ya Huduma kwa Polisi (NPSC) wamekuwa wakipokea hongo kutoka kwa maafisa wa polisi ambao maadili yao yanatiliwa shaka, yanafaa kuchunguzwa.

Kulingana na madai hayo, maafisa wa NPSC wanaochunguza polisi wamekuwa wakipokea hongo ya kati ya Sh300,000 na Sh500,000 ili kuruhusu maafisa wenye maadili ya kutiliwa shaka kuendelea kuhudumu.

Mamlaka ya Kuchunguza Utendakazi wa Maafisa wa Polisi (IPOA) pia imekiri kupokea malalamishi kuhusiana na madai ya kuwepo kwa visa vya ufisadi katika shughuli hiyo inayoendelea ya kuwapiga msasa zaidi ya maafisa 77,400 wa polisi. IPOA, hata hivyo, imekiri kuwa naina mamlaka ya kufanya uchunguzi dhidi ya NPSC.

Tangu mwaka wa 2014 tume ya NPSC imekuwa ikichunguza maafisa wa ngazi za juu katika idara ya polisi ambapo zaidi ya maafisa 1,200 wameruhusiwa kuendelea kuhudumu na wengine zaidi ya 60 wakaachishwa kazi.

Shughuli ya kuchunguza idadi kubwa ya maafisa wa polisi bila shaka hukumbana na changamoto tele, yakiwemo madai ya ufisadi na upendeleo haswa kutoka kwa wale wasioridhika.

Kulingana na mwenyekiti wa NPSC, Johnston Kavuludi, madai hayo yanalenga kutatiza shughuli ianayoendelea ya kuchunguza maadili ya maafisa wa polisi. Mwenyekiti anasisitiza kuwa tume inaendesha majukumu yake kwa uadilifu.

Bw Kavuludi pia amejitokeza na kusema kuwa maafisa wa tume hiyo wamekuwa wakipokea vitisho kutoka kwa watu wasiojulikana. Bw

Japo madai hayo huenda yasiwe ya kweli, kuna haja ya Tume ya Maadili na Kupambana na Ufisadi (EACC) kufanya uchunguzi wake ili kuthibitisha ikiwa kuna ukweli au la. Ikiwa NPSC itaruhusu idara husika kufanya ~~kufanya~~ uchunguzi, maafisa wa polisi wanaochunguzwa na Wakenya kwa ujumla watapata hakikisho kuwa shughuli hiyo ni ya haki na wazi.

Hatua hiyo pia itasaudia kudumisha hadhi ya tume ya NPSC inayochunguza maafisa wa polisi.

Kadhalika, maafisa polisi walio na ushahidi kuhusiana na madai kwamba maafisa wa NPSC wanapokea hongo, wanafaa kujitokeza

TAIFA LEO
NATION CENTRE KIMATHI STREET NAIROBI 12/02/2016

# Pesa zilizookolewa ziendee maendeleo

HATUA ya serikali kuamua kupunguza kwa asilimia 50 bajeti inayotumiwa kwa usafiri wa maafisa wakuu wa umma ni ya kupongezwa.

Maafisa wakuu wa umma wamekuwa, kwa muda mrefu, wakitumia vibaya pesa katika usafiri ambao hausaidii wananchi kwa njia yoyote.

Tangu serikali za ugatuzi zilipoanza kuhudumia taifa baada ya mwaka wa 2013, mojawapo ya changamoto kubwa zaidi imehusu utumizi mbaya wa pesa hasa na madiwani.

Tumeshuhudia safari za ng'ambo ambazo hazina umuhimu wowote, kwa kiwango ambacho hata baadhi ya mataifa ya kigeni yalipiga marufuku madiwani kuzuru nchi hizo.

Si madiwani pekee wanaofaa kulaumiwa bali pia viongozi wengine katika bunge la kitaifa, seneti, afisi ya rais na hata katika idara ya mahakama.

Changamoto iliyopo sasa ni kuhakikisha kuwa pesa zitakazookolewa kutokana na hatua hiyo, hazitaishia mifukoni mwa watu binafsi.

Tunatarajia mamilioni ya pesa ambazo zilitumiwa kupumbaza maafisa wa umma kwa kuwaruhusu kusafiri nje ya nchi mara kwa mara bila sababu, sasa zitapata kutumiwa katika miradi muhimu itakayoendeleza mbele maendeleo.

Miradi mingi ya maendeleo inasubiriwa kutekelezwa na wananchi hasa katika sekta za afya, elimu na kilimo ambazo ndizo huleta matumaini makubwa kwa maisha bora ya wananchi.

Tungependa kuona maafisa wakuu katika serikali za kaunti na katika serikali kuu wakiweka mikakati inayolenga kutumia pesa hizo kwa miradi itakayosaidia wananchi.

Itakuwa aibu ikiwa utawala uliopo utakumbukwa kwa kufanya safari nyingi zaidi nje ya nchi bila kujali maslahi ya wananchi.

Hivyo basi mwaka mmoja uliosalia kabla uchaguzi mkuu uandaliwe unafaa kutumiwa kuonyesha wananchi kuwa hawakukosea kuchagua viongozi wao kwenye uchaguzi mkuu uliopita.

Wananchi pia wanahitaji kuonyeshwa kuwa hawakukosea walipopitisha kwa wingi katiba mpya mwaka wa 2010, iliyosababisha kuundwa kwa serikali za kaunti.

Badala yake, ndoto ya wananchi kuhusu kuletewa maendeleo karibu nao, yafaa ianze kuonyesha dalili za kutimia.

Ni Gazeti la Kampuni ya Nation Media Group
Mkurugenzi Mkuu: **JOE MUGANDA**
Mhariri Mkuu: **TOM MSHINDI**
Mhariri Msimamizi: **NICHOLAS MUEMA**

TAIFA LEO

NATION CENTRE KIMATHI STREET NAIROBI

15/02/2016

# Tujitokeze vituoni tuwe wapigakura

SHUGHULI ya kuwaandikisha watu kuwa wapiga kura inaanza rasmi leo kote nchini.

Usajili huu unaoendelezwa na Tume Huru ya Uchaguzi na Mipaka (IEBC), unalenga kuhakikisha kuwa kuwa mamilioni ya vijana waliopata vitambulisho baada ya Uchaguzi Mkuu wa 2013, wanapata fursa ya kujiandaa kushiriki kwenye Uchaguzi Mkuu ujao.

Hii ina maana kuwa Wakenya wasiopungua milioni nne wanatarajiwa kuandikishwa kuwa wapiga kura, kati ya leo na Machi 15.

Mwenyekiti wa IEBC Bw Issack Hassan anatarajiwa kuongoza uzinduzi rasmi wa zoezi hilo katika ukumbi wa kijamii wa Pumwani, eneo bunge la Kamukunji, Nairobi leo asubuhi.

Kuzinduliwa kwa usajili huo kunaashiria kuanza kwa safari ya kuelekea kwenye Uchaguzi Mkuu wa 2017.

Usajili huo umekumbwa na pingamizi kutoka upande wa upinzani, hasa kufuatia madai kuwa maeneo yenye idadi kubwa ya watu waliohitimu kuwa wapigakura, yalivyotengewa vifaa vichache vya usajili ikilinganishwa na maeneo yenye watu wachache.

Madai hayo ya Mkurugenzi wa Uchaguzi katika ODM, Bw Junet Mohamed yametolewa wakati ambapo IEBC imekariri kuwa inazingatia ukubwa wa maeneo wala si idadi ya watu.

Kauli ya meneja wa Mawasiliano wa IEBC, Bi Tabitha Mutemi haionekani kuaminika na kila mdau kwenye shughuli hii ya uchaguzi. Kwa mfano haieleweki ni vipi maeneo mengi yaliyopokea vifaa vichache ni ya muungano wa Cord au vyama vingine vya upinzani.

Bi Muteni alieleza kuwa IEBC ilizingatia ukubwa wa wadi ilipogawa vifaa hivyo. Wadi zenye ukubwa wa kilomita 30 kwa mraba kwenda chini zilikabidhiwa kifaa kimoja, na zilizo kilomita kati ya 31 na 500 zikapewa vifaa viwili. Ikiwa huo ni ukweli, basi lazima madai ya Bw Junet kwamba takwimu za Nyanza, Magharibi na Pwani zinatofautiana pakubwa na zile za Kati na Rift Valley, yachunguzwe.

Changamoto nyingine ni ya maelfu ya Wakenya ambao hawajachukua vitambulisho vyao. Majuzi tulielezwa kuwa zaidi ya vitambulisho 500,000 viko katika afisi za usajili wa watu kote nchini.

Serikali yapaswa kuanzisha mbinu ya kuhakikisha kila aliyetuma maombi, anapewa kitambulisho chake kwa wakati. Aidha, Wizara ya Mambo ya Ndani inapaswa kutii amri ya Rais Uhuru Kenyatta na kuharakisha kumpatia kitambulisho kila Mkenya aliyehitimisha umri wa miaka 18, ili wapate kujisajili kupiga kura.

Tunahimiza watu wajitokeze kujisajili, bila kungoja kuhongwa.

Ni Gazeti la Kampuni ya Nation Media Group
Mkurugenzi Mkuu: **JOE MUGANDA**
Mhariri Mkuu: **TOM MSHINDI**
Mhariri Msimamizi: **NICHOLAS MUEMA**

TAIFA LEO

NATION CENTRE KIMATHI STREET NAIROBI

16/02/2016

# Kuwapa wakulima masoko hakutoshi

KILIMO kwa miaka mingi kimechukuliwa kuwa uti wa mgongo wa nchi yetu.

Si Kenya pekee ambapo kilimo ni muhimu, bali kote ulimwenguni, hakuna nchi inayoweza kulisha watu wake bila kutilia mkazo kuhusu kilimo.

Lakini kwa bahati mbaya, kwa miaka mingi wakulima humu nchini wamekuwa wakimenyeka juani, huku wahuni wachache wakifurahia jasho lao kivulini.

Watu ambao wamekuwa wakinunua kwa niaba ya wanunuzi halisi, wamekuwa donda ndugu na chanzo cha kufilisika kwa wakulima kote nchini.

Jamaa hawa hata sasa wanaendelea na mbinu ambapo hujipeleka kwa wakulima na kununua bidhaa zao kwa bei ya chini, kabla ya kuziuza kwenye masoko kwa bei maradufu.

Kwa hivyo tangazo la Waziri wa Kilimo, Bw Willy Bett kwamba serikali inapanga kuwaanzishia wakulima masoko, ni la kufurahisha.

Kwa mujibu wa waziri Bett, wakulima watakuwa wakiuza mazao yao moja kwa moja kwenye masoko, badala ya kutegemea watu wengine kuyanunua na kuyapeleka kwenye masoko.

Waziri alisema ni jambo la kuhuzunisha kwamba wakulima, ambao ndio wanaomenyeka zaidi katika shughuli ya kuwatafutia watu riziki, huishia kuwa hohehahe bila ya pesa mifukoni. Kinyume chake, watu ambao hawajui hata jembe linavyoshikwa, ndio wanaofurahia manoti na faida kubwa.

Jambo hilo limekuwepo miaka nenda, miaka rudi. Serikali pia imekuwa ikifahamu ulaghai unaoendeshwa na watu wanaowapunja wakulima. Kwa hivyo, ni matumaini ya Wakenya kwamba sasa wakulima watakuwa wakipata faida wanayostahili.

Mpango huu wa serikali unastahili kuharakishwa hata sasa. hata hivyo, serikali pia yapaswa kuangazia masuala mengine yanayowakumba wakulima.

Mojawapo ni bei ghali ya pembejeo za kilimo. Wakulima wengi wameacha kilimo cha kahawa, majani chai, pareto, tumbaku, miwa na mazao mengine kutokana na gharama ya kuendeleza kilimo.

Kwa hivyo, wakati inapowatafutia masoko ya moja kwa moja, itakuwa vyema pia iwapo itahakikisha kuwa, mbolea ya bei nafuu pamoja na matingatinga miongoni mwa vifaa vingine vya shambani, vinapatikana kwa bei nafuu kwa wakulima.

Ni Gazeti la Kampuni ya Nation Media Group
Mkurugenzi Mkuu: **JOE MUGANDA**
Mhariri Mkuu: **TOM MSHINDI**
Mhariri Msimamizi: **NICHOLAS MUEMA**

TAIFA LEO
NATION CENTRE KIMATHI STREET NAIROBI
19/02/2016

# Madai ya ufisadi sasa yanachosha

TAASISI zote za serikali zinazohusika katika vita dhidi ya ufisadi zinafaa kuthibitishia wananchi kuwa zimejitolea kikamilifu kutekeleza majukumu yao.

Madai mapya ya majuzi zaidi kuhusu sakata ya ufisadi katika shirika la Huduma ya Vijana kwa Taifa (NYS) yametoa picha mbaya kwa Tume ya Maadili na Kukabiliana na Ufisadi (EACC) na Idara ya Upelelezi wa Jinai (DCI).

Hii ni kutokana na kuwa waliotajwa upya kwenye sakata hiyo, akiwemo aliyekuwa Waziri wa Ugatuzi Bi Anne Waiguru, walikuwa tayari wametangazwa kutokuwa na hatia yoyote.

Jambo hili limetilia doa EACC ambayo imelazimishwa kuchunguza upya madai dhidi ya waziri huyo wa zamani, licha ya kuwa awali iiikuwa imesema haikupata ushahidi wa kumhusisha na sakata hiyo.

Ingawa bado yanayofichuliwa ni madai ambayo hayajathibitishwa kama yana ukweli ndani yake, suala la kuwa kuna dai kubwa kiasi hicho ambalo halikuwa limechunguzwa awali linaondoa matumaini kwa wananchi kuwa vita dhidi ya ufisadi vitashindwa hivi karibuni.

Tume hiyo ilitarajiwa ingetumia rasilimali zake kufanya uchunguzi wa kina na hapangekuwa na mapengo kama yale yaliyodhihirika hivi sasa.

Kutajwa kwa maafisa wa DCI katika sakata hiyo pia kunaleta picha mbaya kuhusu juhudi za serikali kukabiliana na janga hilo ambalo linasababisha hasara kubwa kwa wananchi.

Taasisi hizo zitahitajika kujikakamua kuhakikishia wananchi kuwa zimejitolea kukabiliana na ufisadi katika idara za serikali.

Tunatarajia uchunguzi utafanywa kikamilifu safari hii, na hatua zitachukuliwa dhidi ya wale wote watakaopatikana na hatia bila kubagua yeyote kisiasa wala kimamlaka.

Wananchi wamechoshwa na jinsi wanavyozungushwa kwenye mviringo wa madai ya ufisadi kila mara bila kuona mtu yeyote akiadhibiwa kisheria.

EACC haifai kuonekana kama jibwa linalobweka bila kung'ata, hata wakati ambapo linahitajika kuzuia maadui wa maendeleo kufanya mambo ambayo yanaathiri vibaya maisha ya wananchi wa kawaida.

TAIFA LEO

NATION CENTRE KIMATHI STREET NAIROBI

20/02/2016

# Gor na Bandari wasituletee aibu

Kama desturi, klabu za Kenya zinaelekea kuleta aibu kwenye soka ya Shirikisho la Afrika (CAF). Hii ilionekana wiki jana baada ya Gor Mahia na Bandari FC kutandikwa na timu pinzani kwenye mashindano ya Klabu Bingwa Afrika na Kombe la Mashirikisho ya Afrika, mtawalia.

Hata hivyo, bado kuna nafasi ya klabu hizi kuwaondolea Wakenya na hasa mashabiki aibu na mahangaiko ya kifikra kwa kupindua matokeo hayo mabovu.

Gor ambayo ilitandikwa na CNaPS ya Bukini mabao 2-1 jijini Nairobi, itahitaji kufunga 2-0 au 3-1 ndipo ifuzu kwa hatua ijayo nayo Bandari iliyochapwa 2-0 na Saint Eloi Lupopo ya Jamhuri ya Congo mjini Lubumbashi, italazimika kutumia uwanja wa nyumbani vizuri ili kufunga angaa magoli 3-0 au 4-1 ndipo ijihakikishie nafasi ya kusonga mbele.

Ni zamani sana tangu klabu ya Kenya ivuke hatua hii ya mchujo kwenye mashindano hayo mawili. Ilikuwa Sofapaka iliyotandika timu nyingi tena mahiri zikiwemo Atletico Sports Aviacao ya Angola, Ismaily ya Misri na St Eloi Lupopo -kabla ya kulemewa na Club Africain ya Tunisia -hadi ikafika raundi ya tatu ya soka ya Mashirikisho ya Caf mnamo 2011.

Huu ndio ufanisi mkubwa zaidi kwa taifa hili tangu Gor Mahia ishinde kandanda ya Caf Cup Winners mnamo 1987 ambapo K'Ogalo ililaza Esperance ya Tunisia na kutwaa kombe hilo kihistoria.

Hii ndiyo sababu Wakenya wamejaa shauku kuu ya ama kushinda soka yoyote ile ya kiwango cha bara au angaa kupiga hatua ya kuridhisha -Gor na Bandari wang'amue hilo.

Hakuna njia nyingine mbadala ila kuwapa mashabiki furaha kwa kupindua matokeo hayo waliyopata kwenye duru ya kwanza ya mchujo wa mashindano hayo wikendi iliyopita.

Gor na Bandari hawana sababu ya kutotimiza hilo hasa inapozingatiwa kuwa tatizo la kifedha hasa kwa Gor Mahia limepungua baada ya kupata ufadhili mzuri kutoka kwa shirika la kibahati nasibu la SportPesa. Na inapozingatiwa kuwa CNaPS ni timu ndogo, basi K'Ogalo wanastahili kuwapa mashabiki wake sababu ya kuendelea kuwaunga mkono.

Bandari, tatizo haliko upande wa fedha hasa na hivyo, hapana haja ya kukosa kujitolea hata ingawa wanakibiliana na timu ngumu kiasi. Kwa ufupi, Kenya haiko tayari kupata aibu mara hii.

Ni Gazeti la Kampuni ya Nation Media Group
Mkurugenzi Mkuu: **JOE MUGANDA**
Mhariri Mkuu: **TOM MSHINDI**
Mhariri Msimamizi: **NICHOLAS MUEMA**

TAIFA Jumapili

NATION CENTRE KIMATHI STREET NAIROBI

21/02/2016

# Ukatili katika siasa Uganda haufai kitu

UCHAGUZI Mkuu wa urais nchini Uganda ulikamilika jana, huku Rais Yoweri Kaguta Museveni akitangazwa mshindi dhidi ya mpinzani wake mkuu Dkt Kizza Besigye.

Ijapokuwa hakuna visa vikubwa vya ghasia vilivyoripotiwa, kuna mapungufu kadhaa yaliyojitokeza ambayo yanapaswa kukemewa.

Kwanza, polisi walionekana wakitumia nguvu kuwahangaisha wafuasi wa Dkt Besigye, huku wakimkamata mara tatu kwa wiki moja, wakitaja hatua yao katili kama "kulinda usalama wa taifa."

Pili, walionekana hata wakitumia vitoa machozi kuwatawanya wafuasi hao, kwa kiwango hata cha kutumia bunduki ili kuwatisha.

Kimsingi, lawama za moja kwa moja zinaelekezwa kwa Serikali ya Rais Museveni kwa kuonekana kutumia nguvu na ukatili dhidi ya Upinzani.

Kutokana na matukio hayo, Kenya na nchi nyinginezo barani zinafaa kufahamu kuwa chaguzi za urais ni muhimu sana kwani huwa zinawakilisha sauti na matakwa ya raia.

Upigaji kura huwa ndiyo njia ya pekee kwa wananchi kuwaweka mamlakani viongozi wanaowataka na kuwaondoa wale ambao wanahisi kutofurahishwa na utendakazi wao.

Inapojitayarisha kuandaa Uchaguzi Mkuu wa 2017, Tume Huru ya Uchaguzi na Mipaka (IEBC) inapaswa kudhihirisha uhuru wa kiutendakazi bila kuegemea upande wowote ule.

Ikizingatiwa kwamba mgawanyiko wetu wa kisisa huwa mzito sana, IEBC inapaswa kufahamu kwamba kosa lolote la kimapendeleo huenda likazua ghasia na machafuko ya kikabila kama ilivyoshuhudiwa mnamo 2007/2008.

Kwa upande mwingine, Serikali pia inapaswa kuhakikisha kwamba haitumii vyombo vya dola kuuhangaisha Upinzani.

Na maadamu uchaguzi wowote huwa ushindani wa kisiasa, pande zote zinapaswa kuheshimiana; kwa kuendesha kampeni zake bila mwingiliano wowote.

Ikiwa ni kukosoana, si lazima Serikali itumie vikosi vya usalama kuuhangaisha Upinzani, au viongozi wa Upinzani kuanza kuwatukana wenzao Serikalini.

Ikumbukwe kuwa wakati wowote vurugu hutokea, wananchi ndio huwa wanaumia zaidi; hasa akina mama na watoto.

Kwa hivyo, wito wetu ni kwa raia wa Uganda kuendelea kudumisha amani kwa msingi wa mustakabali mwema na ufanisi wa taifa.

TAIFA LEO
NATION CENTRE KIMATHI STREET NAIROBI

22/02/2016

# Tutalipa wabunge Sh2b za kazi gani?

UFICHUZI kwamba wabunge wetu wamekubaliana walipwe mshahara wa miezi minane ambapo hawatakuwa bungeni unasikitisha.

Imebainika kuwa, walikuwa mjini Mombasa mwishoni mwa wiki, wabunge waliafikiana kuunga mkono pendekezo la mmoja wao kwamba walipwe mshahara wa miezi ambapo kisheria wangetarajiwa kuwa kazini.

Wanasema kwa vile walianza kazi Machi 2013, miaka mitano itakamilika Machi 2018. Lakini kwa vile Katiba inasema Uchaguzi Mkuu wa kuanzia 2017 unapaswa kuwa Jumanne ya pili ya mwezi Agosti, kipindi chao hakitadumu kwa miaka mitano.

Awali wabunge hao walijaribu kila mbinu kurefusha muda wa bunge la sasa ili angalau wafikishe Disemba, lakini jaribio hilo likagonga mwamba.

Baada ya mbinu zote kushindwa, sasa wanajiamulia kwamba ni lazima kila mbunge alipwe pesa za kuanzia Agosti hadi Machi. Wao peke yao pamoja na maseneta watafikisha zaidi ya Shilingi Bilioni mbili. Lakini wasiwasi ni kuwa, wakipitisha pesa hizo, wawakilishi wa wadi zaidi ya 1,300 nao watataka walipwe karibu Sh1 milioni kila mmoja kwa muda huo. Isitoshe, kuna magaana 47 ambao mshahara wao ni Sh1.1 milioni.

Japo magavana hawajasema chochote kuhusu mpango huo, ni wazi kuwa sheria haiwabagui, na kwa hivyo wote watalipwa sawa na wenzao walioingia uongozini wakati sawa.

Mpango huu wa wabunge ni ulafi na kutaka kujifanya wao ni bora kuliko Wakenya wengine. Ni majuzi tu ambapo Tume ya Kuajiri Walimu (TSC) ilikataa agizo la mahakama la kuwalipa walimu mshahara wao wa mwezi mzima, kwa dai kuwa hawakuwa kazini. Wakati huo walimu walipokuwa na mgomo, serikali ilikataa kuwalipa.

Sasa inakuwaje wabunge wataidhinisha walipwe mshahara kwa miezi minane ambapo Wakenya watakuwa wameshaamua kuwa mkataba wao umemalizika?

Miaka miwili iliyopita wabunge walipopanga kujiongeza mshahara, Wakenya walipiga kelele lakini wakawapuuza. Tunatumai kuwa safari hii, Wakenya watatumia silaha muhimu ya kura, kuzuia ulafi huu ambao umepita mipaka.

Kwani Kenya ina utajiri kiasi gani, hata iwalipe mshahara zaidi ya watu 1,500 kwa miezi minane wakiwa hawafanyi kazi yoyote ya kuwatumikia wananchi?

Ni Gazeti la Kampuni ya Nation Media Group
Mkurugenzi Mkuu: **JOE MUGANDA**
Mhariri Mkuu: **TOM MSHINDI**
Mhariri Msimamizi: **NICHOLAS MUEMA**

TAIFA LEO

NATION CENTRE KIMATHI STREET NAIROBI

24/02/2016

# Rubani ashtakiwe lakini tusimbague

TUKIO ambapo rubani wa ndege ya Naibu wa Rais William Ruto alinaswa kwenye video akimpiga polisi imeibua suala la kiwango cha usalama anachopewa naibu wa rais.

Katika video hiyo, helikopta iliyokuwa ikimsafirisha Bw Ruto ilionekana ikiwa imeegeshwa bila ulinzi wowote wa kuridhisha, isipokuwa kuwepo kwa polisi ambao inaaminika walihitajika kudhibiti umati mkubwa uliokuwepo.

Ni ukosefu huo wa ulinzi ambao ulisababisha umati, wengi wao wakiwa watoto, kukimbilia na kuzingira ndege hiyo.

Katika hali kama hii, maisha ya naibu wa rais ambaye ndiye wa pili kwa mamlaka ya uongozi wa taifa yangekuwa hatarini kama kungekuwa na mtu yeyote mwenye njama ya kumdhuru kwa kusababishia ndege hiyo hitilafu ya aina yoyote.

Huenda hii ni mojawapo ya sababu zilizompelekea rubani huyo kushikwa na ghadhabu kiasi kwamba akampiga polisi wa kike aliyekuwa karibu, akimtaka afanye kazi yake badala ya kuchezea simu ya mkononi.

Machoni mwa Wakenya wengi, rubani huyo hakuwa na haki ya kuchukua hatua mikononi mwake, na wengi waliharakisha kuamua alifanya vile kwa misingi ya ukoloni mamboleo.

Tunachofaa kukashifu hakifai kuzingatia pakubwa rangi ya mwili wa rubani huo, wala sio tu kwa sababu aliyempiga alikuwa polisi na kuzidi hayo ni mwanamke, bali hata kama angekuwa ni raia wa kawaida hakustahili kupigwa.

Ni matumaini yetu kuwa uchunguzi wa kina utafanywa kubainisha chanzo cha yale yaliyoshuhudiwa na hatua za kisheria zinazohitajika zitachukuliwa ipasavyo bila ubaguzi.

Wananchi wasiwe na pupa kumhukumu rubani huyo na kutaka arudishwe kwao kabla ukweli wote ubainike.

Kazi hiyo iachiwe idara husika za kiserikali ikiwemo mahakama.

Zaidi ya hayo, ulinzi wa kiongozi mwenye hadhi kubwa nchini kama ya naibu wa rais haifai kufanyiwa mzaha.

Idara ya polisi inafaa kupiga msasa mbinu zake za kutoa ulinzi kwa naibu wa rais na vyombo vyake vya usafiri anapoenda kufanya mikutano ya hadhara mashinani.

Ihakikishe maafisa wanaotwikwa jukumu hilo wana uwezo wa kutosha kuzuia njama yoyote ambayo inaweza kusababisha taharuki kitaifa.

Ni Gazeti la Kampuni ya Nation Media Group
Mkurugenzi Mkuu: **JOE MUGANDA**
Mhariri Mkuu: **TOM MSHINDI**
Mhariri Msimamizi: **NICHOLAS MUEMA**

TAIFA LEO

NATION CENTRE KIMATHI STREET NAIROBI 27/02/2016

# Karata ya kinara wa FKF si hakika

HUWA aghalabu busara mtu kujivunia kitu chake mwenyewe. Na hivyo ndivyo alivyoanza kuashiria rais wa shirikisho la soka nchini (FKF), Nick Mwendwa.

Kinara huyo wa kabumbu wiki hii alimteua kocha mzawa Stanley Okumbi kutwaa mikoba ya Bobby Williamson ambaye amedumu kama kocha wa Harambee Stars kwa takriban miaka miwili.

Hata ingawa msimamo wa Mwendwa huenda ukawa mzuri kwa kiwango fulani, yamkini nchi hii itakosa kupiga hatua ya maana kutokana na sababu mbalimbali kumhusu na kocha huyo.

Waama kocha mzawa anaelewa vyema kabumbu ya humu nchini kuliko mkufunzi yeyote yule kutoka nje. Lakini ukweli ni kwamba inawezekana kocha huyo mzawa hana tajriba, welewa na maarifa ya kutosha kufikisha Harambee Stars mahali ambapo mashabiki wengi wanatamani ifike -katika fainali za Kombe la Afrika na Dunia.

Mapungufu ya kocha huyu yanahusiana hasa na ukweli kwamba hajawahi kufundisha timu ya kiwango hiki. Ujuzi wake kama mkufunzi wa Harambee Stars Under-23 na klabu ya Mathare United huenda usitoshe kujenga timu ya kitaifa yenye uwezo wa kutetemesha mahasimu kwenye mashindano ya kimataifa.

Kihistoria, ni makocha wachache sana wazawa ambao wamewahi kufaulu kiasi cha kuridhisha wakiwa na kikosi cha taifa. Marshall Mulwa, Jacob 'Ghost' Mulee na Francis Kimanzi wanaweza kutajwa kama miongoni mwa wakufunzi wachache wazawa waliowahi kusaidia Harambee kupiga hatua ya maana.

Wengine wote hawana wajuacho isipokuwa mapendeleo au ukosefu wa upana wa mawazo katika uteuzi wa kikosi cha taifa, upangaji mechi kwa ajili milungula na mienendo mingine isiyoadilifu.

Lakini kwa upande mwingine, makocha wa kigeni hasa kutoka Ulaya, licha ya kuhitaji mshahara mkubwa, wamekuwa wakizua athari ya maana si kwa timu ya taifa tu bali hata kwa klabu.

Izingatiwe pia kuwa timu nyingi za kitaifa barani zinazofaulu kwenye mashindano ya hadhi ya juu aghalabu huwatumia makocha wa kigeni kufanikiwa. Naam inaeleweka kwamba kwa sasa kuna upungufu mkubwa wa kuendeshea soka hapa Kenya, ikiwemo kulipa maafisa wa benchi la ufundi ila isisahaulike kuwa serikali ilikuwa imejitwika jukumu la kulipia Harambee mshahara wa kocha.

Labda hekima tunayoweza kufanya kwa sasa ni kusubiri kuona jinsi Okumbi atakavyotanikisha timu hii ndiposa ibainike iwapo mrithi kutoka ng'ambo atatafutwa au la.

TAIFA LEO

NATION CENTRE KIMATHI STREET NAIROBI 07/03/2016

# Wakazi wa Malindi na Kericho waepuke fujo

WANANCHI watakaoshiriki kwenye chaguzi ndogo za Malindi na Kericho leo yafaa wadumishe amani wakati wa uchaguzi na hata baada ya matokeo kutangazwa.

Chaguzi hizo zilivutia ushindani mkubwa kama ilivyooneka-na kwenye kampeni na bila shaka hiyo ni ishara ya ukomavu wa demokrasia nchini. Hata hivyo historia ya nchi inaonyesha katika chaguzi zenye ushindani mkubwa aina hiyo, mara nyingi ghasia huzuka uchaguzini au matokeo yakitangazwa.

Wakati mwingi ghasia hutokea kutokana na uchochezi unaosababishwa na viongozi wa kisiasa wenye ufuasi mkubwa zaidi.

Ushindani mkubwa umeonekana kati ya Bw Aaron Cheruiyot (Jubilee), na Paul Sang (Kanu) katika uchaguzi wa Useneta wa Kericho.

Kwingineko katika uchaguzi mdogo wa ubunge Malindi, ushindani mkubwa unatarajiwa kuwa kati ya Bw Willy Mtengo wa Chama cha ODM na Bw Philip Charo wa Chama cha Jubilee.

Inafaa polisi wawe macho katika kipindi hiki chote ili kiongozi yeyote na wafuasi wao watakaochochea wananchi au kuzua aina yoyote ya mtafaruku wachukuliwe hatua za haraka kisheria.

Wananchi wafahamu kuwa kama kutatokea ghasia za aina yoyote, viongozi wanaowachochea hawataathirika pakubwa bali ni maisha ya mwananchi wa kawaida ambayo yataathirika.

Viongozi wa kisiasa wataendelea kuwa na ulinzi ambao unalipwa na ushuru wa mwananchi wa kawaida, na familia zao zitazidi kuendelea na maisha ya kawaida bila matatizo kama ambavyo imekuwa ikishuhudiwa wakati ghasia za kisiasa zinapotokea.

Wananchi wawe wenye busara na kukumbuka katika enzi hii katiba imetoa mwelekeo wa jinsi ya kutatua malalamishi ya kisiasa kwa njia za kisheria.

Kwa upande wake, Tume Huru ya Uchaguzi na Mipaka (IEBC) pia ihakikishe mikakati yote imewekwa ili uchaguzi ufanywe kwa njia ya haki na uwazi bila kutoa sababu zozote zitakazopatia wanasiasa nafasi ya kuchochea wananchi.

Tume hiyo isikubali kuhangaishwa na upande wowote wa kisiasa, iwe ni upande wa serikali au upinzani.

Ni Gazeti la Kampuni ya Nation Media Group
Mkurugenzi Mkuu: **JOE MUGANDA**
Mhariri Mkuu: **TOM MSHINDI**
Mhariri Msimamizi: **NICHOLAS MUEMA**

TAIFA LEO
NATION CENTRE KIMATHI STREET NAIROBI
03/03/2016

# Makazi yajengwe kabla uajiri mpya

RAIS Uhuru Kenyatta ameagiza kusajiliwa kwa makurutu 10,000 wapya wa polisi ili kuimarisha hali ya usalama nchini.

Kufuzu kwa makurutu hao wapya Februari 2017 kunatarajiwa kuhakikisha Kenya imeafikia viwango vya Umoja wa Mataifa-polisi 400 kwa kila raia mmoja.

Agizo la Rais Kenyatta linajiri siku chache baada ya Mamlaka Huru ya kuchunguza Utendakazi wa Idara ya Polisi (IPOA)kutoa ripoti iliyoonyesha hali mbaya ya nyumba za polisi.

Ripoti hiyo ilisema takriban polisi 58,000 hawana nyumba mwafaka za kuishi hali ambayo ilisababisha maafisa wa polisi kujinyonga na kuchangia mizozo miongoni mwao.

Ni vyema rais kuzingatia ripoti ya IPOA kabla ya kuharakisha shughuli ya kuongeza maafisa wa polisi nchini.

Kando na changamoto za idadi ya polisi nchini, kuna matatizo mengine kama ya kulinda maslahi ya maafisa ambayo rais anapaswa kutilia maanani.

IPOA ilionya kuwa kuishi kwa mazingira mabovu kunaathiri kisaikolojia utendakazi wa polisi.

Ni bayana kuwa kusajiliwa kwa makurutu wapya katika Idara ya Polisi kutafanya hali kuwa mbaya zaidi iwapo suala la nyumba halitatatuliwa kikamilifu.

Ni aibu kuwa na idadi kubwa ya polisi ambao wanaishi kwa vyumba vidogo vinavyofinyana licha ya kuwa wengine wameoa na wana haki ya kulinda maisha yao ya kibinafsi.

Hali hii mbaya ya nyumba vilevile inaathiri polisi kupambana na matukio ya dharura kwa mujibu wa IPOA.

Kama inavyofanyika katika usimamizi wa wanajeshi, maafisa wa vyeo vya juu wa polisi wanapaswa kupewa marupurupu ya nyumba ili kutafuta makao maeneo ambayo si mbali na afisi zao ili kuwapa nafasi maafisa wa vyeo vya chini.

Serikali inapaswa kushirikiana na sekta ya kibinafsi kutoa vyumba vinavyowafaa maafisa wa polisi.

Hali hii pia itawapa maafisa wa polisi motisha ya kufanya kazi.

TAIFA LEO

NATION CENTRE KIMATHI STREET NAIROBI

17/03/2016

# Wakulima wapate usaidizi unaofaa

WAKULIMA wengi hasa kutoka maeneo ya Rift Valley wanaendelea kujitayarisha kwa msimu wa kupanda na kuna haja ya kupewa usaidizi wa kutosha kutoka idara husika za kilimo.

Maeneo ya Rift Valley na baadhi ya sehemu za Magharibi mwa nchi kuna utajiri mkubwa wa kilimo na ni sharti serikali itoe mandhari mazuri ili kuinua mazao.

Ni kweli wakulima wanakumbwa na changamoto za mabadiliko ya hali ya hewa lakini kuna utepetevu mkubwa kwa upande wa serikali kusaidia sekta ya kilimo nchini.

Kwa mfano masuala ya bei duni pamoja na kuongezeka kwa matapeli sokoni ni suala ambalo Bodi ya Kitaifa na Mazao na Nafaka (NCPB), imeshindwa kuepushia wakulima.

Ukweli mchungu ni kuwa kwa sasa Kenya haina chakula cha kutosha kulisha raia wake, na tunaendelea kutegemea vyakula kutoka nchi licha ya kuwa na raslimali zote za kukuza chakula cha kututosheleza.

Masuala yaliyowasilishwa na wakulima mbele ya kamati ya Bunge kuhusu Kilimo bado hayajatatuliwa.

Kwa mfano, serikali bado haijatekeleza kikamilifu ahadi yake ya kutoa mbolea kwa bei nafuu.

Isitoshe maghala ya NCPB kote nchini hayana mbolea ya kutosha licha ya kuwa huu ndio msimu wakulima wanahitaji mbolea kwa wingi wanaposubiri mvua kunyesha.

Baadhi ya matawi ya NCPB ambayo yana mbolea ya kadiri yamekumbwa na visa vya wizi wa bidhaa hiyo huku baadhi ya wasimamizi wakishtumiwa kwa ubaguzi wakati wa kuuza mbolea.

Serikali za kaunti vilevile zinapaswa kutengea sekta ya kilimo fedha zaidi ili kuhakikisha wakulima wanapata mbegu na vifaa vya kilimo virahisi bila kusafiri hadi miji mikuu.

Chini ya miaka miwili ikamilishe muhula wake wa mbili, serikali ya Jubilee haijateleza nyingi ya ahadi zake kuhusu kilimo.

Ni muhimu serikali iweke mikakati ya kutoa mafunzo kwa wakulima kuhusu mbinu za kisasa ili kuwapunguzia gharama na kuongeza mapato yao.

Mazao ya Kenya kama vile kahawa na chai yana hadhi kubwa katika masoko ya kimataifa na ni vyema kuwatia wakulima moyo kwa kutoa mandhari mazuri ya kiuchumi na kitaaluma.

Ni vyema pia wakulima wafunzwe jinsi ya kuhifadhi maji ya mvua.

Kilimo ni uti wa mgongo wa uchumi wetu na sharti upewe uzito na serikali za kaunti na ile kuu.

Ni Gazeti la Kampuni ya Nation Media Group
Mkurugenzi Mkuu: **JOE MUGANDA**
Mhariri Mkuu: **TOM MSHINDI**
Mhariri Msimamizi: **NICHOLAS MUEMA**

TAIFA LEO

NATION CENTRE KIMATHI STREET NAIROBI 18|03|2016

# Utajiri wa mafuta unufaishe wote

KUPATIKANA kwa kisima kingine cha mafuta eneo la Kerio Valley kunaipatia Kenya matumaini ya kujiunga na kundi la mataifa yenye utajiri mkubwa wa mafuta duniani.

Kuongezeka kwa idadi ya kampuni za kimataifa zinazosaka kandarasi ya uchimbaji madini na mafuta nchini ni ishara kwamba taifa hili limejaliwa raslimali nyingi.

Kufuatia hali hii, kuna haja ya Kenya kuweka misingi dhabiti ya kisheria na mbinu mahsusi za kufidia raia wanaoathirika na uchimbaji madini ili kuepuka mizozo inayoshuhudiwa katika mataifa mengine yenye utajiri huo.

Kabla ya mafuta, kuligunduliwa madini ya makaa eneo la Mui, Kaunti ya Kitui na mengine eneo la Kwale, lakini ufanisi wa uchimbaji wake umekwama kutokana na mizozo kuhusu fidia kati ya serikali na wenyeji.

Kenya bado ni ngeni katika sekta ya madini, hivyo changamoto zinazoshuhudiwa zinatokana na kutokuwepo na sheria mwafaka za kuongoza sekta hiyo.

Sharti serikali itoe mikakati na mwongozo wa uchimbaji madini na matuta kabla ya matapeli wa ughaibuni hawajaibuka na kugeuza Kenya kuwa kama mataifa ya Kiarabu ambayo yana utajiri mkubwa wa mafuta lakini wenyeji wanataabika kwa sababu ya mizozo.

Tayari kumeripotiwa kashfa za utoaji zabuni za uchimbaji madini hali iliyopelekea aliyekuwa Waziri wa Madini Najib Balala kufutilia mbali kandarasi za kampuni 42.

Baadhi ya maafisa wa serikali walidaiwa kupokea hongo ya Sh80 milioni ili kutoa leseni kwa kampuni fulani za kuchimba madini.

Sekta ya madini ni sekta muhimu ambayo haipaswi kuingizwa siasa zinazonuia kuwanyima Wakenya haki ya kunufaika na raslimali zao.

Ushindani mkubwa wa madini na mafuta unaendelea katika masoko ya kimataifa na sharti Kenya ijiweka katika nafasi ya kunufaika na bidhaa hizi badala ya kutegemea mazao ya kilimo pekee.

Wawekezaji wa kigeni wapewe mandhari mazuri ya kusaidia Kenya kuchimba madini lakini kwa kufuata kanuni na sheria za kulinda mali ya Wakenya.

Lakini kampuni za kigeni zinapopewa nafasi katika sekta hii, ni muhimu serikali itoe nafasi kwa kampuni na wataalamu wa humu nchini kujifunza kutoka kwa wenzao wa kigeni ili wawe katika kiwango sawa.

Ni Gazeti la Kampuni ya Nation Media Group
Mkurugenzi Mkuu: **JOE MUGANDA**
Mhariri Mkuu: **TOM MSHINDI**
Mhariri Msimamizi: **NICHOLAS MUEMA**

TAIFA LEO

NATION CENTRE KIMATHI STREET NAIROBI 21/03/2016.

# KCSE: Zipo sababu nyingine za kufeli

WALIMU wakuu wa shule za umma ambazo hazikufanya vyema kwenye mitihani ya kitaifa ya mwaka uliopita wanastahili kueleza kwa nini matokeo hayakuridhisha.

Ripoti zimetokea kuwa kuna mipango ya kuadhibu walimu hao, ingawa Wizara ya Elimu na Tume ya Kuajiri Walimu (TSC) zinafaa kujua matokeo ya wanafunzi hutegemea mambo mengi zaidi kuliko juhudi za walimu wakuu.

Hatuwatetei walimu wakuu wasio na bidii katika kazi zao, bali huenda wizara na TSC zikachukua hatua ambazo hazitatatua tatizo kuu lililopo. Si siri kuwa walimu katika shule za umma hufanya kazi katika mandhari duni mno, kuliko wenzao walio wa shule za kibinafsi.

Hali hii iligeuka kuwa mbaya zaidi kufuatia kuanzishwa kwa elimu bila malipo, ambayo ilipelekea idadi ya wanafunzi kuongezeka kupita kiasi katika shule za umma.

Wabunge wengi wamejitahidi kujenga madarasa zaidi na pia kufungua shule mpya katika maeneobunge yao kutokana na ongezeko la wanafunzi lakini bado changamoto za utoaji wa elimu bora zinakumba serikali.

Mojawapo ya matatizo makuu yanayokabili matokeo katika shule za umma ni kuwa hakuna walimu wa kutosha kuhudumia wanafunzi hao wengi ipasavyo.

Vyama vya walimu vimekuwa vikipigania suala hilo huku vikitaka serikali iajiri walimu zaidi hasa kuchukua mahali pa walimu wanaofariki, wanaostaafu na wanaoacha kazi kwa sababu zingine lakini hilo halijafanikishwa. Hii ni mojawapo ya masuala yanayohitaji kutatuliwa kando na kutilia mkazo zaidi hitaji la kuadhibu walimu wakuu.

Ukweli uliopo ni kuwa hapatakuwa na mabadiliko kwenye matokeo ya wanafunzi kama walimu wakuu watabadilishwa ilhali mandhari ya utoaji wa elimu bado ni mabovu. Kwa hivyo mbali na kuadhibu walimu wakuu watakaopatikana na hatia ya kutowajibika katika kazi zao, serikali ichukue hatua zaidi kwa kuboresha mandhari ya elimu katika shule za umma kote nchini.

Ni matumaini yetu kuwa ripoti ya jopo maalumu lililoteuliwa na Waziri wa Elimu Dkt Fred Matiang'i kuchunguza chanzo cha matokeo mabaya kwenye mtihani wa KCSE wa mwaka uliopita, itaangazia sababu zingine zilizoleta matokeo hayo mbali na ulegevu wa walimu.

Ni Gazeti la Kampuni ya Nation Media Group
Mkurugenzi Mkuu: **JOE MUGANDA**
Mhariri Mkuu: **TOM MSHINDI**
Mhariri Msimamizi: **NICHOLAS MUEMA**

TAIFA LEO

NATION CENTRE KIMATHI STREET NAIROBI 24/3/2016

# Majadiliano kati ya IEBC, Cord muhimu

Ni dhahiri kwamba muungano wa Cord haukufarahishwa na uamuzi wa Tume Huru ya Uchaguzi na Mipaka (IEBC) wa kukataa kuidhinisha pendekezo la kura ya maamuzi ya Okoa Kenya.

Hisia za Cord ni kwamba, muungano tawala wa Jubilee na IEBC zilishirikiana kuzima kura ya maamuzi ambayo Cord iliazimia kuandaa.

Nao viongozi wa Cord wamesema kwamba watarudi kwa wafuasi wao kutafuta ushauri zaidi, hali iliyofasiriwa kuashiria uwezekano wa kuzuka kwa maandamano mapya nchini.

Tunafahamu kuwa kuandamana ni haki ya kikatiba ya raia wote lakini inapasa kutekelezwa kwa kuzingatia sheria.

Humu nchini, maandamano yanahusishwa na ghasia na makabiliano makali kati ya waandamanaji na maafisa wa polisi na tuna hakika viongozi wa Cord wanaelewa hivyo.

Msimamo wetu ni kwamba hatua zozote ambazo pande zote zitachukua zisikoseshe Wakenya amani au kuharibu mali ya watu.

Ni wazi kwamba muungano wa Jubilee haukutaka kura ya maamuzi ya Okoa Kenya kufaulu lakini hakuna anayeweza kuthibitisha kwamba waliingilia shughuli ya kukagua sahihi ambazo Cord waliwasilisha kwa IEBC.

Litakuwa jambo la busara endapo viongozi wa Cord watawasiliana na IEBC ili waelezwe dosari zilizosababisha pendekezo lao kukataliwa.

Tume pia inaweza kuwaita viongozi wa upinzani na kuweka bayana mfumo uliotumiwa kukagua sahihi hizo. Kwa kufanya hivyo, tume itakuwa imezima maandamano ambayo upinzani huenda ukaandaa.

Na ikiwa tume haitawaita viongozi wa upinzani kwenye kikao kisha waamue kuandamana, polisi wanapasa kuhakikisha usalama.

Wito wetu ni kuwa hatua zichukuliwe kuepusha ghasia kwa sababu hali kama hiyo inaweza kutikisa uthabiti telezi tunaofurahia nchini kwa sasa.

Kenya ina mfumo wa sheria ambao ukifuatwa kikamilifu unaweza kutatua mambo mengi. Tulichozoea ni kusahau tulipotoka na tunapoelekea kama nchi.

Hivyo basi, kukataliwa kwa kura ya maamuzi, hakufai kutumiwa kuyumbisha taifa letu. Itakuwa bora wanasiasa kutoka mirengo yote kuepuka kuzungumzia suala hilo katika mikutano ya hadhara. Muhimu ni wote kufuata sheria.

Ni Gazeti la Kampuni ya Nation Media Group
Mkurugenzi Mkuu: **JOE MUGANDA**
Mhariri Mkuu: **TOM MSHINDI**
Mhariri Msimamizi: **NICHOLAS MUEMA**

TAIFA LEO

NATION CENTRE KIMATHI STREET NAIROBI 25|03|2016

# Sheria ya kuadhibu mafisadi itafaa zaidi

HATUA ya Baraza la Mawaziri kuidhinisha Mswada wa Rushwa 2015 ni ya kutia moyo lakini itakuwa na maana zaidi mswada huo ukianza kutekelezwa baada ya kuwa sheria.

Kuundwa kwa sheria inayojisimamia kukabiliana na ufisadi nchini kumeshangaza mataifa mengine lakini hatua hiyo inafaa kwa sababu ni bayana uovu huo umekuwa janga la kitaifa Kenya.

Mswada huo unatoa mapendekezo mazuri ya kupambana na ufisadi katika idara za serikali na pia ndani ya sekta ya kibinafsi.

Kulingana na Mswada huo, Wakenya au kampuni za humu nchini ambazo zitapatikana na hatia za kutoa au kupokea hongo katika mataifa ya kigeni watahukumiwa kulingana na sheria husika.

Wale ambao wana tabia ya kupeana hongo hasa kwa maafisa wa trafiki au idara za serikali, waadhibiwa vikali pia.

Kwa jumla Mswada huo wa Rushwa 2015 una dhamira nzuri ya kuhakikisha ufisadi umezimwa nchini lakini utekelezaji wake huenda ukasalia kitendawili kikubwa.

Kenya haina upungufu wa sheria kukabiliana na baadhi ya maovu lakini kujitolea kwa viongozi walio mamlaki kutekeleza sheria ndio kizingiti kikuu.

Kwa mfano, Serikali kuu pamoja na zile za kaunti zimeunda sheria kali kukabiliana na uuzaji na unywaji wa pombe haramu lakini visa hivyo vinaendelea kuripotiwa kila siku. Kisa na maana ni kuwa maafisa waliojukumiwa wamegeuka kuwa wavunjaji wa sheria zenyewe ili kujinufaisha kibinafsi.

Ufisadi ni zimwi ambalo kuzimwa kwake kutahitaji zaidi ya sheria kali.

Ni maradhi ambayo tayari yamesambaa katika damu za Wakenya pamoja na viongozi wao na tiba yake inahitaji tathmini ya vigezo vikuu vya kijamii.

Ukweli mchungu ni kuwa raia wa kawaida ndio wanapata hasara kubwa kutokana na ufisadi baada ya kukosa huduma muhimu kutoka kwa serikali.

Hatupingi kuundwa kwa sheria za kupambana na ufisadi lakini kuwe na azimio ya kweli pasipo kuunda sheria na kubakia maandishi kwenye karatasi tu.

Japo ufisadi umekitia mizizi nchini, habari nzuri ni kuwa tuna nafasi na uwezo wa kuutokomeza pakiwepo na kujitolea kutoka kwa viongozi pamoja na raia.

Ni Gazeti la Kampuni ya Nation Media Group
Mkurugenzi Mkuu: **JOE MUGANDA**
Mhariri Mkuu: **TOM MSHINDI**
Mhariri Msimamizi: **NICHOLAS MUEMA**